# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 28 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. SEIF ALI IDDI):-**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. DR. CYRIL A. CHAMI):-**

Taarifa ya mwaka ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kwa Mwaka 2004/2005 *(The Annual Report of the Arusha International Conference Centre for the Year 2004/2005)*

**MHE. JUMA H. KILIMBAH (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE):-**

Maoni ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 20062007.

**SPIKA:** Hongera sana Mheshimiwa Kilimbah kwa kusimama hapo mbele kwa mara ya kwanza. Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje

na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007:-

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa nakupongeza sana namna ulivyotoka leo. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge nitawatambulisha wageni mara baada ya kipindi cha maswali kwisha. Kwa hiyo, namwita Katibu tuingie katika hatua inayofuata.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 298

### Gari la Kubebea Wagonjwa

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kwa kuwa magari ya kubeba wagonjwa (*ambulance*) ni muhimu sana kwenye vituo vya afya, Hospitali za Wilaya, Mikoa na Hospitali za Rufaa na kwa kuwa, vipo vituo vya afya na Hospitali za Wilaya hapa nchini ambazo hazina magari ya kubeba wagonjwa- ikiwemo Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa na kituo cha afya cha Kibakwe kilichopo Wilayani Mpwapwa:-

(a) Je, ni vituo vya afya na hospitali za Wilaya ngapi hapa nchini ambazo hazina magari (*ambulance*) ya kubeba wagonjwa?

(b) Je, Serikali ina mipango gani wa kuhakikisha kwamba vituo vya afya na Hospitali za Wilaya hapa nchini ikiwemo hospitali za Wilaya ya Mpwapwa na kituo cha Kibakwe kilichopo Wilayani Mpwapwa vinapatiwa magari ya kubeba wagonjwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba magari ya kubebea wagonjwa (*ambulance*) ni muhimu sana. Aidha napenda nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu, kuwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 Serikali ilifanya zoezi la kujua mahitaji halisi ya magari kubeba wagonjwa katika vituo vya afya na hospitali za Wilaya kote nchini. Zoezi hilo lilibainisha kuwa kuna hospitali za Wilaya 52 na vituo vya afya 238 ambavyo havina magari ya kubeba wagonjwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo ya zoezi hilo Serikali imeanza kuchukua hatua za kutatua tatizo la upungufu wa magari ya kubebea wagonjwa kama ifuatavyo:-

Kwa mwaka wa fedha 2005/2006, jumla ya shilingi bilioni 1.5 zilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari 30. Magari hayo yamekwishanunuliwa na yatasambazwa kwenye Halmashauri kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa. Mwaka wa fedha 2006/2007, jumla ya shilingi bilioni 1.8 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ununuzi wa magari hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kutosheleza mahitaji ya wakati huu jumla ya mahitaji ya magari ni 290. Kwa sasa Serikali haina uwezo wa kununua magari yanayohitajika kwa wakati mmoja. Hivyo basi, vituo vya afya pamoja na Hospitali za Wilaya ikiwemo kilichopo Wilaya ya Mpwapwa na Kituo cha Afya cha Kibakwe kilichopo Wilayani Mpwapwa vitapatiwa magari ya kubeba wagonjwa hatua kwa hatua kadri fedha zitakavyopatikana na kuzingatia vigezo vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo jukumu la Halmashauri husika kuhakikisha kuwa inatenga fedha za ununuzi wa magari hayo katika bajeti za Halmashauri zao hatua kwa hatua kila mwaka ili kukidhi mahitaji. Aidha napenda kutoa wito kwa Halmashauri zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kubeba wagonjwa pale inapowezekana, ili fedha kidogo zinazotengwa na Serikali Kuu ziwe ni kichocheo cha kuhakikisha kwamba kila hospitali ya Wilaya na kituo cha afya vinapata magari hayo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba ni tatizo kubwa na magari ya kubeba wagonjwa katika nchi nzima na Mheshimiwa Naibu Waziri anasema magari yatanunuliwa kwa awamu.

Sasa swali je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba kuwa hivi sasa *TRA* wanafanyakazi nzuri ya kukusanya mapato kila mwezi, watenge fedha za kutosha ili wanunue magari na kupeleka Wilaya zote wanunue magari na kupeleka Wilaya zote na kwenye vituo vya afya ambavyo havina magari?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli TRA sasa hivi inakusanya fedha nyingi lakini pia mahitaji kwa Wizara nyingine ni kama vile yalivyo ya huduma za afya, na kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba tutaendelea kutenga fedha kila mwaka ili kununua hizo gari hatua kwa hatua.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niliulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wakuu wa Mkoa Wakuu wa Wilaya Ma-RAS huwa wananunuliwa magari mapya baada ya muda fulani; na kwa kuwa magari wanayokuwa wanatumia huuziwa au hupewa maafisa wengine Wilayani au Mkoani wakati akiwa bado anafanya kazi. Je badala ya kuwapa au kuwauzia maofisa hao Wakuu wa Wilaya na Mkoa Serikali inaonaje magari hayo kuyapeleka kwenye vituo vya afya ili yasaidie kubeba wagonjwa katika sehemu hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, naamini yale magari ambayo yanakuwa yanauziwa maofisa hao yanakuwa ni magari machakavu na huduma zetu za vituo vya afya zinahitaji magari imara. Kwa hiyo haitakuwa busara kuwapelekea magari chakavu.

Na. 299

**Matumizi ya Lugha ya Kiswahili**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa Kiswahili ni lugha iliyowaunganisha watanzania wote na hivyo kuwa utamaduni na utambulisho wa mtanzania:-

Je, ni hatua gani zinachukuliwa kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kimataifa na ya Afrika?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. EMMANUEL J. NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spikam kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba nimjibu Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika hatua zinazochukuliwa na Serikali kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kimataifa nay a Afrika ni nyingi ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

1. Hivi sasa Kiswahili tayari ni moja ya lugha rasmi katika Mikutano ya Umoja wa Afrika na Bunge la Afrika tangu mwezi Julai, 2004.

2. Wizara yangu inaboresha mafunzo ya Kiswahili kama lugha ya kigeni kwa kushirikiana na nchi za Afrika Mashariki na Kati.

3. Serikali ya Tanzania pia imekwishapeleka pendekezo la kukifanya Kiswahili kuwa mojawapo ya lugha rasmi za Jumuiya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*).

4. Lipo Baraza la Kiswahili la Afrika ya Mashariki linaloundwa hivi sasa ambalo rasimu ya Katiba yake inaratibiwa na Tanzania kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)

5. Kuanzia vituo vya utamaduni nchini na nje ya nchi pamoja na ufundishaji wa Kiswahii katika vituo hivyo hatua kwa hatua.

6. Mheshimiwa Spika, juhudi nyingine zinazoendelea hivi sasa ni kuandaa wakalimani na wafasiri wa kutosha wenye ujuzi wa kuaminika na pia kuandaa misamiati ya kutosha, hasa ya kidiplomasia, kwa matumizi ya nchi mbalimbali za Afrika na nje ya Afrika zinazotaka kutumia Kiswahili.

7. Tanzania imeshiriki kikamilisu katika kuunda Chama cha Kiswahili cha Afrika Mashariki (CHAKAMA) ambacho madhumuni yake ni kuwaunganisha walimu wa vyuo vikuu katika kuhamasisha matumizi ya Kiswahili.

8. Mheshimiwa Spika, BAKITA hivi sasa pia linawahamasisha wadau mbalimbali hasa mashirika na kampuni za uchapishaji, taasisi za ukuzaji wa Kiswahili vyuo vikuu na kadhalika, ili wazidi kuandaa programu na vifaa kama vile kanda, *CD-Rom*, *DVD*, kamusi na vitabu mbalimbali vya kufundishia Kiswahili kwa wageni.

9. Kuwahimiza waandaaji wa semina, Mkutano na makongamano nchini kutumia Kiswahili pamoja na lugha za kigeni.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, napongeza sana juhudi za Serikali ambazo zinaonyesha kwamba baadaye Kiswahili kitakuwa lugha ya Kimataifa na ya Waafrika. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza kwa kuwa bado Kiswahili hata hapa nchini kuna baadhi ya makabila bado hawajajua kwa mfano Wamasai na kwa kuwa hata katika Afrika Mashariki, bado kuna nchi ambazo hazikitumii sana Kiswahili kwa mfano Uganda, Burundi au Rwanda.

Je, si vyema kutumia mashirikiano ya Afrika Mashariki Kiswahili kikawa kinazungumzwa Afrika Mashariki kwa ufasaha zaidi baadaye kuenea katika Afrika nzima.

Mheshimiwa Spika, la pili Mheshimiwa Waziri amezungumza katika juhudi zingine ni kupata wakalimani. Je, hawa wakalimani wanapozungumza Kiswahili au kwenda nje kwa kutoa huduma ya ukalimani, Kiswahili fasaha wanatumia lafudhi ipi, lafudhi ya kipwani, ya kiunguja au ya huku bara ya kisukuma au ya kigogo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, la kwanza nchi za Afrika Mashariki kwa pamoja zinashirikiana kukikuza Kiswahili. Kiswahili sasa hivi kinatumika, Tanzania na Uganda na wote wanania thabiti ya kuhakikisha Kiswahili kinakua. Kwa hiyo nawahakikishia kwamba jitihada hizi zitaendelea tutakua pamoja tunataona lugha yetu inavyokuwa kwa haraka kusaidia Afrika na dunia. La pili kuhusu wakalimani wetu watumie lafudhi ipi, tuna bahati lafudhi ambazo tunazo hazijafanya lugha isieleweke, Wasukuma wanaeleweka, Wangoni wanaeleweka na wamasai wakiongea Kiswahili wanaeleweka. Kwa hiyo tatizo la sasa si lafudhi ni kuelewana tu tunapozungumza.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Ahsante sana nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Rais alipokuwa anahutubia Bunge alisema kwamba kuna nafasi 1000 Libya kwa ajili ya kufundisha kiswahili. Je toka Mheshimiwa Rais atoe kauli hiyo ndani ya Bunge, Wizara imechukua hatua gani ya kuwapeleka walimu hao kufundisha Kiswahili Libya kama ni njia moja kueneza Kiswahili katika bara la Afrika?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyotoa. Niseme kwamba swali la pili la Mheshimiwa Selelii tunatumia Kiswahili kipi. Tunatumia kiswahili sanifu, *Standard Swahili.* Lakini hiyo haizuii watu wenye lugha ya kwanza kuathiri lugha sanifu, lakini kwa kweli tunatumia lugha sanifu.

Swali la pili la Mheshimiwa Hamad Rashid ni kwamba ni kweli Rais amesema kwamba Nchi ya Libya inataka walimu 1000. Sasa hivi mazungumzo yanafanyika kati ya Serikali ya Tanzania na Libya na tukifanikiwa tutapeleka walimu nchi ya Libya na si hapo tu pia tuna mahitaji makubwa katika nchi za Burundi, Rwanda, Congo na nchi nyingine. Kwa hiyo natoa wito kwa Watanzania watusaidie ili lugha hii ienee katika nchi za Afrika na dunia nzima na pia iwe ajira kwa Watanzania.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri, lakini nina swali moja dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kuweza kuitangaza vizuri Lugha hii ya Kiswahili kwani hata katika Mkutano wa Umoja wa Afrika kule Ethiopia aliweza kuhutubia kwa Kiswahili. Swali langu ni kama ifatavyo:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuzungumza na waandaaji au waratibu ambao huwa wanaandaa vitu mbalimbali vya kitaifa nchini kwetu waweze kutumia Kiswahili, kwa mfano Miss Tanzania, Miss *World Africa* ama tuzo za mziki Tanzania ambazo huwa zinafanyika hapa nchini kwetu zote zitumike kwa Kiswahili. Tuwe tunafanya kama ambavyo wenzetu wa nchi mbalimbali wanavyoongea lugha zao wanapokuwa wameandaa matamasha au shughuli yoyote nchini kwao.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati umefika sasa hivi Watanzania kujivunia lugha yao ya taifa lugha ya Kiswahili na ningependa kumpongeza mbali ya kuzungumza Kiswahili katika Umoja wa Afrika lakini pia alifanya dhifa moja na Rais wa Comoro na akaongea Kiswahili na watu wengi sana walifurahia.

Mheshimiwa Spika Serikali imetoa Waraka Namba moja, Juni 1974, uliohimiza matumizi ya Kiswahili matumizi ya Kiswahili katika shughuli zote za kiserikali, ikiwa ni pamoja na Bunge, Mhakama na shughuli nyingine. Kwa hiyo, natoa wito kwa Watanzania watumie Kiswahili katika shughuli zote za Kiswahili kwa ajili ya heshima ya lugha yetu.

**SPIKA:** Nadhani huu ni wakati muafaka kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, Waziri Mkuu yuko safarini Dar es Salaam na kama ambavyo imekuwa kawaida Mheshimiwa Waziri wa Habari ndiyo kiongozi wa shughuliza Serikali humu Bungeni

hadi atakaporejea Mheshimiwa Waziri Mkuu. Napenda kwa niaba yenu nimpongeze sana Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, Waziri wa Habari, Utamaduni na michezo kwa sababu majukumu haya mazito ameendelea kuamini wa kukabidhiwa siku hadi siku. (*Makofi*)

Na. 300

**Tatizo kubwa la Maji Mererani**

**MHE. DORAH H. MUSHI** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mererani imepata hadhi ya kuwa mji mdogo lakini kuna tatizo kubwa la muda mrefu la ukosefu wa maji safi na salama na kwa kuwa tatizo hilo limewafanya wananchi kutumia maji ya visima ambavyo sio salama kwa afya zao kwani huwasababishia magonjwa ya mlipuko hasa kwa watoto kuhara damu, kutapika na kuharibika kwa meno; na kwa kuwa kutokana na matatizo hayo wananchi hulazimika kununua maji salama ambayo yanauzwa kwa ndoo moja shilingi 500/=.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwanusuru wananchi wa Mererani kwa kuwapatia maji safi na salama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dorah Mushi, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mji mdogo wa Mererani una idadi ya watu wapatao 50,000. Mahitaji ya maji ni mita za ujazo 1,250 kwa siku. Mji mdogo huu ulikuwa unapata maji ya mtiririko kutoka Wilaya Arumeru. Mradi huu kwa sasa hautoi maji baada ya watu wasiojulikana kuharibu mabomba ya plastiki.

Kwa sasa mji huu unapata maji toka kwenye visima vifupi Kumi na mbili vilivyoko katika vitongoji vya Mererani shule ya msingi, Songambele, Getani, Laizer, Kishili, Mrefu, Saitabau, Tankini, *ADP*, Shule ya Sekondari ya William Mkapa, Elias Siria na Endyamutu. Pia kuna kisima kirefu kwenye kijiji cha Naisingai. Baadhi ya watu wa Mererani waliokaribu na kijiji hiki huhudumiwa pia na kisima hiki. Hata hivyo visima hivi havitoshelezi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa mji wa Mererani umepata hadhi ya kuwa mji mdogo na ni kweli pia kuwa kuna tatizo la ukosefu wa maji na maji salama kwa wananchi wa mji huo. Katika kutatua matatizo ya maji katika mji huo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ina mpango wa muda mfupi na muda mreefu kutatua tatizo hilo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mfupi, kuna mradi wa kisima kirefu unaofadhiliwa na *World Vision Tanzania*. Kisima tayari kimeshachimbwa chenye kina cha mita za ujazo 88 na kinatoa kiasi cha maji mita za ujazo 68 kwa saa, ambayo ni sawa na mita za ujazo 1,632 kwa siku. Tanki la kuhifadhi maji mita za ujazo 135 limejengwa, nyumba ya pampu pamoja na nyumba ya mlinzi zimekamilika. Bomba kuu la maji toka kisimani pamoja na bomba za kusambaza maji tayari zimelazwa. Kazi iliyobaki ni kufunga mtambo kwenye kisima ili mradi uweze kuanza kutoa huduma.

Kwa hivi sasa Shirika la *World Vision* wanaendelea na taratibu za kununua mtambo huo. Mradi huu unatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Novemba 2006. Hata hivyo mradi huu bado hautatosheleza mahitaji.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mrefu, Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro kwa kushirikiana na wananchi wa Kata ya Kikwe, Mbuguni Wilayani Arumeru na Mererani Wilayani Simanjiro, wana mpango wa kuchukua maji kutoka chemchem zilizoko Tengeru.

Wananchi wameanzisha umoja unaoitwa KIMBUME yaani Kikwe, Mbuguni, Mererani kwa lengo la kushughulikia tatizo la maji. Kazi ya usanifu wa mradi imekamilika na gharama za kukamilisha mradi imekadiriwa kuwa ni shilingi bilioni 3.5. Kazi zilizopangwa kufanyika ni kupeleka maji Kikwe, msitu wa Mbogo, Mbuguni na Mererani. Mradi huu utaanza baada ya kupata fedha za kuugharamia ambapo wananchi wako tayari kuchangia nguvu kazi wakati wa ujenzi.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri naomba kumwuliza swali moja la nyongeza. Je kwa kuwa ameshahakikisha kwamba wananchi wa Mererani pamoja na Wilaya ya Arumeru wamekwisha kukubaliana kwamba watachangisha fedha kwa ajili ya kutandaza yale mabomba. Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia ili wananchi waweze kupata maji safi na salama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwmba aweze kushirikiana na Halmashauri ya Wilya ya Simanjiro ili waweze kuingiza mradi huu na kuupa kipaumbele katika miradi ya maji safi na usafi wa mazingira kwa sababu mradi huu una sifa ambazo unaweza ukafadhiliwa katika programu hiyo na pesa za programu hiyo zipo za kuweza kufadhili huo mradi.

Na. 301

**Miradi ya Visima vya Maji**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya sabini Serikali ilikuwa na mpango mzuri wa kusambaza maji vijijini kwa kuchimba visima, kuweka pampu na kujenga matenki ya kuhifadhia maji na kwa kuwa mpango huo ulikufa baada ya pampu nyingi kuibiwa na watumishi wasiokuwa waaminifu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua visima vilivyokufa kutokana na wizi huo katika kata ya Rungwa hali iliyosababisha wananchi kuchangia maji na wanyama pori katika malambo?

(b) Je, Serikali iliwachukulia hatua gani wafanyakazi hao walioiba pampu hizo kwa kisingizio cha kwenda kuzitengeneza na badala yake kuhamishia kwenye miradi yao binafsi?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuchimba malambo ya uhakika katika maeneo hayo kwa matumizi ya binadamu kama mpango mbadala wa kudumu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa John Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye vipengele (a),(b) na (c) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa katika miaka ya sabini Serikali ilikuwa na mpango mzuri wa kusambaza maji vijijini kwa kuchimba visima, kuweka pampu na kujenga matenki ya kuhifadhia maji. Huduma kutoka kwenye baadhi ya miradi hiyo haikuendelea kwa sababu ya uchakavu ua wizi wa pampu za maji kutokana na wananchi kutoilinda na kuitunza miradi hiyo. Mfano mzuri ni ile ya kata ya Rungwa ambayo ilikuwa na visima vitatu vilivyochimbwa kati ya mwaka 1973 na 1975 lakini havifanyi kazi hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kisima kimoja namba *SG.75/73A* kipo kijijini Rungwa pampu ya kisima hiki ilibiwa tarehe 19 Mei 1983. Mradi huu haukuweza kutumika tena kwani baada ya wizi wa mtambo wanakijiji wakorofi walitumbukiza mawe ndani ya kisima. Visima vingine viwili vilichimbwa kwenye kijiji cha Mwamagembe. Kisima namba *SG.101/73* kilifungwa matombo wa maji unaoendeshwa na injini ya *lister* na kisima namba *SG.2/73* kilifungwa *windmill*. Mtambo katika kisima namba 101/73 uliibiwa mwaka 1984 na *windmill* ya kisima cha pili iliondolewa mwaka 1985 kwa ushauri wa mfadhili, baada ya kuharibika na vipuri vya kuukarabati kukosekana.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika harakati za kuwapatia maji wananchi wa kata ya Rungwa kati ya mwaka 2004 na 2005 Serikali ilichimba visima vingine vitatu katika kijiji cha Mwamagembe. Kati ya visima hivyo ni kisima kimoja tu ndicho yalipatikana

maji kiasi cha mita za ujazo 8 kwa saa. Kazi inayoendelea hivi sasa ni ujenzi wa mradi wa kusambaza maji katika kiji cha Mwanagembe. Jumla ya shilingi 94,649,650/= zinategemewa kutumika kwa kazi hii. Kijiji cha Rungwa kitapata huduma ya maji kupitia programu ya kitaifa ya maji na usafi wa mazingira vijijini inayoanza mwaka 2006/2007.

(b) Mheshimiwa Spika, taarifa za wizi wa mitambo yote mawili ziliwasilishwa kwenye vyombo vya usalama. Wizara yangu haina taarifa zinazoonyesha kuwa watumishi wa Serikali walihusika na wizi wa pampu hizo. Hivyo basi hakuna hatua zilizochukuliwa dhidi ya mtumishi yeyote kwa kuwa hakuna mtumishi aliyetuhumiwa kwa wizi huo. Endapo Mheshimiwa Mbunge anafahamu watuhumiwa, naomba awasilishe taarifa polisi ili hatua za kisheria zichukue mkondo wake.

(c) Mheshimiwa Spika, hatua ambazo zinachukuliwa na Serikali kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la sehemu (a) zitatosheleza mahitaji ya maji ya binadamu katika maeneo hayo. Kuhusu uchimbaji wa malambo, Serikali kwa kushirikiana na wananchi na Halmashauri ya Wilaya itaendelea kuchimba malambo kwa kuzingatia mahitaji kama yanavyoibuliwa na wananchi kupitia Halmashauri zao za Wilaya.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza swali moja la nyongeza. Kama majibu yanavyoonyesha, kumekuwa na wizi wa wazi wazi na kweli wananchi wametaabika sana kutokana na wizi huo. Sasa, katika miradi hii inayochimbwa sasa hivi ili kuwapatia wananchi maji, Serikali itahakikishaje kwamba vitendo kama hivyo, havitokei tena ili wananchi waweze kuendelea kupata maji ya uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wali kwamba miradi hii ilikuwa haina uangalizi. Lakini napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote na kuwaomba kwamba tusaidiane kwa kupitia kwenye Halmashari zetu kuwahamasisha wananchi na zaidi wale wanakijiji ambao watakuwa mradi huo ni wa kwao, wenyewe waweze kuwa ni walinzi wa mradi, waweze kushirikiana na kuweza kila wakati kufichua maovu na watu ambao hawaitakii mema miradi ya maji.

Na. 302

**Tatizo la Mioto Nchini**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa moto umekuwa ni adui mkubwa wa uoto wa asili na mazingira kwa ujumla hapa nchini; na kwa kuwa tatizo hilo linaongezeka sana wakati wa kipindi cha ukame:-

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya dharura ya kudhibiti mioto nchini?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kusimamia na kufuatilia ufanisi *(performance)* wa programu ya upandaji miti nchini katika mazingiara yaliyoathirika na moto?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 sehemu ya ix inazungumzia masuala ya mioto. Iwapo mhusika atataka kuchoma moto katika eneo nje ya mazingira anamoishi, atatakiwa kupata kibali cha kufanya hivyo. Baada ya kupata kibali, mhusika atatakiwa atoe taarifa kwa watu walio ndani ya nusu kilometa kutoka mahali ambapo anataka kuwasha moto. Aidha, aliyewasha moto anawajibika kuudhibiti moto huo.Vile vile yeyote atakayeona moto ambao utaleta madhara au unaleta madhara, anawajibika kusaida kuuzima.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaandaa Tamko Rasmi la Serikali kuhusu udhibiti wa matukio ya mioto. Katika Tamko hilo, Serikali itabaini vyanzo mbali mbali vya moto. Tamko hilo pia litaelekeza mbinu za kudhibiti moto. Aidha, baada ya tamko, elimu itatolewa kwa kuanzia kwenye maeneo yenye matatizo makubwa ya moto kuhusu matumizi ya sheria katika kudhibiti uchomaji moto misitu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na *NGOs*, vijiji na sekta binafsi, ina programu za kuhifadhi misitu na kupanda miti maeneo mbali mbali nchini kwa ajili ya kuhifadhi uoto, vyanzo vya maji na ardhi hasa maeneo yaliyoathirika kwa moto. Baadhi ya maeneo ambayo programu hii ya hifadhi ya misitu ya asili na upandaji wa miti inatekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- Ruvu – Hekari 3400, zimepandwa miti kwa njia ya kilimo cha mseto kwa kushirikisha kaya 1900 za Vijiji vinavyozunguka misitu ya Ruvu kwa ajili ya uoto ulioathirika. Hekari 4600 zimeachwa kwa ajili ya uoto wa asili.

- Usimamizi Shirikishi wa Misitu yaani *Participatory Forest Management (PFM).* Uhifadhi wa misitu na upandaji miti unafanyika chini ya programu hii katika Wilaya 53 nchi nzima ikiwashirikisha wanavijiji, watu binafsi, *NGOs* na Taasisi mbali mbali yakiwemo maeneo yaliyoathirika na moto. Shughuli za usimamizi shirikishi zilianza kwenye viwanja 14 katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Morogoro na Lindi. Wilaya 15 katika mikoa ya Morogoro, Tanga, Pwani, Mtwara, Ruvuma na Lindi. Wilaya 25 katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Singida, Dodoma, Pwani, Ruvuma, Mtwara, Rukwa, Tabora, Kigoma, Kagera, Shinyanga na Mwanza. *(Makofi)*
- Wizara yangu pia, inahimiza wananchi kuendeleza misitu kwa kutumia elimu yao ya jadi. Kwa mfano mkoani Shinyanga uendelezaji wa misitu kwa kutumia uoto wa asili umeleta mafanikio katika kuokoa maeneo ambayo hayakuwa na misitu kabisa

kutokana na moto na mifugo. Wizara yangu inaendelea kueneza njia iitwayo *Ngitili* katika kanda ya Ziwa kupitia kituo cha *NAFRAC*.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo ya Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa vile Tanzania tunajulikana kwa kuhifadhi Banoanuai na Banoanuai nyingi na nzuri kwa kweli iko katika hifadhi za taifa *(Protected Areas)*. Kwa vile katika *Protected Areas* zetu Tanzania na hasa mbuga kubwa kama za Serengeti, tumekuwa tunatumia moto kama chombo cha kutusaidia kuhifadhi Banoanuai, tunatumia *Cool Burning* au *Controlled Burning*. Miaka ya karibuni utafiti umeonyesha kwamba *Controlled Burning* na *Cool Burning* inaua sana Banoanuai hasa viumbe wadogo wadogo, masalio ya ndege na wanyama wadogo wadogo. Kwa hiyo tunapozungumzia Banoanuai, ina haribiwa sana. Je, Wizara au Serikali ina mpango gani kufuatilia suala la matumizi ya moto katika hifadhi zetu kuhakikisha kwamba moto unaotumiwa unakuwa endelevu?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba nimjibu Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:- Kwanza, napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, moto huwa unatumiwa ili kuzuia moto unapotokea wakati wa ukame sana, kuumiza sana Bayoanuai na uoto wa asili. *Controlled Burning* anayoiongelea Mheshimiwa Mbunge, inatumiwa zaidi katika maeneo ambayo yamehifadhiwa ili kuweza kuwatetea na kuwa-*protect* viumbe wanaoishi katika maeneo hayo wakati moto ukiwashwa wakati wa ukame sana.

Mheshimiwa Spika, utafiti umeonyesha kwamba *early burning* inawaruhusu viumbe ambao wako katika hifadhi hizo kuweza ku-*regenerate* na kujirudia katika hali yake ya kawaida kwa muda mfupi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, manashuhudia utajiri wa fani uliomo humu. Swali la Profesa linajibiwa na Serikali, upande mwingine ni Profesa pia. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mioto hii ya misitu mikubwa, ikitokea huwa ni mioto mikubwa sana na athari yake pia ni kubwa sana. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuwa na helkopta za kuzimia moto pindi inapotokea kama nchi nyingine za nje zinavyofanya?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, katika nchi zilizoendelea za Magharibi ni kweli kwamba helkopta na ndege ndogo zinatumika katika kuzima mioto. Lakini shughuli hizo kwa kweli ni ghali sana na vyombo hivyo ni vya ghali sana na hapa kwetu tutaweza kuvitumia kama tunavyozidi kupata uwezo. Wito tunaotoa kwa wananchi kwa ujumla ni kwamba wachunge sana na

kuhakikisha kwamba mioto inazimwa wakati ikiwa ndio imeanza, isiachwe ikawa mikubwa sana. Pili, katika maeneo ambayo mioto imeishakuwa mikubwa, wananchi wajaribu kuchoma mioto mingine ielekee kule moto mkubwa unapokua ili kuweza kuzima moto huo.

Na. 303

**Gharama za Kumsomesha Daktari**

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa kumsomesha mwanafunzi hadi kupata shahada na hasa daktari ni gharama kubwa sana; na kwa kuwa wasomi wengi waliofikia kiwango hicho huwa wanakwenda nje ya nchi kutafuta maslahi zaidi:-

(a) Je, Serikali bado haijaona umuhimu wa kutunga sheria itakayowalipisha ada fulani watu wa namna hiyo ili ipate mapato kutokana na elimu waliyoipata?

(b) Kama hiyo inawezekana. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwaelimisha wananchi wanaotaka kwenda nje ya nchi kuwa wajulishe wanakokwenda badala ya kutoroka ili kipato chao kijulikane kwa lengo la kulipa kiasi fulani kwa Serikali kutokana na kipato hicho?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kunibu swali la Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mbunge wa Chakechake, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:- Nitaanza na maelezo ya utangulizi.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kumsomesha mwanafunzi hadi kupata shahada hasa ya udaktari ni gharama kubwa. Inakisiwa kwamba kumsomesha daktari inaigharimu Serikali shilingi milioni 40.

Nakubaliana naye pia kwamba wasomi wengi waliofika kiwango hicho huwa wanakwenda nchi za nje kwenda kutafuta maslahi zaidi. Utafiti uliofanywa na Mtaalam wetu kwa kushirikiana na Shirimka la Afya Duniani mwaka 2003, ulionyesha kwamba kwa kipindi kile, wataalam wa afya waliokuwa nje ya nchi walikuwa 213 na kati yao madaktari walikuwa 130.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi. *(Makofi)*

(a) Kwa miaka mingi baada ya uhuru Serikali ilikuwa inalipia gharama zote za kusomesha wanafunzi hadi ngazi ya Chuo Kikuu. Wanafunzi walikuwa wanasaini mkataba wa kuitumikia Serikali kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu kuanzia pale wanapohitimu. Hii iliwezekana wakati ule kwa kuwa Serikali ilikuwa ndiye Mwajiri Mkuu wa wahitimu ambapo wahitimu walikuwa na uhakika wa kuajiriwa na Serikali.Kutokana na mabadiliko ya sera za uchumi na uajiri ambapo sekta binafsi inapewa nafasi kubwa, mikataba kama hiyo haitekelezeki.

Kwa hiyo, Serikali imebuni na imeanza kutekeleza utaratibu maalum wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wanaohitaji na wanaostahili. Utaratibu huu upo kwa mujibu wa sheria na katika sheria hiyo kuna vipengele vinavyombana mkopaji endapo atakiuka masharti ya kurejesha mkopo.

(b) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba wahitimu wangeonyesha moyo wa uzalendo na shukrani kwa Serikali wanapoondoka kwenda nchi za nje kutafuta maslahi zaidi badala ya kutoroka, wangetegemewa kuaga. Katika swali lake Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, amependekezaa kwamba wangeaga ili kipato chao kijulikane kwa lengo la kulipa kiasi Fulani kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na mtindo wanaotumia wa kutoroka, sitegemei kwamba watakuwa tayari kuieleza Serikali ya Tanzania mapato yao katika nchi wanazokweenda. Hata wakitungiwa Sheria hapa nchini, sheria hiyo haitakuwa na nguvu katika nchi inayowapokea.

Mheshimiwa Spika, kwa kadri ya uwezo kifedha unavyoongezeka katika Serikali, tunajaribu kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa Sekta ya Afya ili wahitmu washawishike kubaki na kufanya kazi hapa hapa nchini na wale walio ng’ambo warudi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba niulize Swali moja dogo la nyongeza. Je, inapotokea kwamba hawa wataalam pengine wa afya , imetokea pengine amesomeshwa hivyo kwa gharama kubwa, lakini pengine kwa majaaliwa ya Mwenyezi Mungu amefariki au hajapata kazi ya kumfanya aweze kurejesha pengine huo mkopo ambao umetumika kumsomesha, Serikali ita-*recover* namna gain hizo gharama zilizotumika kuwasomesha?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, tunpotunga sheria unaangalia maeneo yote haya na kwamba ikitokea hivi, tutafanya hivi. Ningemshauri Mheshimiwa Zambi aisome ile sheria kwa sababu inaanzia mbali, wadhamini mpaka kufikia kupata mkopo, mambo mengi yameangaliwa kwamba hawa watu wasituponyoke.

**MHE. ANNA K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni kweli kazi zote duniani ni kazi, lakini kaazi ya madaktari, manesi ni kazi ambayo ni kazi ya wito na pili ni kazi ambayo kwanza, wao

wanakuwa wameshika maisha ya binadamu wanaowahudumia mikononi. Wana uwezo wa kumfanya binadamu akapona na pia wanaweza wakamfanya binadamu akafa.

Mheshimiwa Spika, naomba tukubaliane kwamba kazi hii ya madaktari ni ngumu na wanaifanya kwa wakati mgumu sana. Mara kwa mara tukiwa tumelala, wenzetu wako kazini. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuwawekea mazungira bora kiasi ili wasipate ushawishi wa kutoroka na kwnda nje ya nchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya! Ingawa sina hakika kwamba madaktari wana uwezo wa kumweka mtu hai ama … *(Kicheko)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni vigumu, mimi nikiwa Daktari kuwatetea madaktari. Lakini wakati anajibu swali la msingi, nilisema kwa jinsio Serikali itakavyokuwa inapata uwezo, maslahi ya madaktari pamoja na watenda kazi wengine wa afya, yataongezwa, na kuanzia mwezi Januari mwaka huu walitupiwa jicho la huruma akaongezwa kidogo na sasa hivi tuna matatizo kwa wafanyakazi kutoka hospitali za Misheni wanakuja hospitali za Serikali. Kwa hiyo hilo limezaa tatizo. Lakini nashukuru kwa kuwaonea huruma na nadhani hizi salaam zimeishafika ka wanaohusika.

Na. 304

**Matumizi ya Mti wa Mparachichi**

**MHE. MWAKA ABDULRAHMAN RAMADHAN** aliuliza:-

Kwa kuwa watu wengi wenye upungufu wa damu hutumia mti wa Mparachichi kwa kuchemsha majani au magome yake na kunywa maji yake ambayo huaminika kuwa yanaongeza damu kwa haraka sana:-

(a) Je, ni kweli matumizi ya mti huo yanaiongeza damu?

(b) Kama majibu ni ndiyo. Je, kuna madhara yoyote yanayoweza kumpata mtumiaji wa mti huo?

(c) Je, matumizi ya mti huo yanasababisha ugonjwa wa kana kama inavyoaminika kwa baadhi ya watu?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhan, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mti wa Mparachichi huota maeneo mengi Duniani ikiwemo nchi yetu Tanzania. Lakini hakuna utafiti wa kisayansi uliothibitisha katika nchi

yoyote kuwa majani au magome ya mti wa mparachichi yanaongeza damu. Mara nyingi matunda ya mparachichi hutumiwa kama chakula na mafuta ya kulainisha ngozi na nywele, lakini matumizi ya majani na magome ya mti huo kama dawa yanaendana na imani na desturi katika jamii fulani fulani. Imani hiyo haiambatani na ushahidi wa kisayansi.

(b)Ulimwengu wa sayansi haujapata ripoti inayodhihirisha kwamba madhara yoyote yanaweza kujitokeza kutokana na matumizi ya majani au magome ya mti wa mparachichi.

(c)Aidha, hakuna taarifa ya kisayansi inayohusisha majani, matunda au magome ya mti wa mparachichi kusababisha saratani. Matunda ya mti wa mparachichi kama ilivyo kwa miti mingi, yana kiwango kikubwa cha *Vitamin A, B, C, D, G, K* pamoja na *mono-unsaturated fatty acids* na *tocopherols*. Tofauti na imani kwamba mparachichi unaweza kusababisha saratani, kisayansi tunajua kuwa matumizi ya *vitamin* hizi nilizozitaja zina uwezo wa kuzuia saratani ya matiti na tezi kwa wanaume *(prostate cancer).*

**MHE. MWAKA ABDULRAHMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda pia kumwuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa ameeleza kwamba hakuna utafiti wowote uliofanyika juu ya magome ya mparachichi. Je, Waziri yuko tayari kupitia Wizara yake ya Afya kufanya utafiti wa magome ya mparachichi ambayo ndio yanasadikika kuwa yanatia *cancer* na hasa ukizingatia kwamba hivi sasa akina mama wengi ndio wnapata matatizo ya *cancer*?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, wakati najibu swali la msingi, nimeleeza kwamba utafiti umefanywa katika nchi nyingi, nakiri kwamba hapa Tanzania hatujafanya. Lakini katika tafiti zilizofanywa, hazijaonyesha kwamba ipo haja kwa sisi kufanya hiyo kazi kwa sababu huko walikofanya, hayo magome na majani hayatumiki kwa kazi nyingine yoyote. Lakini kwa ushauri wake ina zungumzika, tutaliangalia.

**SPIKA:** Wakati tunaendelea na kipindi cha maswali, ninapenda tu kueleza kwamba Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii nimesoma naye shule ya Sekondari Tabora miaka ya nyuma. Nilikuwa simwezi kabisa kwa amasomo ya Kemia, Fizikia na Baiolojia. Lakini na yeye alikuwa haniwezi kabisa kunisogelea kwenye masomo ya Lugha, Kiingereza na Historia. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 305

**Kipande cha Barabara Kinachopita Katikati ya Mji wa Magu**

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Kwa kuwa magari makubwa bado yanapita kwa wingi katikati ya mji wa Magu kubeba abiria na mizigo na hivyo kusababisha kero ya magonjwa yatokanayo na vumbi na pia kuisababishia Halmashauri ya Wilaya ya Magu hasara ya kuikarabati mara kwa mara:-

(a) Kwa nini kipande hicho cha barabara hakikuwekewa lami wakati barabara ya Mwanza - Musoma ikijengwa upya kama ilivyofanyika kwa mji wa Nzega na miji mingine?

(b) Je, ni lini Serikali itakiwekea lami kipande hicho cha barabara ili kuondoa adha inayotokana na vumbi linaloathiri afya za watu na pia kuiondolea Halmashari ya Magu mzigo wa kuikarabati barabara hiyo mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILITON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mbunge wa magu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipande cha barabara kinachopita katikati ya mji wa Magu kiko chini ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kinahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Magu. Kutokana na kutokuwepo kwa fedha za kutosha wakati wa kujenga upya barabara ya Mwanza – Musoma, kipande hicho hakikujengwa.

Kwa kuwa barabara hiyo ni ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu, ninamshauri Mhshimiwa Mbunge awasilishe suala hili TAMISEMI ili kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Magu, barabara hiyo iwekwe kwenye mipango yao ya maendeleo ya kuwekewa lami na hatimaye kuondoa kero kwa wakazi wa nmji wa Magu. Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Mwanza ipo tayari kutoa ushauri wa kitaalam kama utahitajika.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na pia kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Magu wanaathirika sana na barabara hii kwa sababu wananchi wengi wanajipatia mahitaji yao na kujipatia riziki katika mtaa huo. Kwa kuwa kipande hiki kina kilomita 1.6 tu; na kwa kuwa gharama za kujenga

zimetathminiwa kuwa milioni 616 peke yake; Na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Magu haina uwezo wa kujenga barabara hiyo, suala hili lilipelekwa kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa na Bodi ikaridhia kwamba suala hili liende kitaifa na usla hili likapelekwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Naibu Waziri amesema wakati barabara ya Mwnza – Musoma inajengwa, fedha hazikuwepo, Je, sasa hivi pesa hazijapatikana nza kuweza kujenga kipande hiki?

Mheshimiwa Naibu Waziri ataweza kuliahidi Bunge lako na wananchi wa Magu kwamba Serikali itaiweka barabara hiyo katika bajeti ya mwaka ujao ili wananchi wa Magu waondokane na kero hii moja kwa moja?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo naifahamu kwa sababu huwa na mimi naipita mara moja moja ninapopiata pale Magu. Najua ina usumbufu.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, barabar hiyo kwa kweli ni ya TAMISEMI na ameuliza kwamba je, fedha sasa zipo? Mimi nasema kwamba fedha bado hazipo za kuweza kujenga barabara hiyo kwa maana ya kutengewa kwa barabara hiyo.

Lakini kama nilivyomweleza, kama umuhimu upo kama alivyoeleza na nadhani upo na ndio maana wamefikisha hata kwenye Bodi ya Barabara, nashauri Halmashauri iweke kwenye Bajeti ya mwaka kesho ili iweze kutengewa fedha.

Na. 306

**Ujenzi wa Soko la Kimataifa**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2005/2006 ilionyesha kuwa Wizara husika imeamua kujenga masoko ya kimataifa katika maeneo ya Segera (Tanga) na Makambako (Njombe):-

Je, ni lini ujenzi wa masoko hayo muhimu utaanza kwenye maeneo yaliyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini kama ifuatavyo: -

Ni kweli kwamba, katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2005/2006 Wizara iliyokuwa na dhamana ya uendelezaji wa masoko ya mazao ilitoa ahadi ya kuendeleza masoko ya mazao katika sehemu mbalimbali nchini. Nukuu ya ahadi hiyo ni kama

ifuatavyo: “Kuratibu na kufanya tathmini ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya masoko katika sehemu maalum. Tathmini itaanza na ujenzi wa soko la mboga na matunda katika mji mdogo wa Segera na soko la nafaka na bidhaa mchanganyiko katika mji mdogo wa Makambako.”

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu ulilenga kuendeleza juhudi za uzalishaji wa mazao na upatikanaji wa soko la uhakika kwa wananchi walioko katika maeneo hayo ambao huzalisha mazao hayo kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu ya masoko huhitaji fedha nyingi ikilinganishwa na uharaka wa upatikanaji wa faida. Kwa kiasi kikubwa hali hii haiwavutii wawekezaji binafsi. Pale ambapo sekta hii haiwezi kuwekeza katika miundombinu ya aina hii pengine kwa sababu ya ukosefu wa faida ya haraka ama ukubwa wa gharama za ujenzi, Serikali imekuwa ikichukua jukumu hilo. Hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Jackson Makwetta kwamba, Serikali itaendelea kutenga fedha mwaka hadi mwaka ili kukamilisha ujenzi wa soko hili hatua kwa hatua hadi likamilike. Soko linalotazamiwa kujengwa Makambako ni soko ambalo litaweza kutoa huduma mbalimbali yaani *one stop centre*.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza.

Kutokana na Mji wa Makambako ulipo, wafanyabiashara wa mazao kutoka Malawi, *Congo*, Zambia, Zanzibar, Dar es Salaam na Kenya kufika pale kununua mazao. Lakini hukuta mazao yako kwenye mavumbi tu kwa sababu hakuna soko. Je, kutokana na hali hiyo na ili kuvutia lengo la kujenga soko la kimataifa, si ingekuwa vizuri kwa Wizara hii kutembea kwa miguu miwili kutumia *program* ile ya masoko madogo madogo ili kujenga soko la wastani pale wakati wakiendelea kujenga soko hili la kimataifa na kwa ratiba ambayo tutaijua kusudi watu wajue nia nzuri hii ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, masoko ambayo yanajengwa kwa sasa hivi yale madogo madogo ni ya *AMSDP*. Tayari katika Mkoa wa Iringa yale masoko mawili ya Mufindi na Ludewa tayari yanaanza kujengwa kwa sababu tenda ilifunguliwa tarehe 27 Juni, 2006. Soko hilo ambalo analizungumzia yeye la Makambako na Segera ni masoko yale ambayo yanaitwa *mall*, kwa mfano yale ya Afrika Kusini, Uingereza na Marekani, yale ambayo yana vitu vingi kuna benki humo ndani, kuna sehemu ya usindikaji, kuna sehemu ya ufungashaji na sehemu za kutoa habari za masoko. Sasa mwaka jana zilitengwa Shilingi milioni 21.5 kwa ajili ya upembuzi ama uchunguzi wa awali. Lakini pesa hizo hazikuweza kutumika zote, zilitumika Shilingi milioni 4.9 kwa sababu ya njaa na ukame ambao uliipata nchi yetu. Mwaka huu kwa ajili ya soko hilo zimetengwa Shilingi milioni 120. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Makwetta, asiwe na wasiwasi kabisa, kazi hiyo itafanyika. Hivi karibuni tu mkiishapitisha Bajeti yetu hizo pesa zitaanza kwa ajili ya kumtafuta yule *consultant* ambaye atafanya kazi ya kufanya upembuzi yakinifu, yaani kwa maana ya kuangalia *supply* na *demand assessment* ya eneo hilo, kuangalia eneo kama linatosha kwa *future expansion*, kuangalia eneo hilo kwa vigezo vya kwamba

Halmashauri kwa kuwa ndiyo itakayokuwa inasimamia basi tuangalie kwamba wao wana mawazo gani na watatoa mchango gani, lakini wafanyabiashara pia ni lazima wahusishwe pamoja na huduma zingine kwa mfano umeme na maji ni lazima tuwahusishe katika ujenzi na utekelezaji wa soko hili. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umeishapita. Ninayo matangazo hapa. Nikianza na wageni.

Waheshimiwa Wabunge, imekuwa ni vizuri kutangaza wageni kwa sababu vinginevyo itakuwa ni ubaguzi kwa sababu ni utaratibu tumeutumia, sasa tukiusitisha ghafla hatutatenda haki.

Kwa heshima na taadhima naomba nimtambulishe mgeni wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Dr. Asha-Rose Migiro. Mgeni huyu mashuhuri yuko kwenye *Speaker's Gallery*, ni Mzee Hamis Kitende Kisaburi, kutoka Murutunguru Ukerewe, yeye ni Baba Mkwe wa Waziri. Karibu sana mzee, karibu sana. *(Makofi)*

Pamoja naye, tuna Mheshimiwa Rosemary Nyerere, kutoka Butiama ambaye amefuatana na mzee pia. Wote hawa ni wageni wa Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, Waziri wetu wa Mambo ya Nje. Wale mliokuwa katika Bunge hili siku za nyuma mtakumbuka kwamba Mheshimiwa Rosemary Nyerere alikuwa Mbunge mwenzetu. *(Makofi)*

Mgeni wa tatu wa Mheshimiwa Waziri ni Bwana Mbelwa Kairuki, yeye anatokea Dar es Salaam, ni rafiki wa karibu wa familia ya Dr. Asha-Rose Migiro. Upande wa kushoto wapo walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Mazengo ya Mjini Dodoma, naomba msimame. Karibuni na tunaendelea kuwashukuru walimu ambao wanachukua fursa hii kuwaleta vijana kuangalia Bunge lao la Tanzania linavyofanya kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Balozi Seif Ali Iddi ameniomba niwatambulishe wageni wake kadhaa ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Jimbo lake la Uchaguzi la Kitope, Zanzibar. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani na poleni kwa safari ndefu kutoka Zanzibar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, *Chief Whip* wa Kambi ya Upinzani, ameniomba nitangaze kuwa ana mgeni wake Mheshimiwa Shaibu Suleiman Hamad, ambaye yeye ni Mwenyekiti wa Chama cha *CUF* wa Wilaya ya Wete Pemba, yule pale. Karibu sana Mheshimiwa, wewe umetoka mbali zaidi tena, Pemba. Ninafurahi kuwatambulisha pia viongozi wa Shirikisho la Vyama vya Wachimba Madini Tanzania *(FEMATA),* ambao ni Bwana Gervas Makwinya, Modestus Maembe, lakini cha kufurahisha zaidi ni kwamba kiongozi wao ni mwanamke Ndugu Hellen Mwambegele, wale pale. Hakika nchi yetu akinamama wanapiga hatua. Mama huyu anaongoza ujumbe huo wa watu watatu, mwanamke ni yeye peke yake, lakini anawaongoza vizuri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Capt. John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, ameomba niwatambulishe wageni wake ambao ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, *Lieutenant Col.* Mstaafu Jacob Kulemba, yule pale. Naona Mwenyekiti wa Halmashauri naye ana shepu shepu kama zile zile za Mbunge. Pia kuna Mheshimiwa Diwani wa Mbinga, Ananus Ngai na wengine ni Joel Mbewa na Gairo Mwafulwa. Karibuni sana Waheshimiwa na poleni sana na matatizo ya usafiri ya huko Mbinga. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu mikutano/vikao, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa William Kusila, anawatangazia wajumbe kwamba, kutakuwa na mkutano mfupi saa tano asubuhi leo katika chumba namba 133.

Mheshimiwa Mgana Msindai, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa anawatangazia wajumbe wote kutakuwa na Kikao leo saa tano asubuhi chumba Namba 227.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, anawatangazia wajumbe wa Kamati hiyo ya Maendeleo ya Jamii kuwa kutakuwa na kikao leo saa tano na nusu asubuhi Chumba Namba 231.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwafahamisha kwamba kesho saa 3:00 asubuhi katika ukumbi wa zamani wa Bunge kutakuwa na semina ya kuzindua Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo itakayotolewa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Hii ni semina muhimu sana katika kuweka uelewa wetu sisi Waheshimiwa Wabunge kuhusu programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo. Naomba nyote ambao mtakuwepo hapa Dodoma tuweze kuhudhuria ili tuweze kupanua ujuzi wetu kuhusu sekta hii muhimu.

Jumapili, tarehe 30 yaani kesho kutwa katika ukumbi huo kutakuwa na semina nyingine. Kitabu kipya kinachoitwa: *"The Promise"* ambacho kinatolewa na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Nimepata bahati ya kupata nakala ya kitabu hiki. Kwa kweli napenda kusema kwamba, Waheshimiwa Wabunge ambao hawatahudhuria watakuwa wamekosa jambo moja zuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa uvumilivu wenu.

Katibu, hatua inayofuata, endelea na *Order Paper.*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007**
**Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa**

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyotolewa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kuungana na Mawaziri wenzangu kuwapongeza kwa dhati kabisa Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuongoza Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kumpongeza Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuongoza Awamu ya Sita ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ushindi wao mkubwa unadhihirisha imani waliyonayo wananchi kwa viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi bila kujali itikadi zao za kisiasa. Kwa hakika udhindi wao ni wa kihistoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa kwa kura nyingi na Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge hili Tukufu kuwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina budi vile vile kutoa pongezi nyingi kwako wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuliongoza Bunge hili Tukufu. Aidha, naomba kumpongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, mwanamke wa kwanza katika historia ya nchi yetu kushika wadhifa huu. Busara na usahihi wa kuchaguliwa kwenu unadhihirishwa kwa umakini na uhodari mkubwa. *(Makofi)*

Natoa pongezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushindi walioupata kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, ushindi uliowawezesha kuwemo ndani ya Bunge leo hii. Uchaguzi huu umeidhihirishia dunia ukomavu na upevu wa kisiasa wa Watanzania katika kujenga nchi yenye amani, utulivu na demokrasia. Hakuna shaka hata kidogo kwamba Tanzania ni kisiwa cha amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepatwa na matatizo mbalimbali ya kijamii kama vile kufiwa au kuuguliwa. Tunaomba Mwenyezi Mungu awape faraja na azilaze roho za marehemu mahali pema, Amin.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwashukuru watoa hoja walionitangulia, hususan Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa , Waziri wa Fedha,

Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa , ambao hotuba zao zimetoa dira ya Taifa letu katika mwaka huu wa fedha. Hotuba hizo zimegusia mambo ya kimsingi yanayohusu Wizara yangu na zimefanya kazi yangu kuwa nyepesi. Hivyo, sina budi kuwashukuru.

Naomba pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri wengine wote walionitangulia kwa kuzungumzia kwa ufasaha maeneo ya ushirikiano wa kimataifa wanayoyashughulikia katika Wizara zao. Wizara yangu imekuwa ikishirikiana vyema na kwa karibu sana na Wizara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee na kwa unyenyekevu mkubwa ningependa kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani yake kwangu na kwa kuniteua kuwa mwanamke wa kwanza katika historia ya Tanzania kuongoza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Fursa hii imeniongezea ari ya kuitumikia nchi yetu kwa unyenyekevu na uaminifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niitumie fursa hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, kwa maoni na ushauri kwa Wizara yangu ambao umeiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio. Tutaendelea kuchota busara za Kamati hii katika kutekeleza kazi za Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wenzangu ninaoshirikiana nao pale Wizarani kwa kuandaa na kukamilisha hatua zote za Bajeti na hotuba hii kwa dhati. Naomba niwashukuru Naibu Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Seif Ali Iddi na Mheshimiwa Dr. Cyril August Chami, Katibu Mkuu, Balozi Charles Kashasha Mutalemwa, Naibu Katibu Mkuu, Balozi Patrick Cyprian Mombo, Wakurugenzi, Mabalozi wetu walioko nchi za nje pamoja na wafanyakazi wenzangu wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 pamoja na mambo mengine, Wizara yangu ilipanga kutekeleza malengo muhimu yafuatayo: -

(i) Kuratibu na kutekeleza mpango kabambe wa Sera ya Mambo ya Nje na majukumu mengine ya Wizara, ikiwa ni pamoja na kutangaza maeneo ya uwekezaji vitega uchumi, kutafuta masoko ya bidhaa zetu nje, kuvutia watalii, kutafuta misaada na unafuu au misamaha ya madeni;

(ii) Kushiriki katika utatuzi wa migogoro ya kimataifa;

(iii) Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa;

(iv) Kuratibu ziara za nje za Viongozi wa Kitaifa na zile za Viongozi Wakuu wa Nchi na Serikali wa Mataifa mengne wanaotembelea Tanzania;

(v) Kuimarisha uongozi, utawala na usimamizi wa fedha katika Wizara kwa kuajiri watumishi wapya, kuwapatia mafunzo muhimu watumishi wa Wizara, kuimarisha uwakilishi wetu nchi za nje, kununua majengo na magari kwa ajili ya baadhi ya balozi zetu; na

(vi) Kukusanya maduhuli ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006 Wizara imeendelea na juhudi zake za kutekeleza sera yetu mpya ya Mambo ya Nje yenye msisitizo wa diplomasia ya uchumi. Juhudi tunazofanya hivi sasa katika kuvutia wawekezaji, kuhamasisha shughuli za utalii na kutafuta masoko zinakwenda sambamba na kuwaandaa watendaji wa Wizara, wadau na wawekezaji wetu wa ndani. Maandalizi hayo ni pamoja na kuwapa taarifa mbalimbali zitakazowawezesha kuzifahamu na kuzitumia fursa za kiuchumi zinazojitokeza ndani na nje ya nchi. Ili kufanikisha hayo, Wizara yangu iliandaa mkutano wa wadau uliolenga kuongeza uelewa wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi, mwezi Agosti, 2005. Pia, Wizara iliandaa mkutano wenye malengo hayo hayo ya wadau na Mabalozi wanaotuwakilisha nje mwezi Novemba 2005. Mikutano hii ya wadau imewezesha kuteuliwa kwa maafisa maalum katika Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali watakaohusika na masuala ya diplomasia ya uchumi kwa kushirikiana na Wizara yangu, ambayo ndiyo yenye dhamana ya kuratibu sera hii.

Mheshimiwa Spika, moja ya mikakati ya Wizara ni kuandaa mikutano ya kanda ili kujadili masuala mbalimbali ya utekelezaji wa sera yetu. Katika mikutano hiyo, mabalozi waliopo Kanda za Afrika, Asia, Marekani na Ulaya walipata fursa ya kubadilishana uzoefu wa mikakati ya kutafuta wawekezaji, masoko, msamaha wa madeni na kuvutia watalii. Miongoni mwa mbinu na mikakati inayotumika ni pamoja na kuandaa na kushiriki makongamano ya biashara, uwekezaji na maonyesho ya utalii. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara iliandaa mikutano ya aina hiyo katika miji ya New Delhi, India, Mombasa Kenya, Brussels Ubelgiji na New York Marekani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha 2006/2007 Wizara yangu itaendeleza utekelezaji wa sera hii kwa kutumia njia ya mikutano, makongamano, usambazaji wa taarifa mbalimbali na kwa kushiriki katika maonyesho ya biashara, uwekezaji na utalii. Lengo letu ni kuhakikisha tunaendelea kufanya juhudi zaidi kuvitangaza vivutio vya utalii na maeneo ya uwekezaji yaliyopo Tanzania katika biashara, kilimo, madini, mawasiliano na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, moja ya mikakati ya utekelezaji wa Sera yetu ya nje ni pamoja na kutafuta misaada ya kufuatilia masuala yote yanayohusu madeni kutoka nchi na mashirika ya wahisani. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kutokana na uhusiano mzuri uliopo kati yetu na Japan, mwezi Machi 2006 Serikali ya Japan ilisaini mkataba wa Shilingi bilioni 6.6 kwa ajili ya kusaidia Tanzania kupambana na umaskini. Hali kadhalika, mwezi Juni 2006 Serikali hiyo ilitoa kiasi cha Shilingi bilioni 12.85 kwa

ajili ya kuifanyia matengenezo makubwa barabara ya Kilwa yenye urefu wa kilometa 11.6, kutoka Mivinjeni hadi Mbagala-Rangi Tatu, Jijini Dar es Salaam. Aidha, Serikali ya Japan ilitoa msaada wa kiasi cha Shilingi bilioni 13.72 kwa ajili ya kusaidia mradi wa maji huko Zanzibar. Huu ni mradi mkubwa ambao utafanywa katika awamu mbili. Kukamilika kwa mradi huu kutapunguza tatizo la maji visiwani humo kwa asilimia 50. Katika mwaka ujao 2006/2007 Wizara itafuatilia utekelezaji wa miradi hiyo kama ilivyokubalika.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine ya utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje, mwezi Aprili, 2006 Ubalozi wetu India ulifanikisha makubaliano ya mkataba kati ya hospitali ya *M/S Apollo Enterprises Limited* ya India na Bodi ya Udhamini ya Shirika la Hifadhi ya Mfuko wa Jamii *(NSSF)* ya Tanzania kwa ajili ya kujenga hospitali na kufanya shughuli za upasuaji na matibabu ya ugonjwa wa moyo hapa Tanzania.

Uanzishwaji wa hospitali hii una lengo la kuifanya huduma hiyo ipatikane hapa nchini na kupunguza gharama za kusafirisha wagonjwa hao na matunzo yao. Wizara katika mwaka ujao 2006/2007 itafuatilia utekelezaji wa mpango huu kwa kasi zaidi ili matunda ya ushirikiano wetu yapatikane haraka.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza uwakilishi wenye tija kwa Taifa letu, baada ya kufungua Ubalozi wa Muscat mwaka 2005/2006, Wizara yangu sasa inakamilisha mipango ya kufungua Balozi na uwakilishi katika nchi kadhaa. Mpango huo unatekelezwa kwa kufuatilia kwa makini maendeleo ya nchi mbalimbali na kuona ni namna gani nchi hizo zinaweza kuwa na manufaa ya kiuchumi na kibiashara kwetu. Ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mpango huo umebainisha umuhimu wa kuwa na Ubalozi nchini Brazil na Malaysia. Tunatarajia Balozi hizi mbili zitafunguliwa katika mwaka wa fedha 2006/2007. Tunaamini kwamba kwa kuwa na uhusiano wa kibalozi na nchi hizi, tutakuwa na mengi ya kushirikiana na kujifunza katika maeneo ya viwanda, biashara, kilimo na uwekezaji. Aidha, mipango ya kufungua Balozi katika nchi nyingine zenye nafasi ya kuinufaisha nchi yetu itaendelezwa na Balozi hizo zitafunguliwa kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu iliendelea kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa watendaji kutokana na umuhimu wake katika kuongeza ufanisi na tija. Ili kuhakikisha kwamba diplomasia ya uchumi inatekelezwa ipasavyo, Oktoba 2005 Wizara yangu iliandaa mafunzo maalum yaliyoitwa *Leaders of Change.*

Lengo kuu la semina na mafunzo haya ilikuwa ni kuwapa Mabalozi wetu na Viongozi wa Wizara mbinu na nyenzo muhimu za uongozi ili kukabiliana na changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo kwa nia ya kuimarisha na kuleta mabadiliko ya kimsingi katika utendaji kazi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza juhudi hizi, Wizara iliandaa semina na mafunzo elekezi kwa Wakuu wa Utawala na Fedha katika Balozi zetu. Semina zililenga kuimarisha utendaji wao katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje, kuimarisha

masuala ya utawala, utunzaji na usimamizi wa mali na fedha za Serikali na hatimaye kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia inatoa elimu kwa wananchi kwa kuandaa vipindi vya uelimishaji kupitia Televisheni ya Taifa. Hadi sasa vipindi vinane vimesharushwa kupitia kipindi cha Jarida la Uchumi cha Televisheni hiyo. Kipindi hicho kimetumika kuwaelimisha wananchi juu ya dhana ya Diplomasia ya Uchumi na jinsi inavyolenga kufungua fursa katika nyanja mbalimbali kama vile kilimo, utalii, biashara, viwanda na kadhalika. Vipindi hivi vinatarajiwa kuhamasisha wananchi ili waweze kutambua fursa mbalimbali wanazoweza kuzitumia na uwezekano uliopo wa kushiriki katika biashara za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika mfululizo wa kutoa habari na kuelimisha wananchi, Wizara ilitangaza vipindi vinavyoonyesha matukio ya Kikao cha Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwenye Televisheni ya Taifa wakati Tanzania ikiwa Rais wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, mwezi Januari 2006.

Vipindi hivyo maalum vya televisheni vililenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa nafasi hii kwa Tanzania na jinsi nchi yetu inavyotoa mchango wake katika masuala ya kimataifa. Katika mwaka 2006/2007 Wizara inaandaa mpango wa kuwa na vipindi vya kudumu vya redio na televisheni vitakavyofafanua mambo mbalimbali yanayofanywa na Wizara katika ngazi ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilielezwa mwaka 2005/2006 kwamba, migogoro mingi barani Afrika ilikuwa ikishughulikiwa na mingine ilipata ufumbuzi. Mgogoro wa Burundi ulianza kuwa na hali ya matumaini baada ya Uchaguzi Mkuu nchini humo uliofanyika mwezi Agosti, 2005 na Chama cha *CNDD-FDD* kuibuka mshindi. Hivi sasa hatua ya awali ya mazunguzo baina ya Serikali ya Chama cha *PALIPEHUTU-FNL* imefikiwa baada ya pande hizo mbili kutoa saini makubaliano ya misingi mikuu ya kuleta amani ya kudumu ya Burundi. Serikali ya Burundi na kikundi cha *PALIPEHUTU-FNL* walitia saini makubaliano hayo mwezi Juni, 2006 katika Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Nchi za Kanda uliofanyika Dar es Salaam mwezi Juni, 2006. Wizara yangu katika mwaka ujao wa 2006/2007 itaendelea kufuatilia mchakato huu kama sehemu ya jukumu lake ililopewa na viongozi wa Kanda katika kuimarisha amani ndani ya Burundi.

Kwa upande wa Sudan, Serikali ya nchi hiyo ilitiliana saini mkataba wa amani na kikundi kikubwa cha *Sudan Liberation Movement (SLM/A)* huko Abuja, Nigeria chini ya Mjumbe Maalum wa Umoja wa Afrika, Mheshimiwa Dr. Salim Ahmed Salim. Juhudi zinaendelea kuvishawishi vikundi viwili vilivyobakia vikubali kutia saini mkataba huo. Tunampongeza Mheshimiwa Dr. Salim kwa kazi nzuri anayoifanya kwa niaba ya bara letu la Afrika. Mgogoro wa Liberia umetatuliwa. Uchaguzi Mkuu ulifanyika nchini humo na Mheshimiwa Bibi Ellen Johnson Sirleaf alichaguliwa kuwa Rais. Uchaguzi huo umemfanya Bibi Ellen Johnson-Sirleaf kuwa Rais wa Kwanza mwanamke Barani Afrika. Tunampongeza sana na kuitakia nchi yake kila la kheri katika kujijenga upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya amani katika nchi za Mashariki ya Kati bado si ya kuridhisha. Baadhi ya nchi za eneo hilo zimeendelea kukumbwa na migogoro. Mgogoro wa muda mrefu kati ya Israel na Palestina bado haujapatiwa ufumbuzi ingawa Jumuiya ya Kimataifa imeendelea kufanya juhudi za usuluhishi ili kupata amani ya kudumu baina ya mataifa hayo mawili. Huko Lebanon mapigano yanaendelea kati ya Israel na kikundi cha Hizbollah kilichopo nchini Lebanon. Tanzania inaungana na mataifa mengine duniani kuziomba pande zote zinazopigana kusitisha mapigano hayo na kurudi kwenye majadiliano ya amani. Nchi yetu inasikitishwa sana na upotevu wa mali na raia wasio na hatia hususan wanawake na watoto. Kwa kutumia nafasi yetu ndani ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Tanzania itafanya kila jitihada zitakazowezesha kupatikana kwa suluhu ya migogoro hii.

Mheshimiwa Spika, nchini Iraq nako kumeendelea kuwa na hali ya wasiwasi. Hata hivyo yapo matumaini ya kupatikana kwa amani kufuatia kuundwa kwa Serikali inayohusisha makundi yote ya kijamii ikiwa ni njia mojawapo ya kuleta umoja wa kitaifa. Katika mwaka 2006/2007 nchi yetu itaendelea kutoa mchango wake ndani ya mifumo ya kikanda na ya kimataifa ili kuleta amani ya kudumu katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mwezi Januari, 2006 Tanzania katika kipindi chake cha Urais wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa iliitisha kikao maalum kuzungumzia hali ya amani, usalama na maendeleo katika Kanda ya Maziwa Makuu. Nchi zote za Kanda hiyo, Wajumbe wote wa Baraza la Usalama na nchi nyinginezo zilizoalikwa zilihudhuria katika ngazi ya Mawaziri na Mabalozi.

Kikao hicho cha Baraza la Usalama kilipitisha kwa kauli moja Azimio nambari 1653 (2006) ambalo lilidhaminiwa na Tanzania. Azimio hilo, pamoja na mambo mengine, liliutaka Umoja wa Mataifa kusaidia kwa karibu zaidi nchi za Kanda kumaliza migogoro na kuanzisha shughuli za maendeleo. Vile vile, Azimio hilo lilitaka Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Amani iliyoundwa hivi karibuni kutoa kipaumbele kwa Kanda ya Maziwa Makuu hususan kwa miradi iliyoanzishwa baada ya kumaliza migogoro, kwa lengo la kudumisha amani, kuchochea na kudumisha maendeleo. Aidha, Azimio hilo la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilitambua umuhimu wa Azimio la Dar es Salaam juu ya Amani, Utulivu, Usalama na Maendeleo, kama matokeo ya juhudi za Kanda ya Maziwa Makuu kutafuta mafanikio ya sekta hizo. Baadhi ya mafanikio ya juhudi za Kanda na Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ni kuimarika kwa amani na demokrasia katika nchi za Kanda. Mfano mzuri ni nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambayo hivi sasa inajiandaa kwa uchaguzi ambao unatarajiwa kufanyika tarehe 30 Julai, 2006.

Katika mchakao wa kuendeleza na kukuza amani katika nchi za Maziwa Makuu, kikao cha tatu cha Kamati ya Mawaziri ya Kanda ya Maziwa Makuu kilifanyika Bangui, Jamhuri ya Afrika ya Kati mwezi Februari mwaka 2006. Pamoja na kupitisha rasimu ya Mkataba juu ya amani, usalama na maendeleo, miradi ya maendeleo na Iitifaki tisa katika kutekeleza Azimio la Dar es Salaam navyo vilipitishwa. Ni matumaini yetu kwamba

Mkataba huu pamoja na miradi hiyo ya maendeleo itaweka misingi mizuri ya kuimarisha amani na kuleta ustawi katika Kanda yetu.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kwamba, Mkataba huu utatiwa saini katika kikao cha Wakuu wa Nchi na Serikali kinachotarajiwa kufanyika Desemba 2006 huko Nairobi, Kenya. Chini ya Mkataba huu Itifaki kumi na miradi ya kimaendeleo takribani 32 imeainishwa katika sekta nne: Amani na Usalama; Utawala Bora na Demokrasia; Maendeleo ya Uchumi na Utangamano wa Kikanda na Masuala ya Kibinadamu na Maendeleo ya Jamii. Mkataba huo pia utaitangaza Kanda yetu kuwa "Eneo Maalum la Ukarabati na Maendeleo." Hatua hii itachochea uwekezaji utakaozingatia manufaa kwa Kanda nzima. Katika mwaka ujao 2006/2007 Tanzania itaimarisha ushiriki wake katika mfumo huu wa kikanda na kuendelea kutoa mchango wake katika upatikanaji wa amani ya kudumu, utulivu na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na manufaa haya ya jumla kwa Kanda yetu, yapo pia manufaa mahsusi kwa nchi yetu. Kwa upande wa Tanzania utekelezaji wa Mkataba huo unategemewa kuleta miradi kadhaa. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa kuendeleza Lugha ya Kiswahili katika Kanda, kurejeshwa kwa wakimbizi makwao, kukarabati maeneo yaliyokuwa wenyeji wa wakimbizi, mradi wa kutegua mabomu ya kutegwa ardhini dhidi ya binadamu kwa kutumia panyabuku kutoka Morogoro na ukusanyaji wa silaha ndogo na nyepesi. Miradi hii yote inalenga kuimarisha mazingira ya eneo lote lililokuwa kwenye migogoro na kulirudisha katika hali ya utulivu. Katika mwaka 2006/2007 Wizara yangu itahamasisha Watanzania kufuatilia hatua zote zinazochukuliwa katika mchakao huo wa Kanda hii ili kufaidika na fursa za uwekezaji na biashara.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaendelea kuwa mwanachama wa Jumuiya mbalimbali, zikiwemo Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*, Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)*, Nchi za Maziwa Makuu na Umoja wa Nchi Zinazopakana na Bahari ya Hindi *(IOR – ARC)*. Uanachama wetu katika Jumuiya hizi ni fursa muhimu ya kuendeleza maslahi ya Taifa letu kiuchumi, kisiasa na hata kiusalama. Aidha, unatusaidia kujenga nguvu ya kupigania haki duniani na kukuza uwezo wa ushindani katika dunia ya utandawazi. Katika mwaka ujao 2006/2007 nchi yetu itaendelea kuchukua hatua thabiti za kuimarisha ushiriki wetu katika Jumuiya mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuimarisha ufanisi wa ushiriki wetu katika Jumuiya za Kikanda, Mheshimiwa Rais alifanya marekebisho katika muundo wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuunda idara kamili kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Ushirikiano wa Kikanda. Aidha, Mheshimiwa Rais tayari amemteua Balozi na Mkurugenzi wa kuongoza idara hiyo. Tunaamini kuwa kuanzishwa kwa idara hiyo kutakuza utendaji unaohusiana na shughuli za kikanda, ambazo hapo awali zilisongamana katika idara moja ya Ushirikiano wa Kimataifa. Katika mwaka 2006/2007 idara hii mpya inatarajiwa kufanya uchambuzi wa kina wa mashirikiano yetu katika Kanda ili kuweka bayana maslahi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC*, katika kikao chao cha mwezi Agosti 2005, walimteua Dr. Tomaz Augusto Salomao kutoka Msumbiji kuwa Katibu Mtendaji wa *SADC* kwa kipindi cha miaka minne na Bwana Joao Samuel Caholo kutoka Angola kuwa Naibu Katibu Mtendaji kwa kipindi hicho. Kwa kupitia Bunge lako Tukufu, tunawapongeza viongozi hawa wawili kwa kuteuliwa kwao kuongoza menejimenti ya Jumuiya ya *SADC.* Katika mwaka 2006/2007 nchi yetu itaimarisha ushirikiano wake kwa viongozi hawa na Jumuiya ya *SADC* kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa uteuzi wa hawa watendaji wakuu kumeingiza nguvu mpya ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Maendeleo wa *SADC (Regional Indicative Strategic Development Plan),* pamoja na ule wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama *(Strategic Indicative Plan for the Organ).*

Mipango hii ndiyo inayotoa dira ya maendeleo inayolenga kuimarisha uchumi, kuimarisha hali ya maisha, kulinda uhuru pamoja na kuimaisha ulinzi na usalama wa raia wa Jumuiya ya *SADC.* Katika mwaka ujao wa 2006/2007 Wizara yangu itafuatilia kwa umakini mkubwa utekelezaji wa mipango hii kwa manufaa ya Taifa letu na Kanda ya *SADC* kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na nyenzo sahihi za kuweza kutekeleza Mpango wa maendeleo katika ngazi ya Kikanda, Sekretarieti ya *SADC* imeajiri wataalam mbalimbali kulingana na matakwa ya kimuundo ya Jumuiya. Wataalam hawa watasaidia kuratibu shughuli mbalimbali kulingana na idara 5 zilizoko kwenye Sekretarieti. Kati ya wataalam hao walioajiriwa, watano (5) wanatoka Tanzania na hivyo kujaza nafasi zote zilizotengwa kwa ajili ya Tanzania kulingana na mgawanyo wa ajira kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC* uliofanyika Gaborone, Botswana mwezi Agosti 2005, Wakuu hao waliiteua Tanzania kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chombo cha *SADC* kinachohusika na Kuratibu Masuala ya Siasa, Ulinzi na Usalama. Hivyo, itakapofika mwezi Agosti 2006, Tanzania itachukua nafasi ya Uenyekiti wa Chombo hiki kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Mara baada ya kuwa Mwenyekiti, Tanzania itakuwa na jukumu la kuwa mwenyeji wa vikao vya Wakuu wa Nchi na vile vya Mawaziri na kuratibu shughuli nyingine za Chombo hiki cha *SADC.* Katika mwaka ujao 2006/2007, Wizara itatekeleza kwa makini jukumu lake hilo la Uenyekiti la kuratibu masuala ya Siasa, Ulinzi na Usalama katika Kanda ya *SADC.*

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa umoja wa *SADC* unapata Makao Makuu yenye hadhi, kila nchi mwanachama imetakiwa kuchangia kiasi cha Dola za Marekani 500,000,000. kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu huko Gaborone, Botswana. Mpaka sasa michango iliyokwishakusanywa imeshafikia jumla ya Dola za Marekani 5,212,218. Hivi sasa zabuni imetangazwa ili ipatikane kampuni itakayojenga ofisi hizo. Tanzania katika mwaka 2005/2006 imetimiza wajibu wake kama mwanachama kwa kuchangia kiasi cha Dola 500,000. kama ilivyokuwa imeahidi.

Mheshimiwa Spika, ninafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Jumuiya ya *SADC* imeanzisha mradi maalum wenye lengo la kuandika historia ya harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika. Mradi huu ambao umepewa jina la Hashim Mbita, kwa heshima ya Mtanzania mwenzetu katika harakati za ukombozi, unatekelezwa kwa kutumia fedha zilizochangwa na nchi wanachama. Mradi wa Hashim Mbita ni muhimu sana kwa Tanzania kwani utaweka kumbukumbu sahihi za harakati za ukombozi ambao nchi yetu ilichangia kwa kiasi kikubwa. Katika mwaka 2006/2007 Tanzania itatia ushirikiano wa hali ya juu katika kuharakisha ukamilishaji wa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Nchi Zinazopakana na Bahari ya Hindi *(IOR-ARC).* Katika mwaka 2005/2006 jumuiya hii ilipitia mikakati ya utekelezaji wa mipango ya kukuza biashara na uwekezaji baina ya nchi wanachama. Katika mkutano uliofanyika Tehran, Iran, mwezi Februari 2006, Mawaziri walikubaliana kwa pamoja kuwa na dira ya utekelezaji wa ushirikiano wa kibiashara na uwekezaji. Katika mwaka 2006/2007 Wizara itasimamia utekelezaji wa mikakati hiyo na kuangalia namna bora ya kuendeleza ushirikiano huu katika maeneo mengine ya kiuchumi, sayansi na teknolojia.

Tanzania pia ni mwanachama wa Umoja wa Afrika *(UA).* Serikali ya Awamu ya Nne, iliyojengwa juu ya misingi imara ya awamu zilizotangulia, inaamini kwamba umoja na mshikamano ndizo nguzo sahihi kwa mafanikio na ustawi wa Waafrika. Kwa kutambua dhamira ya Tanzania katika shughuli za Umoja wa Afrika, nchi wanachama zimekuwa zikituunga mkono katika masuala mbalimbali yanayohusu umoja huu. Ni kwa sababu hiyo, katika kikao cha sita cha kawaida cha Viongozi na Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja huu kilichofanyika Khartoum, Sudan, Januari 2006, Tanzania ilichaguliwa kuwa mwenyeji wa Mahakama ya Haki ya Afrika. Mahakama hiyo inatarajiwa kuwa na makazi yake mjini Arusha. Zipo faida nyingi zitakazotokana na nchi yetu kuwa mwenyeji wa Mahakama hiyo. Baadhi ya faida hizo ni ongezeko la kipato kwa Taifa kutokana na matumizi ya miundombinu yetu, ajira kwa Watanzania, upanuzi wa wigo wa biashara ya utalii na heshima kwamba nchi yetu inaheshimu haki, utawala wa sheria, amani na utulivu. Katika mwaka 2006/2007 Wizara yangu itafanya maandalizi yote yanayohitajika ili azma ya kuanzishwa Mahakama hiyo mjini Arusha itimie haraka. Kama mwanachama wa *UA,* Tanzania inaunga mkono mipango ya umoja huu ya kuliimarisha bara letu. Mojawapo ya mipango hii ni Mpango wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Kiuchumi Barani Afrika *(NEPAD*) unaoshughulikia mambo makuu mawili. Kwanza, kukuza ubora wa maisha kwa Waafrika kwa kubuni miradi itakayochochea ukuaji wa uchumi katika nchi za Afrika.

Pili, *NEPAD* inalenga kulinda maslahi na maisha ya wananchi wa Afrika kwa kuimarisha utawala mzuri chini ya mpango wa kusimamia utekelezaji wa vigezo vya utawala bora unaojulikana kama *African Peer Review Mechanism (APRM).* Serikali yetu tayari imekwisharidhia kujiunga na mpango huo na Mheshimiwa Rais alitoa saini Mkataba wa Makubaliano mwezi Juni 2006 mjini Dodoma. Wizara katika mwaka 2006/2007 itashirikiana na nchi nyingine kupitia Mfuko wa *NEPAD* kwa nia ya kutekeleza maudhui ya mpango huu. Katika mwaka 2005/2006 nchi yetu imeendelea

kutumia Tume ya Kudumu za Ushirikiano kati yake na nchi nyingine duniani ili kudumisha, kuendeleza na kukuza uhusiano mwema wa kisiasa na kiuchumi. Tanzania inazo Tume za namna hiyo kati yake na nchi kumi na nane (18) duniani. Wizara yangu inaendelea kupitia upya malengo ya Tume hizo ili kubaini maeneo machache yanayotekelezeka na yenye tija zaidi. Wizara yangu inaendelea vile vile kubaini nchi za kuanzisha nazo Tume mpya za ushirikiano ili kujenga mazingira ya kunufaika ziadi. Hivi karibuni, mwezi Mei, 2006 ulifanyika mkutano wa uzinduzi wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Brazil, katika Mji wa Brasilia nchini Brazil. Maeneo ambayo Tanzania inategemea kunufaika na kwa ushirikiano huo ni pamoja na nishati, madini, michezo, kilimo, utalii na afya. Katika mwaka ujao 2006/2007, Wizara itafuatilia kwa karibu utekelezaji wa makubaliano ya Tume hiyo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Tume nyingine iliyofanyiwa katika mwaka 2005/2006 ni ile ya Ushirikiano na Cuba, ambapo Tanzania imefanikiwa kupata Madaktari 12 wa tiba za magonjwa ya binadamu, nafasi 8 za masomo ya shahada ya kwanza kwa wanafunzi katika fani za elektroniki, michezo na udaktari. Pia, nchi hii imekuwa na ushirikiano uliohusisha Taasisi ya Utafiti wa Tiba ya Cuba ijulikanayo kama *LABIOFAM* katika eneo la utafiti wa ugonjwa wa malaria. Katika mkutano wa 14 wa Tume hii uliofanyika Arusha, Tanzania, mwezi Machi 2006 makubaliano yalifikiwa kuendeleza ushirikiano wa pande hizi mbili katika maeneo mbalimbali ya uzalishaji na huduma. Tanzania ni moja ya nchi zinazotekeleza Malengo ya Milenia yaliyokubalika na Jumuiya ya Kimataifa. Mnamo mwezi Septemba, 2005 Wakuu wa Nchi na Serikali mbalimbali duniani, ikiwemo Tanzania, walikutana New York, Marekani kutafakari utekelezaji wa malengo hayo. Katika kikao hicho viongozi walikubaliana, pamoja na mambo mengine, kuzisaidia nchi maskini duniani kuondokana na umaskini uliokithiri kwa kuchukua hatua mbalimbali kama vile kuzifutia madeni. Katika mkutano huo viongozi hao pia walijadili na kukubaliana haja ya kuufanyia marekebisho muundo wa Umoja wa Mataifa, hususan, Baraza Kuu la Usalama la Umoja huo ili lifanye shughuli zake kwa demokrasia na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mkutano huu wa Wakuu wa Nchi, mwezi Februari, 2006 Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Dr. Kofi Annan aliunda Jopo la Watu 13 Mashuhuri Duniani, likiwajumuisha viongozi kutoka Bara la Afrika, Asia, Ulaya na Amerika. Jopo hilo liliundwa ili kutekeleza azma ya wanachama wa Umoja wa Mataifa ya Kubadilisha muundo wa Umoja wa Mataifa kwa lengo la kuuimarisha zaidi na kuongeza ufanisi wake. Vile vile, Mheshimiwa Tony Blair, Waziri Mkuu wa Uingereza aliunda jopo linalofahamika kama *Investment Climate Facility for Africa,* ikiwa ni juhudi za utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Afrika. Tanzania imebahatika kuwa na uwakilishi wa Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwenye majopo haya. Ushiriki wake katika vyombo hivyo ni heshima kubwa kwa nchi yetu na bara la Afrika. Tunampongeza sana Mheshimiwa Mkapa na Wizara yangu inamuahidi kila ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu hayo ya Kimataifa. *(Makofi)*

Ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kufikia malengo ya Milenia, Tanzania imekuwa ikishirikiana katika mikutano na vikao mbalimbali vya Umoja wa Mataifa vinavyohusu maendeleo stahimilivu. Mwezi Mei, 2006 Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 14 wa Kamisheni ya Maendeleo Stahimilivu *(Commission for Sustainable Development)* uliofanyika New York, Marekani. Mkutano huu ulizungumzia maeneo ya nishati kwa maendeleo stahimilivu, maendeleo ya viwanda na mabadiliko ya hali ya hewa. Aidha, mkutano huu ulitoa fursa kwa Tanzania kueleza mikakati ya kuhifadhi mazingira ambapo juhudi hizo zimetambuliwa Kimataifa. Mkutano huo ulikuwa ni chachu ya kubadilishana uzoefu katika matumizi ya maendeleo ya viwanda, kukabiliana na uharibifu wa mazingira pamoja na mabadiliko ya hewa. Katika mwaka ujao 2006/2007 Wizara itashirikiana na Wizara mbalimbali na Taasisi husika katika kuendeleza malengo ya Kamisheni hii kuhusu maendeleo stahilimivu, hususan, katika kuhamasisha utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa Helsinki ni moja ya nyanja ya kujadili matokeo na athari za utandawazi. Mwaka 2005/2006, Wizara yangu ililiarifu Bunge lako Tukufu juu ya mchakato wa Helsinki kuhusu Utandawazi na Demokrasia. Mchakato huu uliasisiwa mwaka 2003 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wakati alipokuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na mwenzie wa Finland, Mheshimiwa Dr. Erkki Tuomioja. Awamu ya Kwanza ya kazi za Mchakato huu ilihitimishwa wakati wa Kongamano la Helsinki la 2005 – *Mobilising Political Will,* ambako ripoti ya mwisho ya mchakato huu iliwasilishwa rasmi. Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu na Mheshimiwa Tarja Halonen, Rais wa Finland, walipata fursa ya kushiriki na kulifungua rasmi Kongamano hilo. Kongamano hilo lilizungumzia kwa kina umuhimu wa utashi wa kisiasa katika kuhimiza utawala bora na maendeleo. Napenda nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, awamu ya pili itahusu utekelezaji wa mapendekezo ya Ripoti ya Mchakato wa Helsinki. Awamu hii itajielekeza kwenye maeneo ya Utawala Bora, usalama wa watu, haki za binadamu, mazingira, umaskini na maendeleo. Katika Mchakato huu, Tanzania na Finland zimekubaliana kushirikiana kwenye utekelezaji wa ajenda ya umaskini na maendeleo. Kwa upande wa Tanzania, ajenda kuu itakuwa ni “Ukuaji wa Uchumi na Ajira” na mkutano wa kuizungumzia ajenda hii utafanyika Novemba, 2007, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka wa 2006/2007 Mchakato wa Helsinki umedhamiria kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yote yaliyopo kwenye ripoti yake kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali duniani. Nchi zifuatazo zimejitolea kuandaa mikutano kadhaa ya utekelezaji huo. Nchi hizo ni Malaysia, Mexico, Misri, Canada, Thailand, Hispania na Uingereza. Naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kuwa kazi za awamu ya pili ya Mchakato wa Helsinki zitahitimishwa kwenye Mkutano Mkuu utakaofanyika Novemba, 2007 Dar es Salaam, Tanzania.Kuhusu Kongamano la Uchumi la Dunia kwa Afrika ambalo Mheshimiwa Jakaya Kikwete alishiriki kikamilifu lilifanyika mjini Cape Town, Afrika ya Kusini mwezi Juni, 2006, madhumuni ya Kongamano hilo yalikuwa ni kuwakutanisha viongozi wa Afrika, wafanyabiashara na wakuu wa makampuni kutoka Afrika na duniani kote kwa lengo la kubadilishana mawazo na uzoefu katika masuala ya maendeleo stahimilivu na kukua kwa uchumi

barani Afrika. Ilibainika kwamba changamoto kubwa ni jinsi ya kuendelea kukuza uchumi wa Afrika kwa kuweka sera nzuri na madhubuti. Katika mwaka ujao 2006/2007 Wizara yangu itashirikiana na Wizara nyingine katika uendelezaji wa sera zinazolenga kuongeza kasi ya kukuza uchumi na kujenga mazingira ya kuliletea Taifa letu maendeleo stahimilivu.

Novemba, 2005 Wakuu wa Nchi na Serikali walikutana huko Malta kwa ajili ya mkutano wa wanachama wa Jumuiya ya Madola. Katika Mkutano huo, pamoja na mambo mengine, viongozi walizingatia kwamba demokrasia na maendeleo havitengani – vinakwenda pamoja na kwamba utawala bora ni chachu ya maendeleo stahimilivu. Wakati huo huo umaskini na matabaka katika jamii vinaathiri demokrasia. Walisisitiza nia yao ya kufanikisha malengo ya Milenia. Aidha, walijadili masuala ya biashara na maendeleo, haki za binadamu, demokrasia, ugaidi, umaskini, teknolojia na matabaka katika jamii na biashara ya Kimataifa yenye manufaa kwa nchi zote. Kwa mwaka 2006/2007 Wizara yangu itatoa mchango wake katika kufanikisha maeneo haya ya Malengo ya Milenia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mwaka 2005/2006 Tanzania iliwasilisha mgombea wa nafasi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wabunge wa Nchi Wananchama wa Jumuiya ya Madola Dr. William Francis Shija. Ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya mchujo mkali na usaili wa hali ya juu, jina la Dr. Shija lilipitishwa dhidi ya wagombea wengine wengi. Ni imani yetu kwamba uteuzi wa Dr. Shija utathibitishwa na Mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Wabunge wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola utakaofanyika Abuja, Nigeria mwezi Septemba, 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania pia ni mwanachama wa kundi la Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote. Mwezi Mei, 2006, nchi yetu ilishiriki katika Mkutano wa Mawaziri wa nchi hizo uliofanyika Patrajaya, Malaysia kuandaa mkutano wa kumi na nne wa Wakuu wa Nchi na Serikali unaotarajiwa kufanyika mwezi Septemba, 2006, nchini Cuba. Mkutano huo utakaofanyika Cuba unatarajiwa kujadili masuala ya ushirikiano kati ya nchi wanachama na mjadala kuhusu Sahara ya Magharibi. Tunategemea Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ataliwakilisha Taifa letu katika Mkutano huu muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ushiriki wa Tanzania katika Jitihada za Kimataifa za Kupambana na Magonjwa, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba, mnamo miaka ya 2000 na 2001, Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika walijiwekea mikakati ya kupambana na magonjwa ya UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu ambayo yameathiri Afrika kwa kiasi kikubwa. Kikao hiki kiliweka pia msimamo wa pamoja wa Nchi za Afrika, uliowasilishwa katika kikao cha Wakuu wa Nchi na Serikali kilichofanyika New York mwezi Mei, 2006. Madhumuni ya kikao hiki yalikuwa ni kufuatilia mafanikio ya utekelezaji wa mikakati ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI, iliyopitishwa katika Azimio la mwaka 2001. Kwa pamoja viongozi hao walikubaliana kutoa tamko rasmi lililoweka wazi haja ya kuwepo kwa msukumo wa kisiasa mkubwa zaidi katika ngazi za juu ili kuimarisha harakati za kupambana na UKIMWI. Katika mwaka 2006/2007,

Tanzania itaendelea kuunga mkono jitihada hizi kupitia programu mbalimbali za ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushirikiano wa Kimataifa na Kikanda, Wizara yangu pia inaratibu ushirikiano kati ya Tanzania na nchi moja moja.. Kwa mfano, Bara la Asia lina nchi zenye uchumi unaokua kwa kasi zijulikanazo kama *Asia Tigers*. Nchi hizo ni miongoni mwa nchi washiriki wetu wa maendeleo katika nyanja za ufundi, teknolojia na biashara. Kutokana na hayo, nchi yetu imeshirikiana na itaendelea kushirikiana na nchi hizo kwa karibu ili kuweza kujifunza maeneo yote yenye manufaa kwetu. Wizara yangu ikishirikiana na wadau wetu wa maendeleo itaendeleza juhudi za kuwawezesha Watanzania kutumia fursa mbalimbali zinazotolewa na nchi hizi kwa kutoa taarifa kuhusu masoko, ubia, teknolojia utalii na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, ziara za viongozi ni mojawapo ya njia muhimu za kukuza ushirikiano. Katika mwaka 2005/2006 kulikuwa na ziara ya Viongozi wa Ngazi za Juu wa Serikali kati ya Tanzania na China. Hivi karibuni Mheshimiwa Wen Jiabao, Waziri Mkuu wa China, alifanya ziara nchini Tanzania kwa mwaliko wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Kutokana na ziara hiyo Serikali ya China imeahidi kushirikiana na Tanzania katika sekta ya afya, hususan mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria. Vilevile, China imeahidi kutusaidia katika maeneo ya elimu, kilimo, ujenzi wa uwanja wa mpira wa kisasa na uimarishaji wa Reli ya Uhuru ya *TAZARA. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha vivutio vyetu vya utalii vinafahamika nchini China, mwezi Agosti, 2005 Wizara yangu ikishirikiana na Bodi ya Utalii ya Tanzania Bara, na ile ya Zanzibar, ziliratibu ziara ya wapiga picha wa televisheni na redio kutoka China kuja kupiga picha vivutio vya utalii wa Tanzania kwa lengo la kuvitangaza nchini mwao. Kama sehemu ya matokeo ya kazi hiyo mwezi Machi, 2006 kikundi cha watalii wapatao 36 kutoka China kilitembelea mbuga za wanyama za Tanzania. Matukio haya yameongeza uelewa wa wananchi wa China kuhusu vivutio na raslimali mbalimbali zinazopatikana Tanzania. Katika mwaka ujao 2006/2007 juhudi kama hizi zitaimarishwa na kutekelezwa katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inao mpango wa maendeleo ujulikanao kama *Tanzania Mini –Tiger Plan,* 2020. Mpango huu unahusu uanzishaji wa shughuli za kiuchumi katika maeneo maalum ili kuharakisha maendeleo ya nchi yetu. Katika utekelezaji wake wamejitokeza Wajapani ambao walitembelea Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa madhumuni ya kuangalia uwezekano wa kuanzisha kiwanda kipya cha kukamua ufuta, kutathmini gharama za kupanua na kuimarisha mfumo wa usafirishaji, uwezekano wa kuanzisha mifumo ya umwagiliaji na uzalishaji wa mazao mashambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nchi nyingi za Bara la Asia, ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Tanzania imeanzisha mfumo wa mashauriano ya kila mwaka kati yake na *Vietnam* ili kukuza na kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizi mbili. Vile vile, Tanzania na Indonesia zinaendelea kujadiliana kuhusu haja ya kuanzisha Tume ya Kudumu ya pamoja ya Ushirikiano ili kudumisha na kuendeleza ushirikiano

wetu katika nyanja za kibiashara, uwekezaji, elimu utamaduni, afya, usafirishaji na kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kukuza na kuendeleza ushirikiano kati yetu na Jamhuri ya Korea, Waziri wa Mambo ya Nje na Biashara, Mheshimiwa Ban Ki-Moon wa nchi hiyo, alitembelea Tanzania mwezi wa Mei, 2006. Miongoni mwa masuala yaliyojitokeza katika ziara hiyo ni pamoja na mjadala juu ya Mkakati Mpya wa Korea kwa maendeleo ya nchi za Afrika, ambayo ni fursa mpya ya mahusiano ya kiuchumi na maendeleo baina ya nchi hizi. Aidha, katika ziara hiyo, kulikuwepo na makubaliano ambayo Tanzania inatarajia kunufaika nayo katika mafunzo ya ufundi, ujenzi wa angalau daraja moja na teknolojia ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba, baada ya kubaini umuhimu wa Thailand katika maeneo ya kiuchumi, Tanzania inatarajia kukamilisha hatua za kuingia Mikataba na Thailand katika nyanja za utafiti, masuala ya usafirishaji wa anga, uwekezaji na biashara. Katika mwaka 2006/2007 Wizara itafuatilia kwa karibu utekelezaji wa Mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Amerika na Ulaya, nchi yetu imeendelea kukuza ushirikiano na Amerika ya Kaskazini, Kusini na Ulaya. Katika ushirikiano huo, Serikali ya Tanzania imeendelea kupata misaada katika maeneo ya Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), uchangiaji katika Bajeti ya Serikali, mapambano dhidi ya UKIMWI, huduma za afya, maendeleo ya sekta binafsi na Utawala Bora. Misaada hii imetoka katika nchi mbalimbali za Jumuiya ya Ulaya na Amerika ya Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano kati ya Tanzania na baadhi ya Mataifa ya Ulaya ni wa kihistoria. Kutokana na ushirikiano huo, Serikali ya Tanzania imeendelea kunufaika na misaada ya kimaendeleo kutoka Serikali za Hispania, Italia, Ireland, Poland, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Urusi na nchi za Skandinavia. Misaada hiyo imelenga sekta ya elimu, afya, ujenzi wa miundombinu, utunzaji wa mazingira, nishati, sekta binafsi, Utawala Bora na misaada ya fedha katika Bajeti ya Serikali. Kati ya misaada hii, ipo misaada iliyotoka nchi moja moja za Ulaya na ile iliyotoka katika nchi hizo kama kundi la nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya.

Mheshimiwa Spika, Tanzania pia inaimarisha mahusiano na nchi nyingine za Ulaya. Katika mwaka 2005/2006, Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya *Czech*, aliitembelea Tanzania mwezi wa Februari, 2006. Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Waziri huyo, aliambatana na wafanyabiashara wakubwa ishirini, kwa malengo ya kutafuta sehemu za uwekezaji na kufanya biashara na Tanzania. Ziara hiyo imefungua mahusiano ya kisiasa na kiuchumi. Vile vile, Tanzania imehudhuria maonesho mbalimbali ya biashara yaliyofanyika nchini Urusi mwezi Januari, 2006. Maonesho hayo yalijikita katika nyanja za utalii na madini. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itafuatilia fursa zote zinazotokana na ziara hizi na vile vile ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na nchi za Bara la Ulaya.

Mheshimiwa Spika, Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alitembelea Marekani mwezi Mei, 2006. Moja ya mafanikio ya ziara hiyo ni Tanzania kuingia katika mpango wa kuondoa umaskini, ulioandaliwa na Serikali ya Marekani unaoitwa *Millennium Challenge Account*. Kwa kuanzia Serikali ya Marekani, kupitia mpango huo, imekubali kutoa dola 11.15 milioni ambazo zitatumika kusaidia vita dhidi ya rushwa nchini. Ni matumaini yangu kuwa, mpango huu pia utasaidia vita dhidi ya umaskini. Katika mwaka 2006/2007 Wizara yangu itafuatilia kwa karibu utekelezaji wa mpango huu wa *Millennium Challenge Account.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kuratibu masuala mbalimbali ya kiitifaki. Viongozi wa Serikali wa Kitaifa walitembelea nchi mbalimbali kwa ziara za kikazi. Katika ziara hizo, viongozi hao walizuru nchi za Afrika Kusini, Botswana, Falme za Kiarabu, Finland, Italia, Kenya, Lesotho, Libya, Malta, Marekani, Msumbiji, Namibia, Rwanda, Ufaransa, Uganda, Uholanzi, Uingereza, Uswisi, Swaziland na Zimbabwe. Ziara hizi zilikuwa za mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, nchi yetu ilitembelewa na Viongozi wa Serikali mbalimbali, kwa madhumuni ya ziara za kikazi. Viongozi waliofanya ziara nchini Tanzania walitoka Afrika Kusini, Burundi, China, Comoro, Congo, Denmark, Ireland, Kenya, Lethotho, Malawi na Zambia.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu, Wizara yangu imeendelea kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi, kuhusu upatikanaji wa *visa* katika Balozi mbalimbali, hususan Balozi za Marekani na Uingereza, kwa ajili ya wanaohitaji kusafiri kwenda nchi hizo. Wizara yangu imekuwa ikijitahidi kutatua tatizo hili kwa njia za kidiplomasia. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu italifuatilia kwa umakini mkubwa suala hili na inakusudia kufanya jitihada zaidi za kuondoa tatizo hilo kwa mujibu wa taratibu za kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, katika siku za karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la maombi kutoka kwa watu mbalimbali ya kutaka kuwa Wawakilishi wa Heshima wa Nchi yetu. Vile vile kumekuwepo na maombi kutoka nchi nyingi rafiki ya kutaka kufungua ofisi za Wawakilishi wa Heshima nchini Tanzania. Ili kukidhi mahitaji yote hayo na kwa kutambua umuhimu wa kuwa na uwakilishi mkubwa wa nchi yetu, hasa katika kipindi hiki cha diplomasia ya uchumi, Wizara yangu imeandaa taratibu mpya za uteuzi na utendaji kazi wa Ofisi za Wawakilishi wa Heshima wa Nchi. Lengo la taratibu hizo ni kupata wawakilishi wa heshima walio bora, waaminifu, wenye sifa na rekodi nzuri na wenye nia thabiti na hadhi ya kuiwakilisha nchi yetu. Katika mwaka ujao 2006/2007, Wizara itakamilisha taratibu zote zinazohusu eneo hili kwa nia ya kuimarisha uwakilishi wa nchi mbalimbali kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Wizara yangu umekuwa ukirekebishwa kila inapobidi ili kukidhi haja ya kuwa na utendaji mzuri na wenye tija, pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia ya uchumi yanayotokea duniani. Kutokana na mabadiliko hayo, hivi sasa Muundo wa Wizara umerekebishwa na kuwa na idara kumi kutoka nane, pamoja na vitengo vitano kutoka vinne. Mabadiliko yaliyofanyika ni pamoja na kuigawa idara iliyokuwa ya Afrika na Mashariki ya Kati na

kuwa Idara mbili, yaani Idara ya Afrika peke yake na Idara ya Mashariki ya Kati. Aidha, katika mabadiliko hayo hayo, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa imegawanywa na kuwa Idara mbili, yaani Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Idara ya Ushirikiano wa Kikanda. Kwa upande wa vitengo, Wizara imeongeza kitengo kipya cha Ugavi na Manunuzi. Ni matarajio yetu kwamba, hatua hizi zitaongeza kasi na ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa wakati. Pamoja na hayo, zoezi la kubainisha mahitaji halisi ya watumishi limeanza na linategemewa kukamilika mwaka wa fedha wa 2006/2007, kwa kushirikiana na Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, ingawa mabadiliko haya ni chanya na yenye manufaa, kuongezeka kwa idara na vitengo, kumeongeza pia tatizo la uhaba wa nguvu kazi, ikizingatiwa kuwa Wizara yangu imekuwa na upungufu wa wafanyakazi wa kada zote kwa muda mrefu sana. Wizara ina watumishi 366 tu, wakati mahitaji halisi ya watumishi ni 478. Katika jitihada za kukabiliana na tatizo hili, katika mwaka 2005/2006, Wizara iliajiri jumla ya watumishi 16. Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ili kuziba pengo hilo na katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara itaajiri watumishi wapya 48 wa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006, Wizara yangu iliendelea na jitihada za kuimarisha mazingira ya kazi, kwa kukarabati ofisi zetu za Makao Makuu na zile za Idara ya Mambo ya Nje Zanzibar. Hivi sasa ofisi zimewekwa samani mpya, tumewapatia watumishi wote ngamizi zilizounganishwa na mtandao wa mawasiliano, yaani *internet*, tumeimarisha kiwango cha ubora wa mazingira ya ndani na nje ya ofisi na kununua jenereta kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la kukatika kwa umeme. Aidha, katika mwaka 2006/2007, tutaimarisha mtandao wa mawasiliano kati ya Makao Makuu na Balozi zetu na pia tutaanzisha tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005, Wizara ililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu kuanzishwa programu ya mafunzo ya Wizara. Zoezi hili lilikwenda sambamba na zoezi la kurekebisha Muundo wa Wizara. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu tena kuwa, kwa vile Muundo wa Wizara umekamilika, tunatarajia kuwa na programu ya mafunzo nayo itakamilika mapema katika mwaka 2006/2007. Programu hii itakuwa ndiyo dira yetu ya mafunzo kwa miaka mitatu ijayo. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara iliwagharimia watumishi watano, kozi za muda mrefu katika fani za biashara na utawala na stashahada ya utunzaji kumbukumbu. Aidha, Wizara yangu iligharimia mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi ishirini kwenye fani ya uandishi wa hotuba na taarifa mbalimbali, utunzaji wa kumbukumbu, uongozi na udreva. Mafunzo haya kwa ujumla, yameongeza ufanisi wa utendaji kazi wa watumishi wetu. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaongeza kasi ya kuwapeleka watumishi katika mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa kuzingatia programu hii ya mafunzo na changamoto zinazotokana na utekelezaji wa sera ya diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linalofanyiwa kazi na Wizara yangu ni la posho za watumishi wa nje *(Foreign Service Allowance*), ambazo mara ya mwisho zilihuishwa mwaka 1979. Viwango vilivyopo viliwekwa kwa kuzingatia hali ya uchumi ya wakati huo, yaani miaka 27 iliyopita. Hali ya uchumi duniani imebadilika hivi sasa na gharama za maisha katika vituo vingi zimeongezeka. Kwa kutambua tatizo hili, Wizara

imechukua hatua ya kuhuisha kwa awamu, posho za utumishi wa nje, kwa kutoa nyongeza kidogo ya muda. Katika kipindi cha mwaka huu wa fedha (2006/2007), posho za utumishi wa nje zitapitiwa upya (*Comprehensive Foreign Service Allowance Review*), ili zizingatie hali halisi ya maisha katika vituo vyetu. Aidha, kanuni za utumishi wa nje *(Foreign Service Regulations)*, zitapitiwa sambamba na posho za utumishi wa nje katika mwaka wa fedha 2006/2007. Ni matarajio yetu kwamba, mabadiliko haya yataongeza ari na hamasa ya utendaji kwa watumishi wa Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kwamba, kuwepo kwa vitendea kazi bora, huongeza ufanisi wa wafanyakazi. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa mpango mkakati wa miaka 15 wa kununua na kujenga majengo katika balozi zake zote. Kwa kupitia utaratibu huo, mpaka sasa Wizara yangu imefanikiwa kupata majengo sita yanayotumika kama ofisi na nyumba 17 za kuishi maofisa wetu. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Hazina, itaongeza kasi ya kutekeleza mpango huo. Ni imani ya Wizara yangu kwamba, utaratibu huu utatupunguzia gharama na kutuondolea adha ya kupanga.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Diplomasia ambacho kiko chini ya Wizara yangu, kimeongeza idadi ya madarasa kutoka manne mwaka 2004/2005 hadi manane na maabara ya kompyuta yenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya wanafunzi 70. Idadi hii inajumuisha maabara ya lugha, yenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya wanafunzi 30 kwa wakati mmoja. Pia kuna darasa maalumu kwa ajili ya Maafisa Waandamizi 30. Mabadiliko haya yamekiwezesha chuo kuongeza idadi ya wanafunzi wake kutoka 112, wakiwemo wanawake 39 katika mwaka 2004/2005, hadi 241, wakiwemo wanawake 130 katika mwaka 2005/2006.

Aidha, ongezeko hili la wanafunzi, limeongeza pia mapato ya chuo kwa asilimia mia tatu, kutoka shilingi milioni 80 mwaka 2004/2005 hadi shilingi milioni 273, mwaka 2005/2006. Ni matarajio yangu kwamba, katika mwaka 2006/2007, wanafunzi wataongezeka sambamba na juhudi zinazoendelea za kuongeza wigo na ubora wa mafunzo hapo chuoni.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, kutokana na takwimu hizo hapo juu, Chuo cha Diplomasia kimeendelea kufanikiwa katika kuleta mabadiliko ili kukidhi haja ya Sheria Namba 7 ya mwaka 2005, iliyobadilisha Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu *(Higher Education Accreditation Council)* na hivi sasa kujulikana kama Tume ya Vyuo Vikuu *(Tanzania Commission for Universities).* Lengo la mabadiliko haya ni kukiimarisha katika nyanja za taaluma, utoaji huduma za utafiti na ushauri kwa wadau mbalimbali, kuimarisha muundo wa uendeshaji wa chuo, kuimarisha hali za wafanyakazi, pamoja na kuongeza idadi ya wanafunzi, vyumba vya madarasa na programu.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kutekeleza mabadiliko haya, chuo kitaanza kutimiza masharti ya Tume ya Vyuo Vikuuc kwa kurekebisha mkataba uliokiunda na kutunga sheria mpya. Sambamba na hatua hizi, katika mwaka 2006/2007, chuo kitaandaa mkakati wa maendeleo kwa kurekebisha mitaala, kuandaa mpango wa miaka mitano na mpango mkuu wa matumizi ya ardhi na kuimarisha miundombinu ya chuo.

Mheshimiwa Spika, taasisi nyingine iliyo chini ya Wizara yangu ni Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha, ambacho kinaendelea kufanya kazi vema na kutoa mchango wake katika Pato la Taifa. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Kituo kiliweza kuwa mwenyeji wa mikutano 120, asilimia 40 ikiwa ni mikutano ya Kimataifa na asilimia 60 ni ya Kitaifa. Mikutano hii imeleta wajumbe wapatao 14,000 Mjini Arusha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Kituo kimeweza kukusanya jumla ya shilingi 4,044,233,285, kutokana na mikutano pamoja na vyanzo vingine vya mapato na kupata ziada ya shilingi 913,802,052/=. Mwaka 2006/2007, Kituo kimepanga kuingiza mapato ya shilingi 4,401,714,325/=, ambalo ni ongezeko la asilimia nane kutoka katika mikutano na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Katika mwaka 2006/2007, matarajio ya Kituo ni kuongeza idadi ya mikutano kwa kujitangaza na kutoa huduma bora zaidi. Azma hii inalenga kuifanikisha kauli mbiu ya kituo ambayo ni "Tunaileta Dunia Tanzania" *(We bring the World to Tanzania).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Wizara yangu ilipangiwa kutumia jumla ya shilingi 49,373,206,300/= kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizi, kiasi cha shilingi bilioni tisa zilitegemewa kukusanywa na Wizara kama maduhuli kutoka katika Balozi zetu kutokana na mapato ya mauzo ya *visa.* Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2006, Wizara yangu ilikwisha kutumia kiasi cha shilingi 55,217,481,017/=, kiasi ambacho ni ongezeko la shilingi 5,844,274,717/= au asilimia 11.8.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya bajeti kwa mwaka 2005/2006 yalikuwa ni kukusanya jumla ya shilingi 9,169,600,000/=. Hadi kufikia Juni 30, 2006, Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 9,569,999,333/=, kiasi ambacho ni sawa na mafanikio kwa asilimia 4.4 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi na malengo ambayo nimeyataja katika vifungu mbalimbali vya Hotuba yangu, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2006/2007, itatekeleza, pamoja na kazi nyingine, malengo makuu muhimu kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 kama ifuatavyo:-

- Kuendelea kuiletea nchi yetu maslahi ya kiuchumi kwa kuwavutia wawekezaji wenye mitaji na teknolojia ya kisasa na watalii.

- Kuendeleza Sera ya ujirani mwema na nchi jirani.

- Kushiriki katika kuimarisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (*EAC*), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Nchi za Afrika (*SADC*), Umoja wa Nchi za Afrika *(UA)*, Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande wowote (*NAM*) na Umoja wa Mataifa.

- Kulitangaza jina la nchi yetu na kuitetea heshima yake miongoni mwa Mataifa.

- Kudai mageuzi katika umoja wa Mataifa kwa lengo la kuongeza sauti za nchi zinazoendelea na;

- Kuitambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi ughaibuni *(Tanzanians in the Diaspora)* na kuweka utaratibu utakao wawezesha kuchangia maendeleo ya Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza kwa ukamilifu majukumu na malengo yake ya 2006/2007, kama nilivyoeleza katika hotuba hii, naomba Bunge lako Tukufu, lijadili na kisha liidhinishe jumla ya shilingi 52,736,298,000/= kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007. Kati ya fedha hizo, shilingi 50,317,870,300/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 2,418,427,700/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Waziri wa Mambo ya Nje, siyo tu kwa hotuba nzuri, lakini iliyowasilishwa kwa *standard* za Kimataifa. Ndugu wageni wetu, mnayemwona ni Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mbunge wa Jimbo la Kilindi, lililoko Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nchi za nje kwanza kabisa, kwa kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi ngazi ya Taifa, Mheshimiwa Yusufu Rajab Makamba, kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi ngazi ya Taifa, pia naipongeza Sekretarieti nzima ya Chama cha Mapinduzi kwa kuteuliwa kushika nyadhifa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati yangu mbele ya Bunge lako Tukufu. Wakati wa kuchambua makadirio haya, Waziri aliieleza Kamati kwa kina, kuhusu Sera ya Wizara katika kipindi hiki ambapo

imeshuhudia na inaendelea kushuhudia, mabadiliko makubwa duniani katika nyanja za uchumi, sayansi na teknolojia.

Kutokana na mabadiliko hayo, Sera iliyopewa uzito ni Diplomasia ya Uchumi katika nyanja zote zinazohusika na masuala ya uchumi ikiwemo biashara, utalii, uwekezaji, masoko na elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Wizara imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, katika mwaka huo wa fedha, Wizara ilikabiliwa na matatizo yafuatayo:-

- Kushuka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Kimarekani, *Euro* na kadhalika. Hali ambayo imesababisha maofisa wetu walioko nje ya nchi, kuishi maisha magumu sana.

- Upungufu wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu kwa ukamilifu.

- Ukosefu wa kasma ya maendeleo.

- Uhaba wa watumishi wenye sifa stahili.

- Uchakavu wa magari Wizarani na katika baadhi ya Balozi.

- Ufinyu wa nafasi ya Jengo la Makao Makuu ya Wizara.

- Nyumba nyingi katika baadhi ya Balozi zetu ni chakavu kwa sababu ya kukosa fedha za ukarabati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutatua matatizo yaliyo orodheshwa hapo juu, kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007, Wizara pamoja na mambo mengine, imepanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kuendelea kuratibu na kutekeleza Mkakati wa Sera ya Diplomasia ya Uchumi katika nyanja za utalii, biashara, uwekezaji, Maonesho ya Kimataifa na kadhalika.

- Kuendelea kukusanya maduhuli ya Serikali.

- Kuajiri watumishi wapya na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Wizara.

- Kuendelea kujenga na/au kununua majengo kwa ajili ya Balozi zetu.

- Kuendelea kuimarisha uwakilishi wetu nchi za nje na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza kikamilifu kazi zilizotajwa hapo juu, Wizara inaomba kiasi cha shilingi 52,736,298,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuijadili bajeti ya hiyo, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao: Kwanza, juhudi za kuboresha Balozi zetu nje ya nchi, ziendelee hasa kwa kununua majengo kwa mfumo wa kulipia taratibu *(Mortgage System),* badala ya kuendelea kupanga kila mwaka. Aidha, Balozi zipewe vitendea kazi vya kutosha ikiwemo kununuliwa magari.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa Wizara hii ina majukumu mengi ya kutekeleza, ikiwemo kununua au kujenga nyumba kwa ajili ya Balozi na watumishi wa Balozi hizo nchi za nje, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, Wizara hii ipewe kasma ya maendeleo au ufanywe utaratibu wa kutumia maduhuli wanayoyakusanya ili wayatumie kwa ajili ya mipango ya maendeleo *(Retention Scheme).*

Mheshimiwa Spika, Tanzania imebahatika kwa kuwa lugha yake ya Taifa ni moja ya lugha za Kimataifa. Serikali ifanye juhudi, kuwaandaa Watanzania kuchukua ajira za kuifundisha lugha hii nje ya nchi. Aidha, kuwe na mpango maalum wa kufundisha walimu wa lugha ya Kiswahili na kuwatafutia kazi nje ya nchi, kama zinavyofanya nchi nyingine katika zama hizi za utandawazi.

Mheshimiwa Spika, Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Arusha (*AICC*), umekuwa ukiitangaza nchi yetu duniani. Hata hivyo, Ukumbi huo kwa sasa unashindwa kukidhi viwango vya Kimataifa kwa kuwa haukujengwa kwa ajili ya mikutano bali kwa ajili ya matumizi ya ofisi. Hivyo, Kamati inashauri Serikali, ijenge ukumbi mpya wa kisasa, kwa ajili ya Mikutano ya Kimataifa kama ilivyofanya katika ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo Jijini Dar es Salaam. Ukumbi huu siyo tu utaendelea kuitangaza nchi yetu duniani, bali utaongeza ajira na kukuza uchumi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali itoe eneo lililopo Hoteli ya Saba Saba Jijini Arusha, kwa ajili ya kujenga ukumbi mpya wa kisasa wa Mikutano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, tano, ili kutekeleza Diplomasia ya Uchumi, ni vema kuwe na Mkakati Maalum wa kuwatafutia Watanzania ajira nje ya nchi ikiwemo mashirika mbalimbali ya Kimataifa. Aidha, Serikali iwaandae Watanzania kwa kuwafundisha lugha mbalimbali za Kimataifa ili kuwawezesha kufanya kazi katika taasisi hizo. Nchi nyingi kwa sasa, zinapata fedha nyingi za kigeni kutoka kwa watu wao, wanaofanya kazi nje ya nchi. Aidha, kuwe na utaratibu wa kuwafahamu Watanzania wanaoishi na kufanya kazi nje ya nchi na kutafuta namna ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, sita, katika kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda, Serikali ya Tanzania iweke wazi, msimamo wake na sababu za msimamo huo, kuhusu kuwemo katika ushirikiano huo. Tanzania inashirikiana na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)*, wakati huo huo Kenya na Uganda ziko *COMESA* na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hali hii inaweza

kudhoofisha uchumi wa nchi, kwa kuwa na taratibu na mikataba mbalimbali ya ushirikiano wa kiuchumi ambayo mingine inaweza kuwa na vipengele vinavyopingana.

Mheshimiwa Spika, saba, kwa kuwa tunakuwa na Balozi zetu nje ya nchi kwa manufaa ya nchi yetu kiuchumi na kisiasa, ni vema kila ubalozi wetu ukapimwa ufanisi wake *(Performance Audit),* katika kuinua uchumi wa nchi kwa kuvutia wawekezaji, kutangaza utalii, kueleza masoko na bidhaa zinazopatikana huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nane, utekelezaji wa Diplomasia ya Kiuchumi, unahitaji nguvukazi yenye taaluma maalum na iliyohamasika vya kutosha. Serikali iangalie namna ya kuhamasisha Watendaji wa Wizara hii, hususan walio nje ya nchi katika Balozi zetu kwa kuwapa mishahara na marupurupu, yanayoendana na hali ya maisha katika nchi wanazofanyia kazi, ikiwemo kupewa Bima ya Matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tisa, katika kukuza uelewa wa masuala ya Diplomasia Kitaifa na Kimataifa, ni vema Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa *(Centre for Foreign Relations),* kikaendelea kuboreshwa kwa kukamilisha upatikanaji wa Hati Miliki ya ardhi kilipo kituo hicho. Aidha, kwa kuwa kituo hiki kinatarajia kuwa Chuo Kikuu Kishiriki, Kamati inashauri litafutwe eneo lingine, lililo kubwa zaidi, litakalofaa kwa maendeleo ya Kituo hiki muhimu na litakalofaa kwa upanuzi unaokusudiwa kufanywa.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara hii, hazitoshi kukamilisha majukumu yake kwa ukamilifu. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwe na usimamizi madhubuti wa sheria na taratibu za fedha ili fedha hizo ziweze kusaidia kutekeleza majukumu ya Wizara ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikinunua na kukarabati majengo mbalimbali kwa ajili ya Balozi zetu nje ya nchi. Kwa kuwa moja ya kazi za Bunge, kwa mujibu wa Katiba ya nchi ni kuisimamia Serikali, Kamati inasisitiza umuhimu wa Kamati ya Mambo ya Nje, kutembelea Balozi zetu ili kujiridhisha na utendaji wa Balozi hizo, ikiwemo kuona ubora wa majengo na vitendea kazi vilivyopo katika Balozi hizo. Hii itaisaidia Kamati kutoa ushauri mzuri zaidi kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa heshima kubwa, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Asha-Rose M. Migiro, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi na Mheshimiwa Dr. Cyril A. Chami, wote wakiwa Manaibu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirkiano wa Kimataifa, Balozi Charles Mutalemwa, Katibu Mkuu na Maofisa wote wa Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa kuwasilisha bajeti hii mbele ya Kamati yetu na hatimaye kuifikisha mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru sana, Waheshimiwa Wabunge, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, kwa michango yao ya kina, wakati wa kujadili mapendekezo ya bajeti hii. Tafadhali naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Mohamed G. Dewji, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Balozi Khamis S. Kagasheki, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha na Mheshimiwa Zaynab M.Vulu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Mheshimiwa Anne S. Makinda na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, kwa uongozi makini katika kuliendesha Bunge letu Tukufu. Tunawapongeza na kuwashukuru sana. Aidha, namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S. L. Foka na Watumishi wote wa Bunge, kwa kufanikisha maandalizi ya taarifa hii. Vile vile nawashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi na Ndugu Neema Kiula, kwa kuratibu shughuli za Kamati hii mpaka kuwezesha taarifa hii kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kamati yangu inaunga mkono mapendekezo ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2006/2007, ambayo ni shilingi 52,736,298,000/=. Naomba Bunge lako Tukufu likubali kuijadili na hatimaye kuipitisha bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii, ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa mwaka wa fedha 2006/2007, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1), Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika,, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema na uzima. Aidha, nachukua fursa hii, kuwashukuru sana Viongozi wa Chama changu cha Wananchi *CUF*, kwa kunipa fursa ya kugombea tena na hatimaye kushinda na kuwafanya Wananchi wa Jimbo la Gando, waweze kunichagua kwa kura nyingi na kuniamini kunipa dhamana hii nzito ya kuwawakilisha katika chombo hiki nyeti sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, pamoja na wenzetu wote katika Kambi ya Upinzani, kwa msaada na maelekezo mazuri waliyonipa wakati wa kuandaaa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa ushauri na michango mbalimbali waliyonipa. Namshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na wasaidizi wake, kwa miongozo na misaada yao. Naungana na wenzangu kuwapongeza viongozi wote, walioaminiwa kihalali kuongoza vyama na vyombo mbalimbali vya kiutendaji. *(Makofi)*

Baada ya shukrani hizo, naomba sasa nianze moja kwa moja kutoa kwa kifupi sana, maoni ya Kambi yetu ya Upinzani, juu ya hoja hii iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, naanza na Sera ya Wizara. Wizara ya Mambo ya Nje ni kubwa na ya muhimu sana kuliko ambavyo tunafikiria, kwani mageuzi yote ya kiuchumi yanayotokea hapa nchini, chanzo chake ni Wizara hii. Pindi sera zake zikishindwa kuwa na mtazamo endelevu, basi nchi yetu inaweza hata kuwekwa rehani. Aidha, kama watendaji wake wakiweka maslahi binafsi kuliko ya Taifa katika utendaji, matokeo yake ni wananchi kuwa omba omba kwa wageni katika nchi yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Wizara hii ndio inayotoa taswira ya nchi yetu katika nyanja za Kimataifa, lakini inatupasa kukumbuka kuwa, nchi yoyote duniani, zilizoendelea na zinazoendelea, ziwe za Kaskazini au Kusini mwa Dunia, inapoandaa Sera zake za Mahusiano ya Kimataifa, huzingatia mambo makuu mawili; usalama wa nchi *(security)* na faida za kiuchumi kwa Taifa *(welfare)*.

Mheshimiwa Spika, usalama wa nchi au kama Waingereza wanavyoita, *security*, ni dhana pana sana. Tunapozungumzia usalama, hatuzungumzii hofu ya kuvamiwa kwa nchi yetu na majeshi ya nje tu, bali tunazungumzia usalama wa ardhi yetu, madini yetu na vitega uchumi vyetu na sekta nyingine za kutoa huduma ambazo kwa njia moja ama nyingine ni muhimu katika kuendesha uchumi wa nchi yetu visichukuliwe au kuhodhiwa na wageni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia *welfare*, tunawalenga moja kwa moja wananchi na kwamba, wananufaika vipi na sera zetu za uhusiano wa Kimataifa katika kuendesha maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, mambo hayo mawili usalama na *welfare*, yakijumuishwa hutengeneza kile ambacho Waingereza wanakiita *national interest*, naomba nitumie neno maslahi ya nchi, kwani ni ukweli usiofichika kuwa, sera za kila nchi juu ya uhusiano wa Kimataifa zinazingatia maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tukiziangalia kanuni *(principles)*, ambazo Tanzania ilizizingatia katika kuandaa sera zake za mahusiano ya Kimataifa katika miaka ya 1960, katika kipindi cha uongozi wa Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, sote tutakubaliana kuwa, kanuni hizo zilizingatia maslahi ya Taifa. Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa, mwaka 2001 ilizichukua kanuni hizo na nyingine zilifanyiwa marekebisho kama vile kuunga mkono jitihada za kutokomeza

ubaguzi wa rangi Afrika Kusini na kuunga mkono katika kupinga ukoloni, kwa kuwa zilikuwa haziendani na dunia ya leo.

Mheshimiwa Spika, kanuni mpya zilizozingatiwa ni kudumisha uhusiano wa ndani zaidi wa kiuchumi na washiriki wetu wa maendeleo *(Development Partners).* Hii iliwekwa ili kukidhi matakwa ya utandawazi. Sio lengo langu kizisoma kanuni hizi, bali natoa changamoto kwa Watanzania wote, walio makini na nchi yao *(Attentive Public)* kuwa, kanuni hizi ndio msingi wa kuanzia, ambapo Wizara inaandaa sera zake za mahusiano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, suala ni kwamba, ingawa kanuni hizo zina nia nzuri kwa nchi na wananchi katika mahusiano yao na nchi za nje, lakini kuna tatizo linapokuja suala la kuandaa na kutekeleza sera hizo. Hapo ndipo panapotokea tofauti za tafsiri, utofauti huo umeonekana hasa katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mchakato mzima katika sekta ya uwekezaji, unazua maswali kama kweli tuna moyo wa kizalendo au tunajali maslahi ya nchi ambayo ni maslahi ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna mikataba mingi ambayo Serikali imeingia na makampuni ya wawekezaji wa nje, ambayo haiko wazi kabisa. Kwa hili tunampongeza Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuligundua hilo na nia yake njema ya kutaka kuipitia upya Mikataba hiyo.

Kambi ya Upinzani tunasisitiza kuwa, maslahi ya Taifa yazingatiwe katika Mikataba hiyo ili tusije tukauza nchi yetu na wajukuu wetu wakakosa miliki katika nchi yao. Aidha, tunaitaka Serikali iwaeleze wananchi, kulingana na misingi mikuu ya utungaji wa Sera za Nje kama nilivyozieleza hapo juu, Watanzania wamenufaika vipi na ushirikiano wa wawekezaji wa kigeni.

Mheshimiwa Spika, katika kuongelea uwekezaji, nimeona ni lazima tuzitenge sekta katika makundi matatu. Kundi la kwanza, nitaliita sekta nyeti. Naomba niiweke sekta ya madini katika kundi hili. Watanzania tunashindwa kuthamini rasilimali hii muhimu na ya kiupendeleo, ambayo Mungu ametujalia. Tuna madini adimu kama *Tanzanite*, ambayo hayapatikani popote duniani. Katika habari zisizo rasmi sana, tunaambiwa kuwa, Baba wa Taifa, alikataa madini yasichimbwe mpaka Watanzania wawe wamesoma na kuna wataalamu wazalendo wa kuishughulikia rasilimali hii ya thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii sekta hii inamilikiwa na watu wa nje, wanavuna malighafi ambazo hatujui thamani yake na wawekezaji hao, tunaowaita washirika wa kimaendeleo, wanaenda kuendeleza nchi zao na si Tanzania. Kambi ya Upinzani, inauliza kweli hapa *national interest* zinalindwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kisingizio chetu ni kuwa sekta hii inahitaji mtaji mkubwa. Ni kweli Watanzania binafsi, pengine hawataweza kuendesha miradi mikubwa kama hii, lakini Serikali yetu inaweza. Kama miradi hii ya thamani itaendeshwa vizuri, basi matatizo ya bajeti za barabara, maji katika majiji na miji yetu, yangetatuliwa kutokana na mapato ya sekta hii ya thamani. Wenzetu walioendelea, hawakuanza kubinafsisha thamani zao katika hali ya chini ya uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi la pili ni Sekta za Huduma *(Service Sector)*, zinazohitaji mitaji mikubwa. Kwa mfano, makampuni ya simu, usafirishaji na kadhalika. Hizo tunaweza kuwakaribisha wawekezaji. Sababu ni kwamba, wenyewe hatuna mitaji hiyo lakini huduma hizo ni muhimu katika maisha yetu ya kila siku. Maadamu hao wawekezaji kutoka nje wanatafuta faida, basi wanakaribishwa kuja kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, kundi la tatu ni sekta za mitaji midogo, aidha za uzalishaji au za kutoa huduma, hizo tuachiwe wenyewe Watanzania tunaziweza, hatuhitaji kupeleka wataalamu wakasome nje ili waje kutengeneza chapati. Basi utakuta wawekezaji wengi kutoka nje, wamewekeza katika *ice cream* na sekta nyingine ndogo ndogo, ambazo tunaziweza. Hapo tunaongeza ushindani usio na sababu kwa wawekezaji wetu wa Tanzania na hili tunadhani, Wizara hii kupitia kwenye balozi zetu, wanahusika kwa kiasi kikubwa katika hali hii, kwani watu hao ni lazima wapate vibali kabla ya kuja Tanzania.

mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutupia jicho misamaha ya kodi wanazopewa wawekezaji kutoka nje, wanapoanzisha biashara zao nchini, kwani limekuwa jambo la kawaida wawekezaji hawa kubadilisha majina na hati za umiliki wa biashara hizo, kila unapokaribia mwisho wa msamaha huo wa kodi. Serikali inapoteza mapato kutokana na ujanja kama huo.

Mheshimiwa Spika, vilevile pamekuwa na tabia ya wawekezaji kutoka nje, kuingiza bidhaa kama matunda na viungo, ambavyo hapa nchini vinapatikana. Kwa nini zisafirishwe nyanya kutoka nje wakati Iringa na kwingineko Tanzania wanazalisha nyanya nzuri na nyingi kwa matumizi ya hoteli?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa, Balozi zetu nchi za nje ziwe makini, kuwatahadharisha wawekezaji hawa mapema. Hili litawezekana tu endapo Wizara itaweka misingi na kanuni zinazokubalika na zinazolinda maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika wa Serikali kufanya mabadiliko katika sera ya uwekezaji ili kuzingatia mustakabali wa Taifa. Maoni yetu ni kuwa, ili mwekezaji apate kibali, basi ni lazima aingie ubia na Mtanzania. Hii itasaidia kuwakwamua Watanzania kiuchumi, lakini pia kudhibiti ujanja ambao umekuwa ukiikosesha Tanzania mapato ya kodi na megineyo. Hili linawezekana na linatumika katika nchi nyingi za Asia, Mashariki ya Mbali na hapahapa Afrika kama ilivyo *DRC*. Katika sekta hii ya uwekezaji, tusiweke rehani maslahi ya Taifa kwa minajili ya mahusiano mazuri na Mataifa ya nje.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa kupitia Wizara hii, imeweza kukuza mahusiano mazuri na nchi mbalimbali, pamoja na mashirika ya Kimataifa. Kama inavyotarajiwa, mahusiano hayo mazuri, yanapaswa kuendelezwa na Mabalozi wetu katika kutangaza biashara zetu huko nje.

Mheshimiwa spika, Serikali inapaswa kutambua kuwa, kazi hii sio ndogo hata kidogo. Katika mahusiano ya Kimataifa, pamoja na ukweli kwamba, sera za ndani ndizo zinazojitokeza zaidi katika kuandaa sera za nje, lakini watendaji wa kidiplomasia, ndio kioo cha nchi yetu katika macho ya Mataifa na pia katika kufanikisha adhma yetu ya mahusiano na Mataifa hayo.

Mheshimiwa Spika, taswira hii ya nchi yetu katika nyanja za siasa, uchumi na utamaduni itapewa nakshi pale tu timu hiyo ya wanadiplomasia, itakapokuwa imeundwa kwa umakini zaidi. Umakini ninaouzungumzia hapa ni pamoja na kujali taaluma na sifa binafsi za kiutendaji *(personal integrity)* katika kuteua timu ya wanadiplomasia hao.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mbali na mahusiano ya kisiasa, ni lazima tuwe na waambata wa biashara, badala ya kuwa na waambata wa kijeshi tu katika Balozi zetu nchi za nje. Tunasema hili kwa mantiki ya kuwa waweze kuangalia ni vipi nchi yetu na watu wetu, wanaweza kufanya biashara na kuwekeza katika nchi za wenzetu. Mfano mzuri nchi ya *DRC*, bado kuna mwanga mkubwa wa uwekezaji kibiashara katika nchi hiyo.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika ambapo uteuzi wa Mabalozi na Wawakilishi wengine wa nchi yetu, usiwe wa kuzingatia ukada wa chama au umwenzetu, kwani hao makada au wenzetu, mara nyingine hawafanyi kazi kwa ufanisi zaidi na ndipo kuikosesha nchi mafaniklio, ambayo yangepatikana kutokana na kuwepo kwao katika Balozi hizo.

Mheshimiwa Spika, suala la kuichukulia Wizara hii kama Wizara nyeti, kwa mantiki ya kuwapeleka watendaji watiifu wasioweza kazi *(loyal but incompetent),* haitaisaidia Tanzania katika dunia hii ya leo ya utandawazi.

Mheshimiwa Spika, ingawa sera yetu mpya ya mambo ya nje, inaliweka mbele suala la mafanikio kiuchumi, lakini bado *values* za nchi yetu katika masuala ya mambo ya nje, zimebaki palepale. Sera yetu mpya bado inaamini kuwa Watanzania ni marafiki wa wanyonge wote duniani. Kamwe sera yetu mpya ya mambo ya nje, haikusema kuwa tunapaswa kuwa marafiki wa kila nchi, hata kama ni wakandamizaji wa haki za ndugu zetu wa kihistoria, ambao bado wanaendelea kunyanyaswa.

Mheshimiwa Spika, kihistoria, Tanzania imekuwa mfano wa kuigwa kutokana na msimamo wake thabiti wa kusimamia haki za wanyonge duniani. Tanzania ndiyo ilikuwa kitovu cha wapigania uhuru na haki duniani kote na hili lilitupa heshima kubwa katika medani za siasa za Kimataifa na hili limetupa heshima kubwa na nguvu za kimaadili *(Moral Authority)* na kuheshimika.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka kadhaa, nchi yetu ilikuwa imesitisha mahusiano ya Kibalaozi na Taifa la Israel kutokana na kukalia kimabavu, ardhi ya Wapalestina na vitendo vyake vya kuwanyanyasa ndugu zetu Wapalestina. Hata hivyo, mara baada ya Viongozi wa Taifa la Israel na watu wa Palestina, Hayati Yitzark Rabin wa Israel na Hayati Yasir Arafat wa Palestina, kusaini makubaliano ya amani kule Oslo, Norway mnamo mwezi Septemba, 1993. Serikali yetu ilionelea ni vyema kurudisha mahusiano yetu na Taifa la Israel katika maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Spika, kadri siku zinavyokwenda, utawala wa Israel umekuwa ukionyesha kila dalili za kutokuwa tayari kuwa Taifa la amani, lenye kuheshimu sio tu haki za Wapalestina, bali hata Maazimio mbalimbali ya Umoja wa Mataifa. Ni dhahiri matendo ya Taifa la Israel katika miaka ya hivi karibuni ni kinyume na matumaini ya makubaliano ya amani ya Oslo, ambayo ndiyo yalikuwa dira ya kurudisha mahusiano yetu na Taifa hilo.

Mheshimiwa Spika, mashambulio ya kinyama dhidi ya watu wa Palestina na hivi karibuni Taifa la Lebanon, ni mifano ya wazi kuwa hali ya mambo katika Mashariki ya Kati sasa si sawa na ile ambayo ilikuwepo wakati ule tulipoamua kurudisha mahusiano yetu na Taifa hilo.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa, hatutaweza kuendelea kufumbia macho ukorofi na uonevu huu. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kwa kupitia Bunge lako Tukufu, kutoa msimamo kuhusu mashambulizi yanayoendelea Lebanon na katika ardhi za ndugu zetu wa Palestina. Tunaishauri Serikali, ipitie upya maudhui ya mahusiano yetu na Taifa hilo.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Dar es Salaam ni moja ya taasisi zinazofanya kazi chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Katika Ripoti ya Mafanikio ya Wwizara hii katika Serikali ya Awamu ya Tatu, imeelezwa kuwa, Chuo kimefanikiwa kwa kuongeza programu zake kutoka nne hadi tisa. Programu hizo zinalenga masuala ya *Management of Foreign Relations, Economic Diplomacy, Defence and Security Management, Strategic Studies, Conflict Resolution, Peace Studies, Protocols and Public Relations* na *International Relations and Diplomacy.*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inahoji ni jinsi gani Chuo hicho kinasaidia katika kufanya tafiti mbalimbali katika programu hizo na jinsi ambavyo zingesaidia katika kuandaa Sera za Mahusiano ya Kimataifa ya Wwizara hiyo, pamoja na kujiunga au kujitoa katika Jumuia za Kimataifa na Kikanda (kama ilivyokuwa kwa *COMESA*), kuikubali au kuikataa Mikataba mbalimbali ya Kimataifa, nchi na makampuni ya Kimataifa? Chuo kinawezeshwa vipi ili kiweze kutimiza majukumu makubwa kilichopewa? Watumishi wa Chuo hicho, kama walimu/wahadhiri wanaandaliwaje ili wabebe majukumu hayo mazito na kwendana na mabadiliko yanayotokea hivi sasa ulimwenguni?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, Chuo hicho cha Diplomasia kiwe *think tank* ya Wizara kwa kufanya tafiti mbalimbali, kutanabaisha hali ya kiuchumi na kisiasa ya Kimataifa ili Watendaji wa Wizara, waweze kupata ushauri kutoka kwa watafiti wa chuo hicho, pamoja na kuandaa semina mbalimbali kwa Watendaji wa Serikali ili kuboresha taaluma zao katika masuala ya uhusiano wa Kimataifa. Hili litawezekana tu pale ambapo chuo hicho kitakuwa na mpango wa muda mrefu wa kuwaandaa wataalamu, waliobobea katika taaluma hizo kwa kuwapeleka kusomea katika vyuo mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya maduhuli ya Serikali katika Balozi zetu kama Ripoti ya Wizara inavyoonesha, yamekuwa yakiongezeka kuanzia shilingi 54,382,199.05/= mwaka 1997/98 hadi shilingi 7,217,094,021.65/= mwaka 2003/2004. Hii inaonesha kuwa, kama Serikali itakuwa makini zaidi, mapato hayo yataongezeka zaidi na kupanua Mfuko wa Hazina ya Taifa. Tunatambua ya kuwa mafanikio hayo yameletwa na uhimizwaji wa Sera ya Diplomasia ya Kiuchumi, kwa kuwahimiza Mabalozi kuhamasisha wawekezaji kutoka nje, utalii na kupigania ufutiwaji wa madeni. Kambi ya Upinzani, inapenda kuelewa ni mapato gani ambayo yalichangiwa na kila Balozi kwa mwaka uliopita na Serikali imechukua hatua gani kwa Mabalozi ambao utendaji wao haukuridhisha katika kuhamasisha ukusanyaji wa maduhuli hayo?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imekuwa ikifuatilia kwa ukaribu mno, hali ya ushiriki wa nchi yetu katika jumuiya hizi za masoko ya uchumi. Tumekuwa tukishangazwa na jinsi maamuzi yanavyochukuliwa pengine kwa haraka na namna maamuzi hayo, yanavyozua hoja nyingi kwa watu wanaojali mstakabali wa nchi yao. Kambi ya Upinzani inataka maelezo kwa nini Tanzania ilijitoa katika *COMESA*?

Mheshimiwa Spika, maamuzi hayo ya kujitoa yalifikiwa kwa maslahi binafsi ya viongozi na si kwa kutumia wataalam tulionao katika masuala na biashara za Kimataifa, kwani baadhi ya wanachama wa soko hilo wanafaidika na matumizi ya barabara na bandari zetu katika kusafirisha bidhaa zao. Tanzania inanufaika vipi pale inapofanya biashara na nchi za jumuiya hii, ambazo imejitoa uanachama?

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi ya Upinzani pia inapenda kuelewa namna Tanzania inavyonufaika na jumuiya za kiuchumi kama *SADC, EAC* kwa kuzingatia ukuzaji wa biashara za ndani katika jumuiya hizo, ajira kwa Watanzania katika jumuiya hizo na ukinara wa Tanzania katika kufanya maamuzi ambayo yanaziathiri nchi wanachama zote katika jumuiya hizo. Tunaishauri Wizara iwe inatoa habari muhimu kwa njia zinazoweza kuwafikia wananchi wa kawaida kwa urahisi zaidi ili wajue ushiriki wa nchi yao katika jumuiya hizo, kwani ukweli ni kwamba, wanachi wa kawaida, bado hawajafahamu namna jumuiya hizo zinavyoweza kuwa na manufaa kwao na kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, matumizi mazuri ya fedha za walipakodi wetu ni kielelezo madhubuti cha Utawala Bora, unaozingatia uwajibikaji kwa kila sekta nchini Tanzania. Hata hivyo, uhalisia wa mambo unaonesha kuwepo kwa ubadhirifu kwa baadhi ya Ofisi za Serikali yetu katika Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Ripoti

ya *CAG* katika miaka miwili iliyopita, imeonesha kuwepo kwa kasoro katika matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, wananchi tulio makini na mstakabali wa nchi yetu, bado tunahoji juu ya nini hasa kilitokea kwenye Ubalozi wa Tanzania kule Rome, Italia kilichopelekea matumizi mabaya ya fedha? Kambi ya Upinzani inapenda ipate maelezo ya kina, juu ya kashfa hiyo na hatua zipi za kiuwajibishwaji zimechukuliwa kwa wale wote waliohusika na sakata hili?

Aidha, Mheshimiwa Waziri, analieleza nini Bunge kuhusu matumizi sahihi ya fedha katika Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa, kulingana na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali?

Mheshimiwa Spika, *AICC* imeweza kuwa mwenyeji wa mikutano mbalimbali ya Kimataifa na kazi yake tunaithamini sana. Hata hivyo, ni lazima tukubali ukweli kwamba, kwa hali tuliyonayo sasa, Kituo hiki ni kidogo na hakiwezi kukabiliana na mahitaji ya mikutano mikubwa ya Kimataifa. Kambi ya Upinzani inapendekeza kwa Serikali kuwa, wakati umefika sasa wa kujenga kituo kipya kikubwa cha mikutano ili kiweze kukidhi mahitaji ya kisasa. Ni vyema tukajiuliza, kama tutapewa nafasi ya kuandaa Mkutano wa *African Union* tutafanyia wapi?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, kituo kipya cha mikutano chini ya Wizara hii kijengwe Mjini Bagamoyo. Tuna sababu nyingi za kuipendekeza Bagamoyo:-

- Kuuendeleza mji huo maarufu wa kihistoria, ambao kwa siku za karibuni hapajakuwa na jitihada za makusudi za kuuendeleza;

- Kukuza utalii katika mji huo, wenye vivutio vingi kama magofu na hifadhi mpya ya Saadani, ambazo watalii wengi hawazijui. Hii itasaidia pia kuhamisha mkusanyiko mkubwa wa watalii katika vivutio vya kitalii vya Ukanda wa Kaskazini *(Northern Circuit)* na kuwahamishia Ukanda wa Kati na Kusini, kwa manufaa ya uhifadhi wa mazingira yetu, bila kuathiri idadi ya watalii wanaokuja nchini; na

- Bagamoyo ipo karibu sana na Jiji la Dar es Salaam hivyo, hakutakuwa na tatizo la malazi kwa wageni hao kutoka nchi mbalimbali katika muda ambao hoteli bora zaidi zitakuwa zinajengwa katika mji huo maarufu - Bwagamoyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, kama Wizara itazingatia mapendekezo haya, ni dhahiri kuwa tutaweza kuwa wenyeji wa mikutano mingi ya Kimataifa na huku tukipanua miji yetu na kuvitangaza vivutio vyetu vya kitalii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nje inapaswa sasa kujua ni Watanzania wangapi wako nje. Kwa kutumia Mabalozi wetu, tunapaswa kujua watu wetu wapo nchi gani, ni wangapi na wanasaidiaje kunyanyua uchumi wa nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Benki ya Dunia, inaonesha kuwa, *remittance or transfer of fund* kwa Watanzania waishio Marekani tu kuja nchini ni dola za Kimarekani milioni mia mbili kwa mwaka. Hii sio fedha ndogo, lakini haionekani kutajwa katika bajeti yetu. Hii inatokana na kutokuwa na takwimu kamili za wananchi hao walioko nje na wanavyoleta mapato ambayo ni muhimu katika kukua kwa uchumi wa nchi yetu. Kambi ya Upinzani inamwomba Waziri wa Wizara hii, alisimamie kwa ufanisi zaidi jambo hili muhimu.

Mheshimiwa Spika, tunaelewa umuhimu wa kuthamini na kukuza lugha yetu ya Taifa, yaani Kiswahili, ambapo vilevile Wizara hii inaweza kwa kiasi kikubwa, kusaidia ukuaji wa lugha hii. Balozi nyingi za nchi za nje kama Ubalozi wa Ufaransa, Ujerumani na kadhalika, wana *cultural centers,* ambapo wamekuwa wakitoa mafunzo ya lugha zao katika kila nchi ambazo wana mahusiano nao ya kidiplomasia. Balozi zetu hazina budi kuzingatia kuwepo kwa *center* kama hizo ili kuwafundisha lugha yetu wananchi tunaoshirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, katika kuzungumzia nchi na sekta binafsi za nchi mbalimbali, zinazofanya jitihada binafsi ya kutaka kujua Kiswahili, Kambi ya Upinzani inapenda kuelewa Wizara hii imesaidia vipi katika kupata nafasi za ajira kwa walimu wa Kiswahili nje ya nchi yetu, kwani, zipo taarifa zisizo rasmi kuwa, nchi ya Libya ilihitaji zaidi ya walimu 1,000 wa Kiswahili; je, ni Watanzania wangapi wamepata nafasi hiyo?

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kulingana na mahitaji ya utandawazi, hivi sasa ipo haja ya Serikali yetu, kutilia mkazo sana mafunzo ya lugha nyingine za kigeni kama Kifaransa, Kiarabu, Kihispaniola, Kijerumani na nyinginezo. Hali halisi inaonesha kuwa, ni Watanzania wachache wanaajiriwa katika Mashirika ya Kimataifa na moja ya sababu ni watu wetu kutoelewa lugha za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, Chuo cha Diplomasia kiwe na programu ya kufundisha lugha hizi muhimu katika ulimwengu wa sasa wa utandawazi ili si tu kuiwezesha timu ya wanadiplomasia kuwasiliana na nchi tunazoshirikiana nazo, bali hata kuwaandaa wataalamu mbalimbali, watakaopata ajira katika Mashirika ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inathamini sana, juhudi za Serikali za kufungua ofisi za kibalozi katika maeneo muhimu ya kiuchumi. Ni dhahiri kuwa, kwa sasa wafanyabiashara wengi wa nchi yetu na Afrika Mashariki kwa ujumla, wananunua bidhaa Dubai, Falme za Kiarabu na nchi za Mashariki ya mbali, kama vile Thailand, Malaysia, Singapore, Indonesia na China.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa, Serikali yetu ifungue Ubalozi katika Kanda hii ya Mashariki ya Mbali ili asaidiane na Balozi wetu wa China katika kufanikisha azma mbalimbali zikiwemo za kibiashara kwa maslahi ya wananchi wetu, wanaofanya biashara katika ukanda huo wa dunia. Lazima tukubali ukweli kwamba, Ubalozi ni kiungo muhimu kwa biashara kati ya nchi na nchi, hivyo

narudia tena kwa msisitizo mkubwa, tuweke waambata wa biashara katika Balozi zetu kama ilivyo waambata wa kijeshi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wawili nataka kuwatambulisha, mmoja katika *Speaker's Gallery* pale ni Mama Stella Masha, mke wa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, yule pale amesimama. Karibu sana, ingekuwa vizuri ungekuwepo wakati mume yuko kazini. Hata hivyo, karibu tu. *(Makofi)*

Pia kwa heshima naomba nimtambulishe Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Karatu, ambaye anaitwa Mheshimiwa Lazaro Titus Masai. Yule pale, anatoka Chama cha CHADEMA. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI HAMIS S. KAGASHEKI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi. Kabla ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Dr. Asha Rose-Migiro, kwa hotuba nzuri na hoja nzuri ambayo ameiwasilisha hapa Bungeni. *(Makofi)*

Napenda pia kuchukua nafasi hii, kwa kuwa si muda mrefu sana tangu amepotelewa na mama yake mzazi, napenda kumpa mkono wa pole. Napenda niwatambue Wasaidizi wake wawili, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na ninasema kwamba, hotuba yao aliyoisoma Mheshimiwa Waziri leo, ni hotuba nzuri ni hotuba ambayo inatupa ripoti ya mambo ambayo yanafanyika na ambayo wanatarajia kuyafanya.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ni fahari kubwa na ninayo machache ya kusema ya kuongezea hapa. La kwanza, linahusu uteuzi wa Mabalozi. Uteuzi wa Mabalozi hapana shaka ni wajibu na ni *domein* ya Mheshimiwa Rais, wala hatuwezi kuwaingilia, lakini kama Wabunge na kama watu wengine, tunaweza kutoa ushauri. Ushauri ambao mimi ninaweza nikautoa ni kwamba, Mabalozi ni kweli ni *pleasure* ya Rais kuchagua watu ambao anawaona wanafaa, watu ambao wanamwakilisha yeye na watu ambao wanaliwakilisha Taifa. Lakini pale Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, sisi ambao tulipata bahati ya kuwa pale miaka ya nyuma, kumekuwa na manung'uniko ya muda mrefu na nafikiri hata Waziri mwenyewe atakuwa anayajua na hasa ni kutokana na watu ambao wanachaguliwa. Naomba pawepo na *balance* pale, kuna watu ambao ni *foreign service* na *officers* ambao ni *carrier,* wamefanya kazi kwa muda mrefu sana ndani ya hii Wizara na yeyote ambaye ameanza mle, matumaini yake ni kwamba, siku moja atakuwa Balozi.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme hili kwamba, naomba Mheshimiwa Waziri, anielewe na alielewe kwa nia nzuri kabisa kwamba, wakati wanafanya uteuzi, waitazame hiyo kwamba, kunakuwa na *balance* kati ya wale ambao ni *political appointees,* ambao wanakuja kwa *contract* na wale ambao ni *carrier foreign officers,* katika taaluma hiyo ama katika Wizara hiyo. Hilo ni la kwanza.

La pili, ambalo naona Mheshimiwa Rais, anajaribu kulifanya kwa uharaka ni hili la uwakilishi katika ngazi ya Ubalozi kuhusu akina mama. Kwa sababu mimi nakumbuka nilipokuwa Wizarani, miaka ya nyuma ile, alipokuwepo Balozi mmoja tu, Marehemu Tatu Nuru, kama nakumbuka vizuri na nafikiri katika Awamu ya Pili alikuwepo Balozi mmoja tu Mheshimiwa Nzaru, sidhani kama kuna mwingine. Kwa hiyo, utakuta katika Balozi 30, Balozi moja tu unakuta ndiyo lipo hilo suala la *gender*. Kwa hiyo, nashukuru naona sasa kumefanyika kidogo jitihada, tangu Rais ameingia madarakani, tayari ameshachagua akina mama wawili, lakini katika hizi Balozi 30, ningeomba iwepo *balance.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *system* ya *posting*, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, *posting* ni suala ambalo ni *very sensitive* ndani ya Wizara. Maana yake yapo malalamiko na yeye anayajua na tunayajua sisi ambao tuko nje. Lakini ningeomba pawe na *balance,* maana yake tusitazame *stations* tu, lakini tutazame mahitaji ya *stations* hizo. Siyo kupelekana tu, lakini upeleke watu kufuatana na mahitaji ya *stations* hizo. Kwa mfano, mbali na maofisa ambao tunawahitaji, lakini katika hili, wale watu ambao wanasaidia *administration, accountants* au *administrative attachee,* unakuta kwamba, ziko Balozi na nafikiri tangu tumepata uhuru na moja ambayo naweza kuipigia mfano ni Ubalozi wa New York, pale *secretary* wa Balozi miaka yote amekuwa ni *locally recruited* pale. Sasa hii upande wa Serikali, inaipa *savings* kwa sababu unapompeleka mtu kutoka Tanzania, ukampeleka kule katika nafasi hizi ambazo wako Watanzania kule, ndiyo wanaozifanya hizi kazi. Kwa uzalendo na kwa moyo mzuri, lakini pia inatupunguzia sisi kama Taifa, kuwalipia mambo ya watoto, gharama za shule, kuwalipia mambo *health insurance.* Yako mambo mengi, ni *packag*e kubwa ambayo nadhani Mheshimiwa Waziri, atakuwa anaielewa hiyo na zipo Balozi wangeweza kutumia *approach* hiyo ya kuweza kuona kwamba, mahali ambapo kweli si lazima kuwa na *a local* kuwa na watu kutoka nje katika nafasi. *In fact* katika *station* nyingine, unakuta mtu ana-*combine administration, accounts na* kadhalika. Kwa kusaidiwa na *HHC* ama *Head of Chancellor*. Kwa hiyo, ningeomba hiyo muweze kuitazama.

Mheshimiwa Spika, la tatu, Waziri amezungumzia juu ya kufungua *new embassies.* Ni vizuri, Brazil ni nchi kubwa kiuchumi katika Latin America, lakini pia katika ulimwengu, nafikiri itakuwa hata inazidi nchi ya Italy, ambayo unaweza ukasema iko katika *G7*, lakini *economically* Brazil iko *more powerful and more strong.* Kwa hiyo, kusema kwamba, unafungua kule, sidhani kama kuna tatizo. Kufungua Malaysia, mimi nadhani ni sawa sawa. Nina swali, Tanzania ilipoamua kufungua *embassies,* upo Ubalozi wa Netherlands, ambao tuliufunga na mpaka sasa hivi umefungwa.

Lakini pale Netherlands, tunazo nyumba mbili, ipo nyumba ya Balozi na iko nyumba ya Ofisi. Sasa mimi nasema, kabla hatujakimbia, kwa sababu ile Netherlands ilipofungwa nakumbuka hata Rome ilifungwa wakati ule, lakini Rome ilifunguliwa, nafikiri na nyingine ilifunguliwa. Sasa naomba Waziri atueleze kwa nini kunakuwa na kigugumizi, kutofungua Ubalozi katika nchi ya *Netherlands?* Naisema kwa nia nzuri kwa sababu Tanzania ni *beneficiary* mkubwa kutoka katika msaada tunaopata katika nchi ya Netherlands, katika Afrika, Tanzania ni ya kwanza. *Recepient* wa kwanza kwa

misaada tunayopata kutoka nchi ya Netherlands, katika ulimwengu ni ya tatu, ni *recepient* wa dunia. Sasa kwa nini tunaipiga chenga? Kama zipo sababu, naomba Waziri atueleze kwa nini hatufungui tena Ubalozi wetu pale Netherlands na nafikiri Naibu Waziri ambaye ni Seif Idd, nafasi yake ya mwisho kabla hajaenda Beijjing, alikuwa pale Natherlands na anajua kabisa *property* zilizoko pale.

Mheshimiwa Spika, la nne, nataka kuzungumzia juu ya hawa viongozi wetu, ambao wame-*retire,* tumemsikia Waziri akizungumzia alivyochaguliwa huko nje, ana *Commission* ndani na ni heshima kubwa kwa Tanzania. Nimemsikia amemtaja Salim Ahmed Salim, mambo ya Sudan huko na kadhalika na kadhalika. Lakini hawa ni *retired officers,* viongozi wa juu, tunawalipa, kwa nini hatuwatumii hapa Tanzania? Kwa mfano, kama Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kweli ni Rais, lakini amekuwa *Foreign Minister* kwa muda mrefu. Mheshimiwa Salim Ahmed Salim, amekuwa *Foreign Minister,* lakini pia amekuwa Katibu Mkuu wa *AU* kwa miaka 12, nafikiri *the longest saving,* wapo watu kama Jaji Joseph Sinde Warioba, anafahamika kabisa kabisa, wanamwita huko nje.

Sasa mimi nasema hapa Tanzania *why,* hatuwezi kuwatumia watu hawa wakawa na *contribution* katika kutusaidia ku-*develop* kama ni *foreign policy,* kama ni *economic policy* hapa ndani ya nchi? Ina maana kusema hii *base* ambayo wanaipata na kazi ambayo wanaifanya huko nje, msingi wao mkubwa ni hapa Tanzania, sasa ulimwengu upate. Naomba kupitia kwako, Wizara ina-*coordinate* mambo mengi, hawa watu kwa kweli tunaweza kuwatumia.

Katika hii *Center* ya *Foreign Relations, for example,* katika *think tanks* ambazo inaweza ku-*establish* za kuweza ku-*develop* mambo mengi, hivi sasa tunapozungumza, *magnetic negotiations* ya dunia nzima, *the sticking point* ikiwa ni *agriculture,* siku ya Jumatatu zime-*collapse.* Sasa baada ya ku-*collapse* huko sisi Tanzania tunakwenda wapi ama tuna *position* gani? Haya hata sikuyasikia, labda ataizungumza Waziri wa Biashara na Viwanda, lakini pia nafikiri linagusa *Foreign,* kwa sababu haya ni mambo muhimu ambayo tunao viongozi wetu, wangeweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, haraka haraka huu ni mchango tu mimi nautoa, kwa hiyo napenda kuboresha tu na Wizara yetu iweze kuitazama kwa mfano, hii *Center for Foreign Relations,* ni chombo muhimu kwangu mimi ninavyoona.

Ni chombo ambacho kingeweza kusaidia ku-*formulate foreign policy* ya Tanzania, sisemi kwamba chenyewe ndiyo kinakuwa na madaraka. Madaraka ya mwisho yako mikononi mwa Waziri na Wizara yake, lakini *inputs* mbalimbali, ambazo wanapata katika *strategic thinking* na katika ku-*develop* zile njia za kuweza ku-*negotiate* katika *negotiations* na *forum* mbalimbali za dunia.

*Centre for Foreign Relations* kusema kweli ingekuwa na *role* kubwa sana. Mwalimu Nyerere aliandika kitabu mwaka 1964 na *title* ya kitabu hicho ni *urge don't shout* na kitabu hicho kinafundisha *how to negotiate,* kinaweka *principles of negotiations*. Nadhani hata *Foreign* wangezidi kukitumia leo na hata *Centre for Foreign Relations*

wangeweza kukitumia. Sasa hii *Centre* ya *Foreign Relations* nina ombi, kupitia kwako ningemwomba Waziri, wangeweza kutengeneza kitu ambacho kinaitwa *annual lecture on Julius Nyerere* katika ku-*develop foreign policy* na ku-*develop other issues*. Mwalimu anatambulika dunia nzima, Kanisa la Kikatoliki sasa hivi wanaanza utaratibu kusema ni mwema kiroho *and so on*. Huyu ni mtu ambaye ameijenga Tanzania. Tanzania *is economically poor, economically weak,* lakini imekuwa *on the international map,* kwa sababu ya Nyerere. Imejulikana dunia nzima, imekuwa *centre of political gravity,* watu wametoka *everywhere* wamekuja Tanzania kwa sababu ya Nyerere *on liberation issues,* ametoka kwenye *liberation* kaja katika *economic issues. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba *Foreign Relations*, kupitia katika chombo hiki, wange-*develop something on Julius Nyerere,* huyu ni mtu ambaye Henry Kisinja alisema kwamba, *he was worth for advisory,* huyu ni mtu ambaye *news work* ya Marekani imesema kwamba, *the Voice of Africa*, huyu ni mtu ambaye Jimmy Katta, *the formal President of the United States* alisema, *he is real a teacher, has the name reflex.* Huyu ni mtu ambaye taasisi zote, Serikali zote, viongozi wote, wamemtambua hivyo, sisi hapa Tanzania *nothing*, ukiniambia kwamba, Taasisi ya Mwalimu Julius Nyerere *they will do it*, nasema *they will not.* Hiyo taasisi nilisema tangu mwanzo kwamba, sikubaliani nayo kwa jinsi ilivyoanzishwa na sikuweza kuficha na ninazo fikra zangu, nadhani si mahala pake, hiki ni kitu ambacho naomba *Foreign Affairs* wakipe uzito, kuweza kuona Mwalimu ana-*fit* wapi na ana-*fit* vipi katika *contribution* ambayo ameifanya katika ku-*develop the policy* ya *economics* na *policy* ya *foreign* katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI**: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata nafasi na mimi nichangie mawili au matatu kuhusu hoja hii. Kwanza, nampongeza Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose M. Migiro, kwa hotuba yake nzuri, ambayo mimi naiunga mkono moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, tulipopata Uhuru mwaka 1961, Mwalimu alisema kwamba, Uhuru wetu hauna maana kama nchi nyingine bado zinakandamizwa, bado ziko chini ya ukoloni. Toka siku hiyo Watanzania hatukupumzika, tulifanya kazi kubwa sana kujaribu kuwakomboa wenzetu na ushahidi umeonekana jinsi kazi kubwa tuliyoifanya nchi zote hizi za Kusini mwa Afrika ambazo zilikuwa chini ya ukoloni. Sisi tulishiriki kwa hali na mali kuweza kuwakomboa wezentu na kwa kweli tulichoishia mpaka leo ni sifa. Sasa mimi napenda kuhoji kwa nini tuishie sifa tu, je, hii Kamati au huu Mradi wa Hashimu Mbitta, utatusaidia au tutaishia kuwa ni historia tu na sifa?

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo ni kwamba, hizi nchi ambazo zimekombolewa, zinaanza kutupita kiuchumi na nyingi zinatupita, pamoja na kwamba, walikuwa miaka mingi wanapigana, lakini sasa hivi ziko mbele kiuchumi. *We are still nursing our wounds* katika hili suala la kuwasaidia. Mimi naomba sana kujua inasema nini Wizara hii, kuwakumbusha wenzetu kwa nini watuache nyuma, kwa nini hawatuchangii sawasawa kiuchumi, kwa nini watuletee wawekezaji tu ambao wanakuja kupora zaidi tena mali zetu?

Mheshimiwa Spika, naomba tupate ufafanuzi vizuri ni nini *agenda* ya Wizara hii, itakuwa ni Mikataba kama ile ya Carl Peters na Chifu Mangungu wa Msovero kwamba, ni mikataba tu ya biashara basi ambayo ni *lop-sided*. Mimi ningeliomba nipate jawabu kidogo, niweze kupata maelezo vizuri, Afrika ya Kusini ni nchi tajiri sana, lakini tunanufaika vipi, wao wametukumbuka vipi, Angola, ukiacha hizi nyingi nyingine, je, wanatukumbuka vipi? Sasa nilitegemea kwamba, baada ya hapo wangesema jamani kuna migodi miwili au mitatu hapa labda na ninyi Watanzania mnufaike. Lakini kitu cha namna hiyo hatujawahi kukiona, badala yake ni kwamba, imekuwa ile ya kusema tenda wema nenda zako.

Mheshimiwa Spika, ningeliomba kabisa kwamba, wenzetu japo kuwa si ustaarabu, lakini wangejaribu kuona kwamba na sisi tunajaribu kuondokana na lindi hilo la umaskini. Tumehangaika miaka, toka 1961 mpaka mwaka 1990, tunashughulikia harakati za ukombozi, watu wetu wamepoteza maisha, lakini hadi sasa katika kutusaidia kwenye nyanja hizo za kiuchumi, sijaona kitu ambacho kimewahi kufanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeliomba pia Wizara ijaribu kutueleza vizuri, kwenye suala la ubaguzi japokuwa tunaelekea zaidi kwenye masuala ya uchumi, lakini Mwafrika bado yuko nyuma. Ubaguzi ungalipo dhidi ya Mwafrika, hii *Breton Woods Commission,* ambayo inasemekana kwamba, ndiyo ilibadili mwelekeo wa masuala ya misaada Afrika. Hii ni dalili mojawapo ya ubaguzi, kwa sababu mara baada ya vita baridi kwisha, wao waligeuza mwelekeo, wakaanza kufadhili zaidi nchi za Mashariki ya Ulaya. Sasa naona hapa kuna *element* ya ubaguzi wa rangi, kwa sababu sisi kwanini tuachwe, walibadili kabisa wakawa wanafadhili upande zaidi wa wenzao Wazungu, lakini sisi tukawa tumeachwa na mpaka leo bado tuna matatizo makubwa, japokuwa wamepora mali zetu, mali nyingi zimekwenda Ulaya lakini wametuacha.

Mheshimiwa Spika, ningeliomba pia ufafanuzi juu ya suala hili la ubaguzi tuweze kuelewa hatima ya Mwafrika hasa ni nini na kwa nini tunakuwa *second class citizens* katika hii dunia, mpaka leo sisi ni watu wa daraja la pili hatuthaminiwi? Ubaguzi mpaka sasa hivi bado upo hata kwenye nyanja za michezo, tumeona *World Cup* juzi juzi jinsi kulivyokuwa na ubaguzi wa rangi wa wazi wazi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri hii sera ya kusema kwamba, ni dipomasia ya uchumi halafu tukaacha mambo mengine ya msingi, Wizara hii ingejaribu kuingalia, tujaribu kuona kwamba, tunarekebisha mwelekeo wa dunia hii.

Mheshimiwa Spika, utumwa ungalipo, si kweli kwamba, utumwa umekwisha, tunasikia nchi kama Maulitania na sehemu nyingine utumwa ungalipo. Waafrika wanachukuliwa kama bidhaa kwenda kuuzwa sehemu nyingine. Mimi ningeliomba kwamba, tusisahau yale mazuri ambayo tulianza nayo, hasa katika kulinda utu wa mwafrika. Hakujawa na usawa hata kidogo na kama sisi wenyewe hatujajikomboa kiutu, Mwafrika hajakombolewa sawa sawa, hatuwezi tukasema kwamba, tunakwenda kujikomboa kiuchumi. Tutajikomboa vipi wakati utu wetu sisi wenyewe hauthaminiwi na mifano mizuri tu iko hapa nyumbani, jinsi mnavyoona hawa wawekezaji wanavyo nyanyasa watu wetu katika sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, nadhani msisitizo wa kwamba tumefanya *u-turn* ya kutoka ukombozi halisi, sasa tunasema tunajikomboa kupitia diplomasia ya uchumi. Nadhani kidogo hapo naomba msisitizo uangaliwe pia kwenye masuala hayo yaliyobaki, kuna ukoloni uliobaki, ukoloni mambo leo, ambao tunahitaji kabisa tuupige vita, lakini tumejikuta tumejitumbukiza katika masuala ya Kimataifa, tumekuwa sehemu ya Kimataifa, sasa mambo yetu tunafanya Kimataifa, lakini kwa kweli tulikuwa na msimamo mzuri kabisa. Tanzania ilikuwa ni nchi mojawapo, ambayo inapiga kelele mapema sana kama kunatokea tatizo, kama kunatokea unyanyasaji na kama kunatokea masuala ambayo yanamdhalilisha Mwafrika. Sasa hivi, tunaiachia hii Jumuiya ya Kimataifa, lakini watu wetu wanazidi kuumia.

Mheshimiwa Spika, ningelipenda pia kuzungumzia upande wa utamaduni wetu, sisi Tanzania hapa tunauza Kiswahili katika nyanja zetu za utamaduni. Kiswahili sasa hivi hapa asubuhi watu wamezungumza kwamba, tuone uwezekano wa kupeleka lugha yetu hata nchi za nje na iwe lugha ya Kimataifa. Nadhani kwa hapo hakuna mtu anayebisha kwamba, tumefanikiwa kwa njia moja au nyingine, kwenye suala hili.

Mheshimiwa Spika, ningelipenda kuuliza, hizi nchi zingine za Kiafrika zinauza nini, mbali ya bidhaa hizi za biashara, lakini kwenye suala la utamaduni, nchi za Kiafrika zinauza nini na sisi tunapokea nini kutoka kwao? Kwa sababu sasa hivi tunavyoona na tunavyokwenda, tunapokea tamadani ambazo kwa kweli ni za kusikitisha, tamaduni ambazo zinamfanya Mwafrika aonekane kuwa kweli ni mtu wa *dark continent*.

Mheshimiwa Spika, nikitoa mfano wa filamu hizi zinazotoka Nigeria, ambazo kwa kweli zinauza waziwazi, uchawi na ushirikina, sasa tunajifunza nini hapo, tunajifunza kupitia picha hizi kwamba, Mwafrika ni mtu ambaye hawezi kujiamini, mpaka kwanza aende ku-*consult* Kamati ya Ufundi au Sangoma au *occult* ndio atoe maamuzi. Sasa tunaelewekaje katika Jumuiya ya Kimataifa na ndio maana tunadharauliwa mpaka leo, kwa sababu hatuwezi kufanya mambo kisayansi na kiutaalamu, tukaaminiwa. Utakuta *potrayal* tunayoipata sisi ni kwamba, ni watu tusiojiamini, ni watu ambao hatuwezi kutoa kitu chochote cha maana mpaka kwanza, tumekwenda mambo ya giza.

Mheshimiwa Spika, sasa ningeliomba kwamba, huu utamaduni wetu ulikuwa ni mzuri na sisi tulikubaliana kabisa kwamba, Watanzania tuache lugha zetu, tukubaliane kukumbatia lugha moja na ambayo inatuunganisha na tumefanikiwa kwa hilo, *of course* sasa inabaki kwenye tamaduni nyingine kuonesha mila na desturi zetu, ngoma nzuri, zinazojenga utu wa Mwafrika. Lakini hizi nyingine hizi, ambazo kwa kweli zinatudhalilisha, ningeliomba tuangalie upande huo, tuweze kumwinua Mwafrika, aweze kuonekana kwamba anakubalika.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho ningelipenda nichangie cha mwisho ni kwamba, huu mradi mpya wa kuandika historia ya ukombozi, kwa kweli ningependa niupongeze, nadhani baada ya ukombozi kamili na baada ya Nelson Mandela kutoka gerezani mwaka 1990, hiyo sehemu yote ikawa huru. Ni kweli kama nilivyosema

mwanzo kwamba, historia yetu ilitaka kusahauliwa, historia ya Mtanzania katika suala la ukombozi ilitaka kusahauliwa, sasa kama Serikali imeona kuna umuhimu huo, ninaipongeza sana kwa hatua iliyochukua ya kuanzisha huu Mradi wa Hashim Mbitta. Iandikwe vizuri historia ili ibaki katika kumbukumbu, Mtanzania amefanya nini katika Bara la Afrika, kweli kabisa, iandikwe vizuri, ianishwe vizuri, ieleweke toka risasi ya kwanza imepigwa, ili iweze kueleweka, *role* ya Tanzania ilikuwa ni nini katika kumkomboa Mwafrika na *role* ya Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Lakini hata hivyo, ninazidi kusisitiza kwamba, Mradi huu nao ungekuwa na chochote pembeni, hizi nchi zijaribu kuona kama zinaweza zikatusaidia ili tuuwezeshe Mradi huu uwe wa kudumu na uweze kukumbukwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, nadhani wanavijiji wa Mahurunga kule Newala au labda Nachingwea au sehemu nyingine ambazo watu hawa walikuwepo, watu wa Angola, Swapo na sehemu zote. Nashangaa wenzetu hapa Wabunge wa maeneo hayo tunalalamika nao kila siku kwamba, hatuna huduma ya maji, tuna matatizo kemkem. Lakini kama watu hawa wangekuwa wametukumbuka kama nilivyosema mwanzo na wakakumbuka hata hayo maeneo tu walau kusema tu bwana tunachukua *Mtwara Corridor*, basi nadhani wangetusaidia vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, ninasisitiza kwamba, histora iandikwe upya na nadhani kuna sababu za msingi kwa nini ameteuliwa Hashimu Mbitta na ni kweli amekuwa kiongozi shupavu katika masuala ya ukombozi, alikuwa Katibu Mkuu wa masuala hayo na amekuwa mstari wa mbele katika nchi zote zile ambazo zimekombolewa. Kwa hiyo, nadhani pamoja na kuenzi suala hili, kuwe na kitu *tangible*, cha kuweza kutusaidia sisi Watanzania, ambao kwa miaka yote hiyo, tulisubiri tukaacha mambo mengi ya kutuendeleza tukasubiri ili na wenzetu waweze kuwa huru.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa kunisikiliza na ninaomba Wizara hii, badala ya kusisitiza masuala tu ya kiuchumi, ijaribu kuangalia tena upya sera yake ili tuweze kuondokana na unyonge huu wa Mwafrika, tuweze kujikomboa vizuri na tuweze kuonekana ni watu ambao, tunaweza tukathaminiwa katika Jumuiya ya Kimataifa na mbele ya watu. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nami nichangie katika Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kwanza, nawapongeza Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya na hasa katika kuendeleza sera hii ya diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nchi sasa hivi inafaidika sana na uwekezaji kutoka nchi mbalimbali, ila nafikiri kitu kimoja ambacho hatujakifanya vizuri ni kutathmini ni maeneo gani ambayo yamefanyika au wawekezaji kutoka sehemu gani wamekuwa wengi zaidi na kama kweli uwekezaji wao basi unatuletea faida katika nchi yetu. Kwa mfano, tuna wawekezaji kutoka nchi kama China hapa wapo wengi tu, lakini hatuna hakika kama kweli uwekezaji wao ni sawa sawa na ule uwekezaji mwingine wa nchi kama za Afrika

Kusini au Uingereza na kadhalika. Kwa hiyo, nafikiri Wizara inahitaji kushirikiana na Wizara nyingine, kufanya tathmini ya hawa wawekezaji, ili pale ambapo tuna *serious investors,* iwe tutilie nguvu zaidi kuliko hawa wawekezaji wengine, ambao wanakuja kubangaiza hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, nilikuwa napitia vitabu vya makadirio, katika Kitabu cha Maendeleo, sikuona Wizara hii ikiomba fedha za maendeleo na nafahamu kwamba, kuna majengo mengi wananunua, wanajenga, kwa mfano, India sasa hivi wanajenga jengo, sasa tulitegemea labda fedha zao zitatoka katika fungu la maendeleo. Nasema hivi, nafikiri huko nyuma tuliwahi kupendekeza katika Kamati kwamba, ni vizuri zikatengwa fedha katika fungu la maendeleo, badala pesa za maendeleo zikaingizwa kwenye *re-current account* na kwa sababu hiyo, ndio maana tunapata haya matatizo tunayoyapata kama Italia kwamba, hakuna fedha maalum zilizotajwa kwa ajili ya shughuli hiyo ya ununuzi, basi inapotokea dharura tu, fedha zinachukuliwa katika utaratibu ambao sio wa kawaida na ndio tukapata matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninashauri kuanzia sasa, kwa sababu tuna programu ya kujenga ofisi zetu katika nchi mbalimbali, tuna programu ya kununua majengo katika nchi mbalimbali, ni vizuri tukawa na programu ya kujua hasa katika mipango ya maendeleo ni wapi na wapi tunakwenda kununua na ni kiasi gani cha fedha kitatumika. Hivi sasa haimo katika kitabu hichi cha maendeleo, imechanganywa katika mfuko ule wa *re-current expenditure,* ambao ufuatiliaji wake unakuwa ni mgumu, kwa sababu maamuzi yanatokea kama vile zima moto. Kuna mfano hai, hivi sasa nafikiri mbali na kujenga ofisi pale India, kuna mpango wa kununua jengo, lakini halimo katika mipango hii hapa. Kwa hiyo, unaona ni vitu vinatokea vya dharura, kiasi ambacho uhakiki wake unakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, tatu, suala hili la Italia limekuwa likiulizwa ulizwa sana ninakumbuka mwaka 2005 wakati tuko kwenye *Public Accounts Committee, Controler and Auditor General* alilielezea tatizo hili kwamba, kwanza utaratibu mzima wa ununuzi wa jingo kwa mujibu wa *Procurement Act*, haukufuatwa. Lakini pili, hata ule uzabuni wake nao ulikuwa wa matata. Tatu, kuna malipo halali yaliyotolewa na kuna malipo yasiyo halali yaliyotolewa. Sasa nafikiri Serikali ingekuwa *very clear* kwa hili. Wakisema bado wanaendelea na uchuguzi mimi nafikiri hawasemi ukweli, kwa sababu *Controler and Auditor General* alipokuja, hoja zake zilikuwa *very clear* kwenye *Public Accounts Committee* na maelezo yakawa ya wazi kabisa na nafikiri yanajulikana makosa yametokea wapi na wapi.

Mimi nafikiri Serikali ingekuwa *clear,* akamaliza hili suala kwa sababu kila wakati linaulizwa na halipati majibu sahihi. Kama ni suala la mahakamani liende mahakamani, kama ni suala limemalizwa ki-*administrative* liweze kueleweka, lakini hadithi kamili ipo na *auditor general* anayo hadithi kamili na mkitaka *Hansard* ya *Public Accounts Committee* basi itapatikana, kulijua hasa tatizo hili liko wapi. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikawa *very clear* katika hili, badala ya kusema tunafanya uchunguzi, hii nafikiri si kauli sahihi sana. Iko taarifa rasmi, nafikiri Serikali ingeitoa Bungeni, hata kama hawana watoe ile ya *Controler and Auditor General,* ambayo aliitoa rasmi, kwa

hiyo, nafikiri ingetusaidia Wabunge tukafahamu hasa kilichotokea, badala ya masuala haya kuendelea kila siku.

Mheshimiwa Spika, lakini cha msingi ni kwamba, sisi tumepitisha sheria hapa ya *procurement*, nilitegemea taasisi zote zitaiheshimu hii sheria. Haifutwi, ndio tatizo linapotokea kwamba, ukiacha kuifuata ile sheria tuliyoipitisha hapa Bungeni, basi matatizo yanakuwa yanatokea kila siku na yataendelea kutokea na nafikiri kuna *areas* nyingi. Sasa kwa sababu sheria yenyewe ya manunuzi tuliyopitisha hapa Bungeni haifuatwi sawa sawa, nafikiri hili lingeweza kuzingatiwa na hasa kwa Balozi zetu za nje. Majengo kule ni ghali sana, pale India tunaambiwa jengo wanalojenga ni karibu dola milioni tatu, kuna jengo lingine linataka kununuliwa karibu milioni tatu vilevile, hatuna uhakika kama ndio *real value*. Kwa hiyo, kuna mambo mengi ambayo nafikiri yangefuatwa kwa utaratibu mzuri, yangeweza kusaidia kutupunguzia gharama. Balozi zetu zinatumia fedha nyingi sana kwenye usafiri, kwenye simu, ukienda simu ya mkononi, mtu mmoja anatumia dola 1,000 kwa mwezi, sasa nasema gharama hizi ni kubwa za matumizi wakati zinaweza zikapungwa kama kuna utaratibu unaofuatwa.

Mheshimiwa Spika, la tatu, wa mwanzo alizungumzia juu ya vigezo vya uteuzi wa watumishi wetu. Hata hawa watumishi tunaowaita *local staff*,, tunatumia *local staff* wa pale pale ndani ya nchi, wakati si sahihi, wakati wako Watanzania wangechukuliwa. Nimeshuhudia India wako *local staff* wa pale wanafanya mambo ya uhasibu, lakini *local staff* Wahindi, si Watanzania walioko pale na sisi tunategemea *local staff* kwa maana si yule aliyekuwa *positive* kutoka Tanzania rasmi, lakini yuko pale katika mazingira ya nchi ile na angeweza kufanya ile kazi vizuri. Sasa nafikiri kuna tatizo hapa kidogo na wanalipwa vizuri kuliko hata Watanzania wengine pale. Sasa hii nayo vile vile si nzuri. Kwa hiyo, nafikiri hili linataka liratibiwe vizuri sana na kutolewa maelekezo hasa *local staff* maana yake ni nini na mishahara yao na marupurupu yao. Kama basi hakuna mwongozo wa namna hiyo, ndio haya ya ajira za kienyeji enyeji zinazotokea, nalo hilo nafikiri lingeweza kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni hili la uteuzi wa maafisa wa ubalozi wenyewe, kwamba kama hatuweki vigezo hasa katika mazingira haya ya sasa, China inafanya biashara kubwa sana duniani. China ndio nchi ambayo inakua kiuchumi sana, basi angalau mtu unampeleka alingane na ile hali halisi iliyoko pale kwamba, anaweza akakufanyia *a critical analysis* ya kuona hali halisi ya kiuchumi inayoendelea pale na vipi mnaweza kujifunza. Nasema si kwamba aliyepelekwa hafai, lakini natoa mfano tu kwamba, uangalie mazingira ya ile nchi tunayompeleka mtu, tulizipuuza nchi za Kiarabu na nchi za Asia, lakini ukiangalia nchi zote za Magharibi, zimefaidika na nguvu za kiuchumi ziliko nchi za Uarabuni.

Sisi tulikuwa tunaogopa kwenda, tumeacha masoko ambayo yako karibu na sisi kwa muda mrefu, lakini hata sasa bado hatujayatumia vizuri, lakini nchi zote hizo za Marekani, biashara zao kubwa wanazifanya pale, kwa sababu ndio kwenye hela. Sasa wanasema sisi tunachanganya siasa na uchumi na hapa ndio tunapopata tatizo, baada ya kuangalia maslahi ya kiuchumi, basi tunaangalia siasa kwanza. Nitakupa mfano mmoja, tulifunga mpaka sisi na Rwanda na Burundi muda fulani, wenzetu wa Kenya wakatumia

nafasi ile, wakaenda wakafanya biashara kubwa, sisi wafanyabiashara wetu wakakwama mpakani na mizigo yao wakala hasara, kwa sababu ya siasa. Sasa nasema, tukichanganya siasa na biashara, nchi itaendelea kupata tabu sana, wenzetu wanaangalia biashara, wewe ukisikia Marekani nani wanakwambia kwanza hela, maneno mengine yatakuja baadaye, ni fedha, watu wanatafuta wanaendeleza uchumi wao.

Kwa hiyo, nafikiri imeshafika wakati sasa tutenganishe siasa na biashara, tufanye biashara, *otherwise* tutapata matatizo sana kuondoa umaskini nchi hii. Sifa moja ya kufanya biashara nchi za Kiarabu ni kwamba, wenzetu wana pesa *cash*, hawana ubangaizo, ukiuza ng'ombe utapata pesa yako utaondoka, ukiuza mbuzi utapata pesa yako utaondoka, je, tunalitumiaje soko lile vizuri, lakini tunachanganya siasa hatufanyi biashara?

Mheshimiwa Spika, Mwalimu aliwahi kwenda Oman, nafikiri mwaka 1984, alipofika pale akafanya ziara nzuri tu, akaondoka pale akapewa zawadi na nini, akapewa msaada wa dola milioni tatu *cash* akaondoka, ndio kile Chuo cha Afya unachokiona Zanzibar. Akasema Mwalimu hawa watu nimewaacha siku nyingi tu kumbe mambo yao ni mazuri, wakati milioni tatu, nchi nyingine akienda kutembelea mara kumi au mara kumi na tano hapati. Sasa nasema lakini kwa sababu ya siasa tu, tumeacha kujenga mahusiano na nchi ambazo tunaweza kufanya biashara vizuri. Nafikiri hii kasumba hii kidogo naomba tuiache, tuangalie biashara, sasa hivi ni wakati wa biashara. Siasa za China, zama ya siasa ya China ya komonisti iko wapi, anafanya biashara, anazungumza na wa Marekani, anafanya biashara, mimi nafikiri hilo ndio kitu cha kuweka msingi hivi katika *mind* zetu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la matumizi ya ofisi zetu za Kibalozi, nilisema kidogo lakini nafikiri nilikazie kwamba, hatujakuwa na utaratibu mzuri wa matumizi ya Kibalozi. Mara nyingi tunaolalamika kwamba, Balozi zetu hazipati pesa za kutosha na kadhalika, lakini ukienda *deep*, ukafanya *analysis* na ndio Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa alivyosema hapa kwamba, tukikitumia chuo vizuri kikaenda kufanya *critical analysis* ya matumizi, utaona kwamba, sisi tunatumia kuliko wanavyotumia wenzetu. Nenda ukafananishe na Ubalozi wa Kenya na Uganda, utazame Watanzania tunavyotumia, vitu viwili tofauti. Nafikiri kuna haja ya kufanya *critical analysis* juu ya matumizi yetu, kweli baadhi ya Balozi nyingine zina matatizo, zinahitaji fedha zaidi, lakini bado udhibiti wa matumizi sio mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri hili niliseme na ushahidi upo, hata mwaka 2005 kulikuwa na shilingi bilioni nne zilitumika mbali na bajeti yao ile ambayo walikuwa wamepata, matokeo yake baadaye tukakaa tukaona utaratibu wa kuweza ku-*reconcile*. Lakini nasema ni kwa sababu zile pesa wanazozipata za *visa* na kadhalika, wanaona kwanza watumie lakini hazimo katika mpango ambao umepangwa na Serikali.

Sasa nafikiri hilo ni tatizo na ndio maana kuna *circular* ya Hazina ilitoka nimeiona, juzi nilipojibiwa swali hapa niliambiwa kwamba haipo, lakini ipo Hazina iliyoelekeza matumizi ya fedha zinazopatikana kutokana na *visa* na kadhalika. Haifuatwi ile *circular* hivi sasa, nafikiri hili nalo lingeweza kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka kujua vilevile kuna hawa *Honorary Ambassadors* tulionao tulitaka kujua ni wangapi wapo, wanachaguliwa kwa misingi gain? Kuna nchi nyingine nyingi tu wameomba watu waweze kutusaidia, hawana gharama kubwa hawa, gharama yao kubwa ni ile heshima tunayowapa ya Bendera yetu na kadhalika.

Lakini kwa kweli wanaweza kusaidia sana ku-*promote economy of our country*. Nimekuta Vancouver pale wale Wahindi waliondolewa Uganda ndio Mabalozi, *Honorary Ambassodor* wa Uganda, wame-*promote business* kubwa sana Uganda.

Tunaweza na sisi kuwatumia watu wetu walioko nje ya Tanzania, hata wenyeji wa nchi zile ambazo wana hamu ya kui-*promote* Tanzania, tuzitumie hizo, ni *less cost* na zinaweza ku-*promote business* na *foreign relationship* na nchi yetu.

Kwa hiyo, zile nchi ambazo tunaweza kufanya nazo biashara, hatuna uwezo wa kufungua Ubalozi, nafikiri tuharakishe, tatizo vilevile ni maamuzi, wako watu wameomba muda mrefu tu hawajibiwi. Nafikiri tungelifuatilia hili lingeweza kutusaidia ku-*promote our business* na tukapunguza gharama za kuendeshea ofisi zetu za Ubalozi.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kwamba, napenda tena Wizara ijitahidi sana kuleta ule uwiano wa watumishi baina ya pande zetu za Muungano. Nakushukuru sana. Ahsante sana.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze sana kwa kazi nzuri unayoifanya kama Spika wetu humu ndani na mimi nakushukuru kwa nafasi ambayo umenipatia lakini pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro, kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Waziri wa Wizara hii lakini pili kwa kusoma hotuba nzuri ambayo ina mwelekeo wa Kimataifa kama wewe mwenyewe ulivyosema, nampongeza sana. *(Makofi)*

Lakini nawapongeza sana Naibu Mawaziri wanaomsaidia pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ambaye kwa bahati nzuri sana nimewahi kufanya naye kazi na hata nje huko nimewahi kwenda naye kwenye mikutano ya *DOHA*, kule *WTO*, Cancun, Brazil na sehemu nyingine. Nampongeza sana naye kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwanza kwamba sikuwa nimejiandaa kuchangia hoja nyeti za Wizara hii lakini nilipoambiwa kuna nafasi nikasema ni vizuri labda niseme machache ambayo ninayo ambayo yanaihusu Wizara hii.

Moja, Waziri alipokuwa anachangia yako maswali mbalimbali ambayo yanatuhusisha sisi na nchi za jirani hasa zile za Burundi, Rwanda na Kongo masuala ambayo yanahusiana na wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, miaka michache iliyopita Tanzania hususan Wilaya ya Kasulu kumekuwa na watu wengi ambao waliuawa na askari wa Burundi, swali hilo lililetwa hapa Bungeni tukaambiwa Burundi hakuna Serikali, itakapokuwa Serikali imepatikana basi tutazungumza na wenzetu wa Burundi tuone kama kunaweza kukatengenezwa mkakati wa fidia.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia kesi maalum ya kijiji cha Nyakimwe ambapo Watanzania kadhaa waliuawa pale mpakani kijiji cha Nyakimwe na kijiji cha Mkigo waliuawa na askari wa Burundi. Watoto wa wazazi hawa wamebaki ni yatima sasa ni watu wa kuombaomba na tuliomba angalau hata Serikali labda ingefanya mpango wasomeshwe lakini hakuna mpango ambao ulikuwa umefikiwa kwa wakati ule lakini tukasema basi tudai fidia kutoka Burundi ili tuweze kupata nafasi ya kuwasomesha watoto hawa. Sasa nilikuwa namuuliza Waziri kama sasa ni wakati muafaka ambapo tunaweza tukadai fidia hii hivi sasa au bado Serikali ya Burundi haijakaa sawa? *(Makofi)*

La pili ninalotaka kulizungumzia ni lile linalohusu Balozi zetu, kwa kweli Mabalozi wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini wengi wanajitahidi kufanya kazi nzuri sana na mimi nawapongeza sana. Hata wakati mwingine tunapowalaumu kwamba hawahudhurii mikutano kwa kweli siyo tatizo lao pengine ni tatizo letu, nimewasikia wasemaji wetu wanasema Wizara hii haikupewa pesa za kutosha na mimi nakubali kabisa kwamba Wizara hii inatakiwa ipewe pesa za kutosha ili na sisi tushiriki vizuri na kikamilifu katika masuala mengi ya Kimataifa hasa kuhudhuria mikutano inayohusu masuala mengi ya kiuchumi. Watu wengi wamekuwa hawahudhurii na ukiwauliza ni kwa nini hawakuhudhuria wengi wanasema ufinyu wa bajeti, hawana fedha za kuweza kuhudhuria mikutano hii. *(Makofi)*

Mimi nina uzoefu na Ubalozi wetu wa Brussels. Pale Brussels tuna Balozi mmoja mzuri sana anafahamu sana masuala haya ya uchumi lakini amekuwa hahudhurii mikutano ambayo pengine angeweza kutupa ushauri mzuri hata katika mikutano yetu tunayofanya ya *SADC* inayozungumzia masuala yote haya yanayohusiana *negotiations* za *Economic Partnership Agreements* za *EU* na *ACP countries.* Lakini pia baadhi ya mikutano sisi tumekuwa hatuhudhurii hakuna maelezo sahihi yanayotolewa kwa nini hatuhudhurii mikutano hiyo, matokeo yake hatuna taarifa nyingi ambazo zinatokea na mabadiliko mengi yanayotokea.

Hivi sasa Tanzania ina-*negotiate* chini ya Mkataba wa *Economic Partnership Agreements* na nchi za Jumuiya ya *SADC* lakini katika nchi zote kumi na nne za *SADC* ni nchi saba tu zimebaki zina-*negotiate* pale. Lakini nchi kadhaa kama nne zote ni nchi ambazo ziko chini ya Mkataba wa Afrika Kusini unaoitwa *South African Customs Union* ambao zile nchi hivi sasa zimeona kwamba watafaidika zaidi kwa kuendelea kuungana na Afrika Kusini. Afrika ya Kusini ina mkataba tofauti na nchi nyingine, ina mkataba wa kwake. Wao katika *SADC* ni waangaliaji tu yaani siyo wajumbe hasa wa *SADC* kwa sababu hata wakija wao hawatasaini ule mkataba wa *SADC*, wao wanao mkataba wao unaoitwa *Trade Development Cooperation Agreement (TDCA)* ndiyo mkataba walio nao.

Mheshimiwa Spika, ule mkataba wao wameu-*design* kwa namna yao wenyewe, kwa *level* yao ya maendeleo waliyofikia, sisi ni wajumbe wa *SADC* tunazo zile nchi nne

na nchi tatu za Angola, Mozambique na Tanzania. Baada ya muda sasa wamefikia mahali wanasema sisi lazima tubaki *SACU* na kinachoendelea hivi sasa ni kwamba zile nchi sasa zinaangalia ni vifungu gani kati ya ule mkataba wa *TDCA* ambao unawafaa na ambao wanaweza wakaubadilisha kidogo ili waende ku-*negotiate* na *South Africa.* Sisi tunaendelea kusema tuna-*negotiate* na *SADC EPA* yaani *SADC Economic Partnership Agreement*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuko mbali na Afrika Kusini, vitu kama vitaingia huko na tukawa na *Customs Union* ya *SADC* sisi hatutakuwa *beneficiaries* wazuri katika mkataba huo. Lakini hata hivyo makubaliano yaliyopo ni kwamba nchi itakayosaini *Economic Partnership Agreement (EPA)* ni lazima iwe ni nchi ambayo haina *Customs Union* nyingine, sisi tayari tuna *Customs Union* nyingine ya Afrika Mashariki, sasa hii inatuzuia sisi tusifanye biashara na *Customs Unions* mbili kwa sababu huwezi ukafanya biashara katika hizo *Customs Union* mbili ambazo kwa kweli utakuwa si utaratibu wa kiuchumi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni sisi kuamua kwa mstari ule ule kwamba je, tutafaidika nini? Tukiendelea na utaratibu huu wa *SADC* yapo mambo mawili yatakayofanyika.

Moja, ni kwamba kama bidhaa zitakuja chini ya Mfumo wa *Free Trade* zitaingia Afrika Kusini, Afrika Kusini lazima zije Tanzania *through the back door* siyo kwa utaratibu huo kwa hiyo haiwezekani sisi tuwe na mkataba ambao ni sahihi chini ya *SADC EPA*. Kwa hiyo, tuna-*negotiate* chini ya *a wrong configuration* ambayo kwa kweli sisi hatusimami au kwa lugha ya kigeni *we do not stand to benefit from the negotiations*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, njia ambayo tunaweza kufaidika moja tu tunaweza tukafaidika na mazungumzo sahihi kwa kurudi *COMESA,* kurudi *COMESA* kutatusaidia sisi kuungana na wenzetu kwanza wa *East Africa* ambao tuna mkataba nao wa *Customs Union* na ambao huu utaheshimika chini ya *ESA. ESA* ni *Eastern and Southern African, EPA* ni *Economic Partnership Agreement, negotiations* ndiyo utaratibu tu utakaotufaa. Wenzetu wale ambao watakuwa wametuhama kwa mfano, sasa hivi Angola inafikiria kwenda *CEMAC*, *CEMAC* ni *Central African Configuration* ya *CEAM EPA* ile ya *Central Africa*. Mozambique ni rahisi kuna vitega uchumi vingi ambavyo vimetoka *South Africa* vimeingizwa Mozambique hata wenyewe *South Africa* wakizungumza wanasema pengine sisi tunaweza ku-*accommodate* hawa Mozambique lakini Tanzania si rahisi maana ziko *complications* nyingi ambazo zinahusu mambo nyeti ya kiutaalam ambayo yanahusiana na *sensitive goods* ambazo zinatakiwa ziingie katika utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba tulifikirie jambo hili pengine wakati unakwisha maana tuna miaka miwili tu ambayo imebaki na pengine siyo miwili *negotiation* ni mwaka mmoja huu wa 2006 umekwisha tuna 2007 ndiyo muda ambao tumebaki nao, tulifikirie sana na twende haraka na maamuzi yetu yaende haraka lakini pia tushiriki katika mikutano ya Kimataifa hasa hii inayohusu *negotiations* za kiuchumi kama kweli diplomasia ya kiuchimi itafanya kazi kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo nataka kulizungumzia ni lile linalohusu misaada isiyotolewa *(unfulfilled promises)* au misaada ambayo inaahidiwa na Mashirika ya Kimataifa lakini sisi tunapanga katika taratibu zetu. *Greanagoles* walipokaa walitoa ahadi, *G8* walipokaa walitoa ahadi, nchi tajiri walipokaa walitoa ahadi na makundi mengi yametoa ahadi nyingi lakini baadaye zinakuwa ni *unfulfilled promises*, hivi liko tatizo gani Mheshimiwa Waziri hakulizungimzia kwamba fedha tunaendelea kupata zipo tunapopata lakini Mheshimiwa Waziri naona kwenye hotuba yake hakuzungumzia kwamba liko tatizo hili na sisi tunaendelea kupanga, lakini fedha zisipotoka tunalaumiana hapa kwamba tukipata itakuwa hivi lakini fedha hazikutoka. Mimi nafikiri angetolea maelezo kidogo ili tuweze kuelewa kinachoendelea katika nyanja za Kimataifa.

La mwisho ni huu Mfuko wa Mwalimu Nyerere. Mheshimiwa Balozi Hamis Suedi Kagasheki, amezungumza vizuri sana kuhusu mfuko huu. Huu mfuko hauna fedha na wala hauwezi kufanya yale ambayo tunataka yafanye, yalete heshima ya Mwalimu Julius Nyerere, je, kwa heshima ya Mwalimu hivi tukileta hapa kitu Serikali haiwezi ikakubali ku-*fund* huu mfuko angalau mfuko na jina la Mwalimu tunayemheshimu, tunayemuenzi, tunayempenda liendelee kupata heshima wale wanaofanya kazi ile ya heshima kubwa wanaonekana wananyanyasika tu wanatembeatembea wanaomba.

Mheshimiwa Spika, huu Mfuko tuuenzi kwa namna yake, tuutafutie fedha kwa namna yake, Serikali ichukue jukumu la kusaidia mfuko huu kwa namna ya pekee na pengine siyo vizuri kuanza kutembea nje kwa mfuko wa mtu mwenye heshima namna hii eti tunaomba hela za kusaidia Mfuko wa Mwalimu Nyerere nchi za nje, ni sisi wenyewe hapa lazima wajibu huu tuuchukue sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nilifikiri niyaseme machache hayo, naunga mkono hoja mia kwa mia na ninampongeza tena Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wenzake pamoja na Wizara nzima ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIIKA:** Waheshimiwa Wabunge nilidhani tungeishia hapo lakini kwa kuwa bado tuna muda na nimepokea ombi ambalo halijachelewa basi namwita Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie kidogo hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa kuwapongeza wote wanaohusika na Wizara hii kuanzia mwenyewe Waziri, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro, naona ameanza vizuri, ameanza kupata uzoefu, naomba aendelee hivyo. Pia ningependa niwapongeze Naibu Mawaziri wote wawili kwa jinsi walivyoonesha uhodari wao wa kumsaidia Mhesimiwa Waziri. Ninamfahamu sana Balozi Seif Ali Iddi, tulikuwa wote Beijing pale kwa miaka mitano ni mchapakazi, mzalendo pia. Kwa hiyo, niliposikia kwamba ameteuliwa kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii sikuona ajabu kwa sababu ana uzoefu mkubwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, ambaye bado

sijamfahamu vizuri lakini nimemwona pia na yeye ameanza kuonekana kwamba anaiweza Wizara hii, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Pia napenda kuwapongeza kwa hotuba hii, ni nzuri inaleta matumaini makubwa katika kipindi hiki ambacho dunia inafanya mageuzi makubwa ya uchumi na kwa kuwa hii ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa itafanya kazi nzuri ya kuisaidia nchi yetu katika kukuza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ningependa kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Chuo cha Diplomasia. Mimi nimesoma pale ni chuo kizuri kwa maana ya utaratibu wenyewe kwa maana ya masomo, walimu, vitabu na hata mazingira ya pale. Lakini ningependa tu pengine Mheshimiwa Waziri anisaidie kwa sababu tulipokuwa tunasoma pale baada ya kumaliza masomo yetu kuna wenzetu ambao walitaka kuendelea zaidi pale walikuwa wanachukua *Diploma* walikuwa wanataka kuchukua *Advance Diploma* na *Post Graduate* wakasema kwamba bado hatujawa na utaratibu huo. Sasa pengine Mheshimiwa Waziri angenisaidia akanieleza kama kuna mabadiliko yoyote ili wanaomaliza pale katika ngazi hii ya *Diploma* basi wanaweza wakaendelea zaidi pale pale ama hata vinginevyo kwa sababu ni chuo kizuri, kina heshima kubwa, kimetoa mchango mkubwa katika ukombozi Barani Afrika na lingine katika chuo hiki ni kwamba naomba ukitangaze chuo kifahamike, mimi nina hakika si wengi wanaokifahamu chuo na hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hawajui kama pana chuo pale cha Diplomasia ambacho kinatoa elimu nzuri tu, basi ni vema ukawekwa utaratibu wa kukitangaza ili Watanzania wengi wakijue kwa sababu ni sehemu ya historia ya nchi yetu hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichangie pia upande wa historia ya nchi yetu na mimi nataka kuungana na wale wote ambao wamezungumzia kwamba historia ya nchi hii iandikwe vizuri na iandikwe vizuri kwa sababu nchi hii tumetoa mchango mkubwa katika ukombozi Barani Afrika. Mimi nina wasiwasi kwamba kama historia hii haikuandikwa, watoto wetu wanaokuja, wajukuu zetu hawataweza kufahamu kabisa kwamba Tanzania tumetoa mchango mkubwa katika Bara hili la Afrika. *(Makofi)*

Nataka nikupe mfano, nyuma kidogo mimi kama nilivyosema nimesoma Moscow siku za nyuma zilizopita, siku moja Watanzania tulialikwa kwenye sherehe za *ANC* pale Moscow na wote mnajua kipindi kile cha *cold war*, Warusi walikuwa wanaonekana wanatoa mchango mkubwa sana katika ukombozi katika *Third World Countries* lakini tulipofika pale kwanza tulipewa heshima kubwa na *ANC*, tuliwekwa mahali ambapo nchi zote kutoka Afrika hazikuwekwa wakashangaa. Si hilo tu hata katika hotuba iliyotolewa pale na viongozi wa *ANC* kuanzia mwanzo mpaka mwisho walikuwa wanazungumzia mchango wa Tanzania katika *liberation* katika Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, palikuwa na Warusi pale ambao katika hali ya kawaida wao ndiyo wangepongezwa zaidi, lakini *ANC* haikufanya hivyo iliipongeza Tanzania hotuba nzima na si ajabu mara tu Mheshimiwa Nelson Mandela alipotoka jela kituo chake cha

kwanza kilikuwa Tanzania. Lakini si hilo tu kwa nini tuandike historia hii upya tunaambiwa na ukweli ndiyo huo risasi ya kwanza kulia katika Zimbabwe ilitolewa na Mtanzania, ndiyo! Najua wengi hamjui hapa si hilo tu wote waliokuwa wanakimbia madhara ya kutawaliwa huko kwao na kunyanyaswa walikuwa wanapita Tanzania, Nelson Mandela alipita hapa alipokwenda Algeria akakutana na Mwalimu Julius Nyerere, akamwambia nakwenda Algeria, akamwambia ukirudi huko pitia Tanzania nina mazungumzo zaidi na wewe. Alipopita hapa akamwambia Mandela usiende *South Africa*, watakukamata na watakufunga baki Tanzania anza mapambano kutoka Tanzania, Mandela akamwambia Mwalimu Nyerere nakuelewa lakini acha niende utanisadia hata kama nitakuwa ndani, someni vitabu. Mandela akaondoka, anafika Afrika Kusini yote mnayajua yaliyompata akamkumbuka Mwalimu Nyerere, alipotoka jela mkono wa kwanza ni kwa Mwalimu Julius Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuyajui hayo, Watanzania tuliokuwa wengi tuyaandike ili watoto wetu na vizazi vyetu wayajue haya, ni nchi maskini, uchumi duni, tulikuwa hatuwezi hata kutengeneza nusu nguo acha baiskeli na gari. Mwalimu Julius Nyerere alisimama kidete sijui wangapi hapa kama tumetembelea maeneo ambayo tulikuwa tunawalinda, tunawatunza na kuwafundisha wapiganaji wa nchi za Kusini mwa Afrika, pale Mpwapwa, Kongwa, Iringa na kwingineko wengi hatujui hapa.

Mheshimiwa Spika, pengine nitoe ombi tu kwamba siku moja tutembelee maeneo haya, Waheshimiwa Wabunge twende tukayaone tuandike historia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina shamba kule Nachingwea, *Farm 17* pale pana handaki lilikokuwa likitumiwa na *FRELIMO* anashuka Marehemu Samora Machel, katika uwanja mdogo anapita chini kwa chini anakuja kuibuka, anazungumza na watu wake anazama tena chini anakwenda anaruka, anakwenda kupigana Mozambique, hatuyajui haya. Tunayaacha yapite kama maji katika mto unaokwenda kwa kasi, tuyaandike. *(Makofi)*

Mimi nafurahi sana kusikia kwamba Hashim Mbita amepewa hii kazi basi tumsaidie, tunaomba Serikali suala hili ilitolee macho kweli kweli ili nchi yetu iendelee kuwa na heshima. Wanahistoria wanasema usipojua historia huwezi kuwa na nguvu hata kidogo, tusiwaachie udhaifu watoto wetu wanaokuja waijue nchi yao. Naomba Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ifanye kazi hii kwa moyo wote tutawakumbukeni daima.

Mheshimiwa Spika, hapa nataka kuunganisha na Mfuko wa Mwalimu Nyerere, nataka nikubaliane na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, ni aibu. Mfuko wa Mwalimu Nyerere unatapatapa kutafuta pesa za kuuendesha pamoja na haya yote niliyoyazungumza, naomba tuuheshimu mfuko huu tuuwekee utaratibu hata kama kwa kukubaliana ndani ya Bunge hili kila mwaka kutenga pesa kwa ajili ya mfuko huu tunaweza kufanya hivyo. Tumjengee heshima Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere amefanya kazi kubwa na mimi nataka kusema siyo Bara la Afrika peke yake bali ni ulimwengu mzima huu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kengele imeshalia napenda nizungumzie uhusiano na nchi za Asia ya Mashariki. Mwaka 1995 katika Mkutano wa akinamama pale Beijing, China, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, anakumbuka Mwalimu Nyerere alisema hivi: "Ninyi Watanzania kama mnataka kuendelea zaidi basi watu ambao wanaweza wakawachukueni ni hawa wenzetu Wachina na nchi nyingine za Asia ya Mashariki, hawa Wazungu wamefika mahali matatizo yetu hawayaoni maana wao wako mbali kabisa."

Mheshimiwa Spika, Wachina sasa hivi ni watu bilioni 1.3, hata kama tunakwenda tukawauzia kitu chochote kile ni soko kubwa sana, ule mradi wa Macdonald sijui kama wengi mnaufahamu hapa *Fast Food* wiki moja Ulaya siku moja China mapato yake siku moja tu ni sawasawa na wiki moja ya Ulaya Magharibi.

Mheshimiwa Spika, leo sisi hapa tunapiga kelele korosho, korosho. Hivi wenzetu Wachina hawa hawazipendi hizi korosho? Wathailand hawapendi korosho? Singapore hawapendi korosho? Hivi ni nini hiki? Hakuna wanaopenda *nuts* kama Waasia, wanapenda sana.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje na Mambo ya Ushirikiano wa Kimataifa kama ni kufungua Balozi mpya basi tufungue katika nchi za Singapore, Thailand na nchi nyingine za Asia Mashariki ili tuitangaze nchi yetu, tupate soko na sisi tuvuke katika janga hili la uchumi tegemezi.

Mheshimiwa Spika, ubaguzi wa rangi katika michezo kwa kweli ni jambo la kusikitisha. Katika kikombe hiki cha dunia kilichomalizika juzi kulikuwa na mambo ya dhahiri kabisa kwamba kwa sababu timu hii kutoka Bara la Afrika haikutendewa haki hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, sisi Tanzania tumeshakuwa waanzilishi wa mambo mengi katika kumtetea mtu mnyonge sasa naomba Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, hili walivalie njuga pia ama sivyo tusishiriki katika Kombe la Dunia, tuwaachie wenyewe, ndiyo! Wanatudhalilisha lakini sisi ni binadamu kama wao tofauti yetu ni rangi tu, tuna akili pengine zaidi kuliko wao, lakini tunapokwenda katika michezo ya Kimataifa wanatunyanyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, suala hili walitafutie ufumbuzi, washirikiane na nchi nyingine za Afrika ili wenzetu wazungu wajue kwamba sisi hatutaki tena kunyanyaswa kwa sababu ya rangi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuunga mkono hoja ya hotuba hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kuhusu hoja yako kwamba historia ya ukombozi iweze kuandikwa nimevutika na mchango wako na nikashangaa unatuomba sisi tusiojua ndiyo tuandike wewe mwenyewe huandiki? *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa natoa wito kwamba unaonekana kuwa ni hazina kubwa ya masuala haya kwa hiyo, nakusihi Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, uisaidie Serikali katika kuyaandika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika hatua hiyo ndiyo tumefikia mwisho wa wachangiaji kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, sasa nadhani itakuwa vema au itakuwa ni kuwatendea haki Wizara ikiwa wachangiaji kutoka upande wa Serikali wataanza mnamo saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

Licha ya kuzingatia tu kwamba leo ni siku ya ibada kwa baadhi wenzetu na si vizuri kuisongasonga sana siku kama hii, kwa maana hiyo basi nitasitisha shughuli ili saa 11.00 jioni Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. Cyril August Chami, aanze kwa dakika 15, saa 11:15 jioni, Naibu Waziri Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, aweze kuzungumza saa 11:15 jioni hadi 11:30 jioni halafu saa 11:30 nitamwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje naUshirikiano wa Kimataifa hadi saa 12:30 jioni na ndiyo tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi. *(Makofi)*

Baada ya tangazo hilo sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11:00 jioni.

*(Saa 6:29 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. DR. CYRIL A. CHAMI):** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Naanza kusema kuwa naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kabla sijachangia hoja hii kwa kujibu maswali kadhaa ya Waheshimiwa Wabunge, napenda kuungana na Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote waliozungumza katika Bunge lako Tukufu kabla yangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi wake wa kishindo katika uchaguzi zilizompa Urais na Uenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuendelea kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa kuendelea kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mbunge, kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe mwenyewe kwa ushindi wako wa kishindo uliokuwezesha kuwa Mbunge na baadaye kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge na kuwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais katika nyadhifa zao na Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili Tukufu kwa kuaminiwa ama na wananchi au Mheshimiwa Rais hadi kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani zangu za pekee kwa wananchi wote na hususan wapiga kura wa Jimbo la Moshi Vijijini kwa imani kubwa waliyonionyesha na kunichagua kuwa Mbunge wao baada ya kuongozwa na Vyama vya Upinzani kwa miaka kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwaahidi kupitia Bunge lako Tukufu kuwa kwa kuwa imani huzaa imani, nitafanya kazi waliyonituma bila upendeleo au ubaguzi wa kiitikadi, kidini, jinsia au kiumri. Nawaahidi kushirikiana nao kuliendeleza Jimbo la Moshi Vijijini kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu naomba na mimi kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri. Napenda kumuahidi Mheshimiwa Rais kuwa nitatimiza kazi alizonipa na atakazoendelea kunipa kwa moyo thabiti pamoja na kuwa mtiifu na mwaminifu kwake na kwa wasaidizi wake wote ninaowajibika kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kumshukuru Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa malezi na maelekezo yake mbalimbali yanayoniimarisha na kuniwezesha kuzimudu kazi zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee nazitoa kwa Waziri wangu Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa uongozi wake mahiri na utayari wake wa kunilea, kunitia moyo na kunisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Nampongeza pia kwa kuteuliwa na Kamati Kuu ya CCM kuongoza Idara nyeti ya Siasa na Mambo ya Nje. Napenda kumhakikishia kuwa uteuzi wake huu sio tu umeonyesha jinsi anavyoaminika ndani ya Chama kama anavyoaminika ndani ya Serikali, bali pia umepokelewa nasi watumishi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa furaha kubwa sana kama kielelezo kuwa tunaongozwa na mwanamama mahiri na mwenye upeo wa juu kabisa wa uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Naibu Waziri mwenzangu, Katibu Mkuu Balozi Mutalemwa, Naibu Katibu Mkuu Balozi Mombo, Mabalozi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie pongezi zangu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa CCM pamoja na Naibu Katibu Mkuu Bara, Mheshimiwa Jaka Mwambi na Naibu Katibu Mkuu Visiwani Mheshimiwa Salehe Ramadhani Feruzi. Nawapongeza pia Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Katibu wa Mipango na Mheshimiwa Rostam Azizi, Katibu wa Uchumi na Mweka Hazina wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, napenda sasa niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii ama kwa kuongea au kwa michango ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mtoa hoja ana muda mwingi zaidi. Naomba nijielekeze kwa wasemaji wanne, najaribu kujibu hoja zao kama ifuatavyo:-

Hoja ya kwanza, imetolewa na Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum na ambaye alikuwa ametoa hoja kwamba ni vizuri Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ikatumia Balozi zetu kwa ajili ya kuhamasisha hizo Balozi ili zitoe elimu ya utalii na uwekezaji na akataja maeneo ya Mlima Kilimanjaro, *Ngorongoro Crater,* Serengeti ambavyo vyote vipo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge lako Tukufu kwamba hiyo ndiyo kazi ambayo tunaifanya. Katika diplomasia ya uchumi naomba uniruhusu niseme machache. Mambo ambayo tunayaainisha ni pamoja na utalii, lakini tunaanza na suala la masoko.

Mheshimiwa Spika, tunalenga kuhakikisha kwamba Balozi zetu zinaisaidia nchi yetu kupata masoko yenye sifa tatu kubwa. Sifa ya kwanza, ni kwamba masoko hayo yawe na uwezo wa kutosha kununua bidhaa zetu. Kama tunalima kahawa au pamba, tuseme tani 200,000 mwaka huu tuweze kuziuza zipate masoko nje na kama mwaka kesho tukiweza kuongeza uzalishaji tukapata tani 400,000 vile vile ziweze kupata masoko. Hizo ni kazi ambazo Balozi zetu tumeziomba na tumezielekeza zifanye na sisi tunazihimiza kuhakikisha kwamba masoko hayo yanapatikana. *(Makofi)*

Lakini sifa ya pili, soko hilo vile vile liwe na tija kwa maana ya kwamba liwe na bei nzuri, inapotokea kwamba labda kuna sehemu kama tatu au nne ambazo zinakuwa na bei tofauti, basi tunalenga kuhakikisha kwamba bidhaa zinakwenda katika lile soko ambalo lina bei ya juu zaidi kwa ajili ya kumfanya mkulima na mfanyakazi wa Tanzania aweze kupata tija kwa kazi yake anayoifanya.

Sifa ya tatu ya masoko hayo ni kwamba lazima yawe yanayotabirika kwa maana ya kwamba yasiyumbeyumbe mno. Kama leo umelima karafuu,umeuza kwa kilo ukapata dola tisa, tungependa mwaka kesho iendelee kuwa dola tisa au dola kumi kuliko kushuka mpaka dola mbili, kwa sababu itakuletea hasara kubwa kama utakuwa umewekeza. Kwa utalii ni hivyo hivyo, tunahakikisha kwamba Balozi zinafanya kazi ya ziada kuwavutia watalii kwa vigezo mbalimbali. Hapa tunashirikiana na Wizara ya Maliasili

na Utalii, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Kituo cha Uwekezaji cha *TIC* na kazi kubwa hapa ni kuhakikisha kwamba vipeperushi, nyaraka na habari mbalimbali zinafika katika zile Balozi na baada ya kufika zinapelekwa kwa walengwa ili waweze kuona jinsi ambavyo nchi yetu ina rasilimali nzuri katika uwanja wa utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea vile vile hata kwenye mambo ya mitaji, kujaribu kuzielekeza Balozi zetu ziangalie mitaji ambayo ina unafuu kwa Mtanzania. Kwa maana ya kwamba tukiwekeza basi tuwekeze katika yale mambo ambayo yanampa Mtanzania nafuu zaidi. Tunaangalia vile vile suala la ajira katika maeneo ya Kimataifa ni sehemu mojawapo ya kazi zetu za diplomasia ya uchumi na vile vile suala zima la teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba wazo lake alilosema si tu kwamba tunalipokea, lakini kwa kweli tumeshaanza kulifanyia kazi na tutaendelea kulifanyia kazi jinsi hali halisi inavyoendelea kujitokeza. Nia iko pale pale na tutaweka nguvu zote mpaka tuone kwamba Tanzania inanufaika kwa kutumia Balozi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ni ule mchango mzuri kabisa ambao ametoa Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki, ambaye pamoja na mambo yake mengi aliyoongea alitushauri kwamba tutumie viongozi wetu wastaafu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki, kamtaja Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kamtaja Mheshimiwa Salim Ahmed Salim na viongozi wetu wastaafu wengineo. Kasema kwa nini tusiwatumie wakatusaidia katika majadiliano yetu ya Kimataifa na akataja suala la Doha na katika kuongea kwake kasema kwamba kwa mfano, sasa hivi Doha imefeli na haifahamiki kwamba tuko wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa faida ya Mheshimiwa Mbunge na vile vile kwa Bunge lako Tukufu, naomba tu niseme kwamba mazungumzo ambayo yalikuwa yanaendelea katika Doha yalikuwa ni mazungumzo kati ya nchi maskini na nchi tajiri na mazungumzo hayo yalikuwa yanalenga mambo yafuatayo ambayo yangesaidia nchi maskini.

Kwanza, kwenye upande wa kilimo yalikuwa yanalenga kuhakikisha kwamba nchi tajiri zinashawishiwa zikubali kuondoa ruzuku kwa bidhaa zake za kilimo ambazo wanauza nje ili tutakapokwenda sisi kuuza bidhaa zetu ziweze kupata soko. Kwa sababu wanapowapa ruzuku wale wakienda kuuza bidhaa zao nje zinakuwa na bei ndogo sana. Sisi nchi maskini tukipeleka bidhaa zetu kule haziwezi kupata mtu wa kuzinunua. Kwa hiyo, ndiyo mambo tuliyokuwa tunawaomba katika majadiliano yale.

Pili, nchi maskini au zinazoendelea zilikuwa zinaomba kwamba bidhaa ambazo sio za kilimo za nchi hizi zinazoendelea zipunguziwe ushuru zinapoingia katika masoko ya zile nchi ambazo zimeendelea. Kwa upande wa huduma nchi zinazoendelea zilikuwa zinashawishi nchi ambazo zimeendelea zifungue soko lake la ajira ili mtu kutoka nchi za dunia ya tatu aweze kwenda kule apate ajira kama vile tunavyofanya urahisi wa wao kuja kupata ajira hapa kwetu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa vile vile na kazi ya kutafuta vyanzo vya fedha ambavyo vingesaidia nchi maskini kujiinua ili ziweze kufanya biashara ambayo inakuwa na uwiano mzuri na zile nchi ambazo zimeendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazungumzo hayo kwa bahati mbaya, ambayo kama yangekubaliwa nchi ambazo zinaendelea zingepata manufaa, yameshindikana na hapa tu nitoe mifano ya ugumu wa majadiliano yale. *(Makofi)*

Kwanza, Marekani imekataa kupunguza kwa kiwango kikubwa ruzuku inayotolewa kwa bidhaa za kilimo iwapo Umoja wa Ulaya na nchi za China, India na Brazil hazitopunguza viwango vyao vya ushuru kwa bidhaa za kilimo na za viwanda. Kwa hiyo, imetoa shinikizo hilo.

Mheshimiwa Spika,vile vile kuendelea kwa Marekani na Umoja wa Ulaya kutoa ruzuku kwa bidhaa za kilimo na kutoa ushindani kwa wakulima wa nchi maskini, kumefanya mazungumzo yale yashindikane.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hii imekuwa vigumu kabisa kwa nchi zile kufikia muafaka na matokeo yake ni kwamba mazungumzo yamevunjika na nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tukiwatumia viongozi wetu wastaafu kama Mheshimiwa Benjamin Mkapa na wengineo nina imani kabisa kwamba mchango wao utasaidia katika kuzifanya nchi za dunia ya tatu kuwa na uzito katika mazungumzo hayo.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mwingine alikuwa Mheshimiwa John Lwanji, ambaye ameongea mambo mengi sana ya manufaa na ambayo napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu inayachukua kwa ajili ya kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile aliuliza kwamba *Bretton Woods Institutions* hatma yake nasi ni nini? Nilikumbushie Bunge lako Tukufu kwamba Taasisi hizi za *Bretton Woods* yaani Benki ya Dunia pamoja na Shirika la Fedha la Kimataifa zilianzishwa mwaka 1944 kwa lengo la kuzisaidia nchi za Ulaya ambazo zilikuwa zimemaliza vita ile ya Pili ya Dunia ili ziweze kufufuka kiuchumi. Baada ya kuzisaidia zile nchi, nchi za Kiafrika zilipata Uhuru miaka ya 1960 na nyingine miaka ya 1970, taasisi zile zimeanza kufanya kazi na sisi, zimeendeleza mashirikiano na sisi, nchi ambazo zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kweli ushahidi umeonyesha kwamba hakuna kitu kikubwa ambacho tumevuna kwa kushirikiana na hizi Taasisi, lakini hatuwezi kujiondoa moja kwa moja kwa sababu hii ni dunia ya utawandazi.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuongea na Taasisi hizi kuhakikisha kwamba kidogo ambacho kinapatikana tunakipata. Lakini tunatambua kama Wizara na kama nchi tunatambua kwamba mkombozi wa Mtanzania ni Mtanzania wenyewe na ndiyo maana tunasukuma sera ya diplomasia ya uchumi badala ya kuongea na hizi Taasisi ili zitupe misaada ya bure.

Mheshimiwa Spika, ni afadhali tukajizatiti, tukaimarisha sera ya diplomasia ya kiuchumi kama nilivyosema tukapata masoko, tukapata mitaji, tukapata teknolojia, hiyo ndiyo ambayo itatukwamua. Kwa hiyo, sasa hivi tunaendelea kuongea nao, lakini tunajua kwamba kazi kubwa ni kujenga uwezo wa ndani kwa maana ya kuimarisha masoko yetu, kuimarisha mitaji ambayo inakuja kwetu, mitaji yenye tija na kuhakikisha kwamba hata utalii wetu unakuwa ni ule ambao unamsaidia Mtanzania au Mwafrika au mtu wa dunia ya tatu kwa ujumla.

Kwa hiyo, napenda kumshukuru Mheshimiwa John Lwanji, kwa mawazo yake mazuri na ninamuahidi kwamba tunaelewa kama yeye anavyoelewa kwamba kwa kweli lazima katika ushirikiano wetu na hizi taasisi tuwe makini, tuhakikishe kwamba hatuendi moja kwa moja bali twende tukijua kwamba maslahi ya nchi ni kitu gani.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji wa nne ambaye nizungumzie habari zake kidogo ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ametoa mawazo mengi na hapa nitazungumzia baadhi yake na mengine atayazungumza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ameongelea suala la kuzifanyia tathmini Balozi zetu na kujua ni zipi ambazo zinafaa kwa kazi fulani maalum.

Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana naye kabisa kwamba upo umuhimu huo na kwa kweli Wizara yetu imeshaanza mchakato huo wa kuzipanga Balozi hizo. Kuna nyingine ambazo zinatusaidia kwa upande wa kiuchumi kupata mitaji, kupata masoko kwa ajili ya bidhaa zetu. Kuna nyingine ambazo nguvu zake zaidi ni kwenye uhusiano wa Kimataifa na nyingine ambazo nguvu zake kabisa ni mambo ya kisiasa. Kwa hiyo, tumezigawa vile na kwa kuzingatia uchambuzi huo hata uteuzi wa Balozi, mamlaka ya uteuzi inashauriwa iteua Mabalozi ambao wakienda kule wanakidhi haja ya hiyo, tunayoita *categorization.*

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge vile vile kwamba hata maafisa wetu tumeanza kuwapeleka kulingana na uzito huo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mahomed ameulizia kwa nini Wizara yetu haina Bajeti ya Maendeleo. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa Wizara yoyote bajeti ya Maendeleo ni muhimu kabisa. Lakini bila kuongelea uwezo wa Serikali hapa niseme kwamba kwa desturi imekuwa ikifahamika kwamba Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa labda kwa kupitia Balozi zetu inakusanya maduhuli, yale maduhuli yanabakia kule kule kwa ajili ya kufanya kazi ya kukarabati majengo, kununua majengo na labda kununua magari na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Wizara yangu imegundua vilevile kwamba hizo fedha ni kidogo sana haziwezi kuendeleza Balozi hasa ikizingatiwa mahitaji halisi ya majengo na vitendea kazi katika zile Balozi.

Kwa hiyo, tunaifanyia kazi kama Serikali kuhakikisha kwamba miaka ijayo sasa Wizara yetu itafikiriwa kwa ajili ya kupata fedha za maendeleo ili zile Balozi zetu ziweze

kupata majengo yanayotakiwa na vitendea kazi vingine. Lakini namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa wazo lake hilo ambalo na sisi tulikuwa tumelichukua.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. DR. CYRIL A. CHAMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa natamka kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile hii ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, naomba uniruhusu kwanza nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na mgombea mwenza wake Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa ushindi mkubwa waliopata katika Uchaguzi Mkuu uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa ushindi wa kishindo aliopata kule Zanzibar. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuthibitishwa na Bunge hili Tukufu. Bunge lilifanya uamuzi sahihi wa kumthibitisha Mheshimiwa Edward Lowassa, kwani kazi yake tunaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika wako kwa kuchaguliwa kwenu kutuongoza katika Bunge hili, mnafanya kazi nzuri hasa wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, ukiwa mzee wa kasi na viwango. Kweli kasi yako na viwango vyako tumeviona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa ushindi wao mkubwa waliopata. Pia nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa imani walioipata kutoka kwa Mheshimiwa Rais kwa kuteua kuitumikia Serikali ya Awamu ya Nne nikiwemo na mimi mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuzishukuru familia zangu wakiwemo wake zangu Bi Pili Juma Iddi na Bi Asha Suleiman Mohamed kwa kunisaidia, kunifariji na kunitia moyo katika mchakato mzima wa uchaguzi. Kwa namna ya pekee namshukuru Bi Asha Suleiman Mohamed kwa kunisaidia kulisimamia Jimbo ikiwa ni pamoja na kutatua matatizo yanayojitokeza wakati mwenyewe siko Jimboni. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru wananchi wote wa Jimbo la Kitope, kwa heshima hii waliyonipa ya kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu. Kama nilivyowaahidi nitawatumikia kwa nguvu zangu zote na uwezo wangu wote. Nawashukuru marafiki

zangu wote wa kike na kiume walionisaidia kwa hali na mali katika mchakato mzima wa uchaguzi kuanzia kura za maoni hadi uchaguzi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa namshukuru Waziri wangu, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa maelekezo na mwongozo anaonipa na kila msaada anaonielekeza ili niweze kutimiza wajibu wangu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, najua wamefanya hivyo kwa nia safi kabisa ya kutusaidia tufanye kazi zetu vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu baadhi ya hoja hizo kadri muda utakavyoniruhusu. Hoja zitakazobakia kinara wetu mtoa hoja atakuja kuzimalizia kuzijibu.

Mheshimiwa Spika, naanza na hoja ya Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki, aliuliza kwa nini Tanzania inataka kufungua Ofisi za Ubalozi nchini Brazil na Malaysia badala ya kuifungua tena Ofisi yetu ya Ubalozi iliyoko The Hague, Uhalonzi ambapo tayari tuna nyumba kule Uholanzi.

Mheshimiwa Spika, hoja hii pia imetolewa na Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa hoja hii ya msingi. Aidha, napenda kutoa maelezo kwamba huko The Hague, Uhalonzi tunayo nyumba moja tu ambayo ni makazi ya Balozi na kwa sasa nyumba hiyo inapangishwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali ina mpango wa kufungua Ofisi za Ubalozi Brazil na Malaysia. Hatua hii haina maana kuwa hatuna mpango wa kufungua tena Ofisi ya Ubalozi nchini Uholanzi kwa sababu ya kutambua umuhimu wake kwetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu iko kwenye mchakato wa kuishauri mamlaka husika juu ya suala hili kwa kuzingatia ukweli kwamba mazingira ya kufungua tena Ubalozi Uholanzi yanaruhusu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, yeye amesema kwamba kwa kuwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, alipokuwa nchini Brazil aliahidi kwamba Serikali ya Tanzania itafungua Ubalozi wa Tanzania nchini Brazil. Serikali iharakishe kufungua Ubalozi huo ili Tanzania inufaike na ushirikiano katika nyanja za nishati, madini, michezo, kilimo na afya.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Mpwapwa kwa maoni yake mazuri. Wizara yangu itaanza mchakato wa kufungua Ubalozi Brazil

mara baada ya kupitishwa kwa Bajeti ya Wizara yangu kwani fedha zake zimekwishatengwa kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika,wako wachangiaji wengine ambao wamechangia kwa maandishi. Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe ametoa pendekezo kwamba mikataba mbalimbali ya uwekezaji na makampuni ya kigeni ni vyema iangaliwe vizuri na kwa kuwatumia wataalam wetu kabla ya kujiunga nayo ili ijulikane kwamba ina maslahi kwa Taifa letu na si kinyume chake.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru kwa pendekezo hili. Hata hivyo, kwa vile Wizara yangu haihusiki moja kwa moja na mikataba ya aina hii itashauriana na Wizara zinazohusika ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inafaidika na mikataba ya aina hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, ametoa rai kwamba Zanzibar kama nchi hakuna budi kuipa fursa ya uhusiano wa kiuchumi na Mashirika ya Kimataifa ili kukuza uchumi wake na isiwe kinyume chake pale ilipojiunga na *OIC* ikaambiwa ijiondoe. Suala hili litajibiwa na Mheshimiwa Waziri baadaye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Balozi Hamis Suedi Kagasheki na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, walizungumzia suala la uteuzi wa Mabalozi.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa hoja za busara za Waheshimiwa Wabunge na napenda kujibu kwamba tumezingatia ushauri walioutoa juu ya uteuzi wa Mabalozi na mamlaka husika zitazidi kushauriwa kuzingatia vigezo walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge ili kuleta uwiano katika uteuzi hususan jinsia na kati ya wanasiasa na wana diplomasia.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro na Mheshimiwa Lucy Owenya, walizungumzia nafasi za kazi Ubalozini na sifa za maafisa wanaofanya kazi Ubalozini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilishaona mapungufu hayo na ilishaanza kuyafanyia kazi. Tayari Wizara imechagua na kupanga Ofisi zetu za Ubalozi nje katika mafungu matatu. Kuna ofisi za Balozi zinazoshughulikia mambo ya uchumi, kuna ofisi za Balozi zinazoshughulikia mahusiano ya Kimataifa na ziko ofisi za Balozi zinazoshughulika na mambo ya kisiasa. Kwa kuzingatia uchambuzi huu watumishi watapelekwa ofisi ya Ubalozi kwa kulingana na sifa zao na kwa kulingana na mahitaji ya kila Kituo.

Napenda kujibu hoja za Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Rosemary Kirigini na Mheshimiwa Fuya Kimbita. Walitoa hoja kwamba Serikali iboreshe maslahi ya watumishi walioko Balozini kwa kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kujali maslahi ya watumishi wetu walioko Ubalozini. Wizara inashughulikia tatizo hili kama ilivyoelezwa katika hotuba yetu ya bajeti kifungu cha 76.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya Mheshimiwa Devota Likokola na Mheshimiwa Lucy Owenya, kwamba kuna Mabalozi wangapi wanawake kati ya Mabalozi wetu walioko nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mabalozi Wanawake wanaowakilisha nje wapo wanne ambao ni Balozi Eva Nzaro yupo New Delhi, India, Balozi Mwanaidi Maajar aliyeko London, Uingereza na Balozi Nyasungara Kadege wa Kituo cha Nairobi Kenya ambapo pia kuna Naibu Balozi Mary Mushi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Balozi Hamis Suedi Kagasheki, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed pamoja na Mheshimiwa Juma Said Omar. Waheshimiwa Wabunge hawa wameishauri Wizara ikarabati na kuzifanyia matunzo nyumba zake.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya bajeti kifungu 77, Wizara inazingatia ushauri huo na itaongeza juhudi katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, uwiano wa watumishi kwa pande zote za Muungano. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu inaajiri kwa kufuata taratibu zote za ajira kama zilivyoanishwa na Tume ya Utumishi wa Umma. Nafasi wazi za kazi hutangazwa katika vyombo vya habari na kukaribisha maombi kwa kuzingatia sifa zinazohitajika. Aidha, Wizara yangu imefanya juhudi za makusudi za kuongeza idadi ya watumishi kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuhamishia Wizarani watumishi sita katika mwaka 2005/2006. Napenda kutumia fursa hii kuwashauri waombaji wa nafasi za kazi kutoka Zanzibar kujitokeza kwa wingi katika kushindania nafasi zinazotangazwa. Hii itatusaidia vile vile kupata watumishi bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya, alitaka kujua upatikanaji wa *visa* za Marekani na Uingereza umekuwa mgumu sana kwa Watanzania. Wizara ina mpango gani wa kuondoa kero hii ya upatikanaji wa *visa* kwa wananchi. Wizara yangu imekuwa ikijitahidi kutatua tatizo hili kwa njia ya demokrasia ikiwa ni pamoja na kuwaita Mabalozi husika na kuwasilisha tatizo hilo. Aidha, Wizara itaendelea juhudi za kushirikiana na Balozi hizo ili kupata ufumbuzi wa tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ametoa hoja kwamba Tanzania ina jumla ya wawakilishi wa heshima wangapi na taratibu gani zinatumika katika kuwachagua. Wawakilishi wetu wa heshima wako 16, Wizara imeandaa taratibu za mikataba mipya ya uteuzi na usimamizi wa utendaji kazi wa wawakilishi kwa heshima yaani *protocol manual* kutoka Januari, 2005. Lakini Wizara inazingatia zaidi kuwateua

wale Mabalozi wa heshima ambao wanaheshimika, waadilifu na waaminifu kusaidia katika kazi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, yeye alitoa pongezi na napenda kumshukuru Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini kwa pongezi alizotoa kwa Wizara yangu hasa kwa Mkuu wa Itifaki Balozi Cisco Mtiro kwa mada yake wakati wa semina elekezi ya Wabunge kuhusu masuala ya Itifaki iliyofanyika *Ubungo Plaza*, Dar es Salaam. Wizara yangu iko tayari kuendelea kutoa semina za aina hiyo ili kuendelea kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuhusu masuala ya Itifaki.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Mohamed Rished Abdalla, Mbunge wa Pangani juu ya ufunguzi wa Ubalozi nchini Oman. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kuhusu suala lake kuhusu hoja ya Serikali ya kufungua Ubalozi huko Oman. Napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari imefungua ubalozi huo Muscat, Oman mwaka 2004 na hivi karibuni Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alimteua Mheshimiwa Hussein Khatib kuwa Balozi wetu huko Oman. *(Makofi)*

Mheshimiwa Paul Kimiti, ametoa hoja ya kuimarisha ujirani mwema, kuandaa mkakati wa kudumu wa kuwashirikisha Wabunge wa nchi jirani kuanza kutembeleana ili kujenga misingi imara ya mahusiano ya kudumu.

Mheshimiwa Spika,ujirani mwema ni mojawapo ya msingi wa sera yetu ya nchi za nje. Kwa msingi huu nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya kuimarisha ujirani mwema, ujirani wetu ikiwa ni pamoja na njia hii ya kutembeleana Wizara yangu itakuwa tayari kusaidia mawasiliano hayo endapo Bunge litawawezesha Waheshimiwa Wabunge kufikia azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Adam Malima, ambaye ametoa shukrani na utatuzi wa mgogoro wa Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia hoja ya Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipoanza mpaka ilipofika saa 5.30 asubuhi hivi ilielekea kama wachangiaji walikuwa wachache sana, lakini kama mtakavyoona wale ambao mnaweza kuniona makaratasi yako mengi kwa kweli wachangiaji walikuwa wengi.

Napenda kuchukua fursa hii kwanza kuwatambua na kuwashukuru waliochangia kwa kauli na hao ni Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mbunge wa Kilindi, Mheshimiwa Khalifa Suleimani Khalifa, Mbunge wa Gando, Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki, Mbunge wa Bukoba Mjini, Mheshimiwa John Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, Mheshimiwa

Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao na nawashukuru na kuwatambua, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Fatma Mikidadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, endapo kuna ambao kwa hali ya kibinadamu tutakuwa tumewaruka, tutapenda kuwafahamu ili tuwatambue rasmi, lakini napenda nikushukuruni nyote kwa michango yenu.

Mheshimiwa Spika, napenda nijielekeze katika baadhi ya hoja ambazo wenzangu Naibu Mawaziri hawakuzigusia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na hoja ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Kwanza tunamshukuru Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, kwa mchango wake katika hotuba yetu sisi. Lakini naomba nijielekeze kwa maeneo ambayo nadhani alikuwa ameyataka majibu. Mengine yalikuwa ni maeneo ya ushauri na naomba kumhakikishia kwamba yale ya ushauri tutayafanyia kazi. Alikuwa amependa kutuuliza ni mapato gani ambayo yalichangiwa na kila Ubalozi kwa mwaka uliopita.

Napenda nimjibu Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, kwamba katika mwaka wa fedha 2005/2006 makusanyo ya maduhuli yaliyopatikana katika Balozi zetu ni shilingi 9,569,999,000/=. Ninao mchanganuo wa Balozi zetu na kuokoa muda nitapenda tu baadaye niweze kumpatia Mheshimiwa Mbunge lakini pia na Bunge lako Tukufu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua gani kwa Mabalozi ambao utendaji wao haukuridhisha katika kuhamasisha ukusanyaji wa maduhuli. Kwa kweli katika Wizara yetu maduhuli kwa kiasi kikubwa yanatokana na upatikanaji wa fedha zile za *visa* na sio Balozi zote ambazo zinakuwa na maombi mengi kwa maana ya kwamba kila Balozi kuwa na maombi mengi. Ukusanyaji wa maduhuli yanayotokana na fedha za *visa* unatokana na wasafiri wanaokuja nchini kwetu na wao mara nyingi mtawanyiko wao unakuwa ni wa kijiografia.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati mwingine nchi fulani zinaleta maombi mengi zaidi ya *visa* hasa katika msimu wa majira ya joto na kadhalika. Kwa hiyo, hatuwezi

kusema kwamba kuna Balozi ambazo hazikukidhi viwango. Lakini maduhuli ya Serikali yamekuwa yakipatikana na kila yalipopatikana yameingizwa katika utaratibu wa kawaida wa kutumia fedha za Serikali ambazo zinasimamiwa na Mhasibu Mkuu ambaye ndiyo Katibu Mkuu wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake pia Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, alitaka kujua kwamba tunachukua hatua gani katika kushughulikia kasoro zinazojitokeza kutokana na hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Utaratibu ulioko ni kwamba hoja zote ambazo zipo katika Taarifa ya Mkaguzi Mkuu huwa zinajibiwa kwenye Kikao cha Kamati ya Fedha za Umma na hilo limekuwa likifanyika na kwa mwaka huu tunasubiri maelekezo maalum kutoka kwenye taarifa hii ya kutoka kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali ili tujue kuna maagizo gani ambayo tuweze kuyashughulikia.

Mheshimiwa Spika, lakini yale yote ambayo yalikuja tumeyashughulikia na tumetoa taarifa na sasa tunasubiri nini kitakuwa hatma ya yale ambayo tuliyatolea maelelzo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujibu hoja hizo napenda pia nimhakikishie Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, kwamba yapo maeneo ameyazungumzia ya uwekezaji ya sisi kufanya tathmini wenzangu nadhani wameyazungumzia. Lakini labda tu niongeze sauti yangu kwa kusema kwamba kimsingi hilo ndilo ambalo tunalifanya ndani ya Wizara. Kwa sasa hivi kwa kuwa tumesema kwamba sera yetu ya Mambo ya Nje imejikita katika diplomasia ya uchumi basi tunafanya tathmini za Balozi zetu, tathmini za maeneo Balozi zilizopo tuone zinaweza zikachochea vipi maslahi ya kiuchumi kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakapokuwa najibu baadhi ya hoja nyingine nitakuwa ninaziruka zile ambazo zimeshashughulikiwa ingawa nitarejea kule kule kwa wenzangu kwa kuwataja wale waliozungumza. Katika hoja ambazo alizizungumzia Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki, alikuwa ametuuliza kwamba utaratibu ule wa kuwapeleka watumishi katika Balozi zetu kutokana na sifa na uwezo walionao. Wenzangu wameshajibu lakini napenda kuongeza kwa kusema kwamba katika hotuba yetu tumeeleza kwamba tumeweka mpango maalum wa mafunzo, mpango ule ni hatua mojawapo ya kuweza kuhakikisha kwamba watendaji tulionao, wafanyakazi tulionao wanakuwa na mbinu na stadi ambazo zinastahiki kwa wao kwenda kwenye vituo ambavyo vinahusika.

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, alizungumzia suala la jengo Italy katika jiji la Rome na kwamba alisema utaratibu haukufuatwa na kadhalika na alitutaka tutoe maelezo kuhusu hilo.

Napenda kumwambia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia katika eneo hilo kwamba kama ambavyo mmefahamu suala hili sasa hivi linafanyiwa uchunguzi. Lakini kubwa lililojitokeza ni kwamba kama kiasi cha wiki moja tu iliyopita Balozi Costarik Mahalu, amefungua kesi ya madai, hiyo ni kesi namba 104 ya mwaka 2006 ambapo anawashtaki watu fulani

fulani na kwa mujibu wa sheria za nchi yetu ni kwamba yale tunayozungumza ndani ya Bunge hili yanaweza yakatumiwa kama ushahidi katika kesi. Kwa hiyo, kwa kuchelea kuwa na athari mbaya au athari nyinginezo kwenye kesi hizi ningeomba kwamba tueleze tu kwamba suala hili hivi sasa liko Mahakamani na haitakuwa vema sisi kulitolea kauli hapa kwa namna ambayo linaweza likaathiri mwenendo wa kesi hii. Lakini mpaka kwa hatua iliyofikia nadhani lilikwishajibiwa kwamba uchunguzi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na hoja hapa imejitokeza nadhani ni ya Mheshimiwa John Lwanji, yeye alikuwa amezungumzia mchango ambao sisi tumeutoa katika nchi yetu na kwamba je, tunanufaika nini hivi sasa baada ya kuwa tumechangia kwa kiasi kikubwa?

Ningependa tu kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba kazi tuliyoifanya ya kuchangia ukombozi Barani Afrika na katika maeneo mengine ya dunia hii inatokana kwa kweli na azma yetu inatokana na dhamira yetu ya kuweza kushughulika au kuwasaidia wale ambao wako katika madhila au wako katika matatizo fulani fulani.

Mheshimiwa Spika, labda tu tukijikumbusha sisi Watanzania wenyewe wale ambao walikuwa ni wanachama wa *TANU* na sasa hivi wanachama wa *CCM* mtakumbuka kwamba mojawapo ya misingi yetu ni kwamba binadamu wote ni sawa na Afrika ni moja hili lilikuwa ni mojawapo ambalo lililotusukuma sisi kuchukua silaha na kuwasaidia wenzetu. Lakini itakumbukwa kwamba hata katika maadili ya Taifa letu tunakumbuka ule wimbo wa kuwasha mwenge, tunasema, sisi tunataka kuwasha mwenge tuuweke Mlima Kilimanjaro, umulike nje ya mipaka yetu, uweze kuleta matumaini ambako hakuna matumaini, ulete upendo penye chuki, ulete heshima mahali ambapo pana dharau.

Mheshimiwa Spika, hayo yote ni mambo ambayo sisi wenyewe tunayaamini kama Taifa na ndiyo yaliyotusukuma. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo tulikuwa tunatimiza wajibu wetu na sidhani kama kwa kweli tunategemea malipo zaidi ya sisi wenyewe kupata faraja kwamba tunaishi katika Bara ambalo ni huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepata pia mchango ambao unahusu haja ya kushirikiana na Shirika linalojulikana kama *International and Inter Religious Federation for World Peace*. Hoja hiyo imetolewa na Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga na alikuwa ametuuliza sisi tunafanya nini na tutashirikiana nalo vipi?

Napenda kumhakikishia kwamba Serikali yetu kwa kweli inathamini sana ushirikiano na taasisi kama hizi na sina shaka kama ambavyo Mheshimiwa Paul Kimiti, yeye sasa hivi ndiyo kiongozi wa tawi letu lililoko hapa, tutashirikiana naye na tutaendelea kushirikiana kwa sababu kwa kweli suala la amani ni suala ambalo halina mwenyewe na Mashirika yawe ya kidini au yawe tofauti na kidini tutashirikiana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepata pia hoja kutoka kwa Mheshimiwa Adam Malima, Mbunge wa Mkuranga, ambaye alikuwa anapenda kuuliza ni kwa nini Tanzania hadi leo haijajiunga na *OIC* wakati kuna nchi nyingi za Afrika ambayo ni wanachama wa Umoja huu zinafaidika kiuchumi. Nakubaliana na Mheshimiwa Adam Malima kwamba ziko nchi nyingine pia za Kiafrika ambazo zinashirikiana na Shirika hili na kwa kweli Shirika hili lina malengo mengi, mojawapo ni lengo hilo la kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, lakini kama mtakavyokumbuka Waheshimiwa Wabunge hoja hii iliwahi kuzungumzwa kwa kina kabisa katika Bunge hili Tukufu katika mwaka wa1993 nadhani ilikuwa ni kikao cha mwezi wa Februari na kilichozungumzwa na ambacho ndicho hicho kinachotokea sasa hivi ni kwamba Serikali yetu ichukue muda kulielewa Shirika hili, kufanya mashauriano ili tuone kama kuna uwezekano.

Mheshimiwa Spika, lakini ikumbukwe tu kwamba Waheshimiwa Wabunge, Shirika likiwa la kiuchumi tunapotaka kuingia sio maslahi ya kiuchumi peke yake ambayo yanaamua tuingie lakini viko vigezo vingine. Kwa hiyo, tuendelee na mjadala, tuendelee kulitafakari suala hili kama ambavyo tayari mwongozo huo ulikuwa umeshatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile tumepata mchango wa Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe, yeye ametoa pendekezo kwamba mikataba mbalimbali ya uwekezaji na makampuni ya kigeni ni vyema yaangaliwe vizuri wakatumia wataalamu wetu. Nadhani huo ni ushauri mzuri na kama mtakavyokumbuka Rais wa Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Jakaya Kikwete, alisema ipo haja ya kupitia kwa mfano baadhi ya mikataba nadhani katika utaratibu huo tutakuwa makini ili kuhakikisha kwamba mikataba hiyo inatunufaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum alikuwa ameuliza je, Tanzania ikiwa ni Mjumbe wa Baraza la Usalama, Serikali ina msimamo gani kuhusu mashambulizi ya Israel na Lebanon? Labda tu niseme kwamba katika suala hili sisi kama Wajumbe wa Baraza la Usalama wa Umoja wa Mataifa hivi sasa hatutatofautiana na msimamo au mwelekeo ambao unachukuliwa ndani ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Tunachosema ni kwamba kwanza kabisa Tanzania inatoa wito kwa pande zinazopigana kuacha mapigano, hilo ni la kwanza. Lakini pili, tunasema pia kwamba kutokana na vita hii kumekuwa na janga kubwa la mahitaji ya kibinadamu kwa hiyo, tunaziomba nchi za Umoja wa Mataifa, tunaiomba Jumuiya ya Kimataifa ijielekeze katika kushughulikia janga la kibinadamu lililotokea hivi sasa. Mtakumbuka miundombinu mingi imeharibiwa, wananchi wamepoteza maisha yao na kwa taarifa tulizonazo ni kwamba Kamishna yaani *Egalant* ambaye anahusika na masuala ya maafa tayari ametembelea eneo lile kwa ajili ya kuona ni mahitaji gani. Kwa hiyo, tunatoa wito kwamba tuweze kujielekeza huko na tuweze kusaidia. Vile vile tunatoa wito kwa wale askari wawili walioshikiliwa waweze kuachiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini itakumbukwa kwamba ndani ya Umoja wa Mataifa mwaka 2004 kulipitishwa Azimio Na. 15/59 la mwaka 2004 ambalo linasema kwanza na hili ni muhimu sana katika kushughulikia suala la Lebanon kwamba Umoja wa Mataifa

unaamini katika Taifa la Lebanon kuwa ni Taifa huru na kwa kufuatia hivyo basi Azimio hili lilitaka majeshi yote ya kigeni yaliyokuwa Lebanon yaondoke na yako ambayo yaliondoka lakini ndani ya Lebanon kuna vikundi vya wanamgambo ambavyo ni pamoja na kikundi hiki cha Hizbra. Kwa hiyo, Azimio hili lilitaka vikundi hivi vivunjwe na pia vinyang'anywe silaha na kwamba Jumuiya ya Kimataifa ishirikiane na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa katika kuhakikisha kwamba hivi vikundi vinapokonywa silaha.

Lakini kubwa zaidi ni kwamba humo humo ndani ya Umoja wa Mataifa kupitia Baraza lake la Usalama ilifahamika wazi na ilikubalika kwamba kikundi hiki cha Hizbra ambako kiko katika eneo la Kusini la Lebanon kina nguvu kushinda Serikali yenyewe ya Lebanon kwa maana ya kwamba ile Serikali haina udhibiti wa kutosha wa eneo la Kusini mwa Lebanon na kwa ajili hiyo basi iliamuliwa kwamba Jumuiya ya Kimataifa ishirikiane kwanza katika kuiwezesha Lebanon kuwa na uwezo wa kushughulikia hilo tatizo la hao wanamgambo. Lakini pili kusaidia kuwapokonya silaha. Jukumu hilo halikupewa Israel peke yake, imepewa Jumuiya ya Kimataifa.

Kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa ni kwamba msimamo wa Tanzania ni msimamo ambao unakwenda sambamba na maamuzi ambayo tayari yameshatolewa ndani ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Swali hilo pia limeulizwa na Mheshimiwa mwingine sioni hapa jina lake lakini napenda pia ichukuliwe nimemjibu na Mheshimiwa ambaye nadhani nitaona jina lake hapa ilikuwa ni Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa mwingine wakitaka kujua tuna msimamo gani kuhusu mashambulizi yanayotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeuliza kuhusu Mradi wa Hashim Mbita. Huu ni mradi ambao umebuniwa na unatekelezwa na Jumuiya ya *SADC*, si mradi wa Tanzania peke yake, gharama za mradi huu zitashughulikiwa katika utaratibu wa *SADC.* Mwenzetu Mheshimiwa Balozi Hashim Mbita ni mmojawapo kwa kweli atakayekuwa katika msitari wa mbele katika kufanikisha mradi huu. Sio tu kwamba umepewa jina lake lakini yeye atashiriki kikamilifu kwa sababu ni mmoja wa wale ambao walitoa mchango mkubwa. Mtakumbuka alikuwa ni Katibu Mtendaji wa Kamati ya Nchi za Afrika wakati ule ya Ukombozi. Kwa hiyo, yeye atakuwa ni mlezi lakini atatoa pia mchango wake.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeulizwa hapa sina hakika kama wenzangu walilijibu suala la Mheshimiwa Fatma Mikidadi kuhusu *Mtwara Corridor.* Nadhani naweza nikalizungumzia kidogo. Mheshimiwa Fatma Mikidadi ameuliza kwamba miradi iliyo chini ya *Mtwara Development Corridor* itaanza kutekelezwa lini. Nina imani kabisa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko atakapotoa hoja yake atalizungumzia. Lakini labda niseme pia katika mfumo wa *SADC* huu ni mradi ambao unapewa umuhimu sana. Kwa sababu mradi wa *Mtwara Development Corridor* utatuunganisha sio tu sisi Tanzania ndani kama nchi, lakini utatuunganisha pia na Mataifa mengine kama vile Msumbiji, Malawi, Zambia. Kwa hiyo, ni mradi ambao umewekwa katika miradi mikuu ya *SADC.* Na *SADC* itakapokuwa inatafuta ufadhili au ubia katika kutekeleza miradi hii na huu mradi utakuwa ni mmojawapo, lakini itoshe tu kusema

kwamba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko na nina imani kabisa atalizungumzia kwa kina suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeulizwa pia suala la kwa nini Tanzania ilijitoa *COMESA*. Hilo nadhani limeshajibiwa na wenzangu kwa nini tulijitoa *COMESA*. Hujalijibu Mheshimiwa? Samahani nilikuwa napekua pekua mno makaratasi hayo. Labda niseme kwamba wakati uamuzi ulipopitishwa kwamba Tanzania ilitakiwa ijitoe *COMESA* ilikuwa ni baada ya wafanyabiashara wengi kuitaka Serikali kwamba labda tujitoe tulikuwa hatuna manufaa makubwa, tulikuwa tunaelemewa na mzigo wa kulipa ada na kadhalika. Kwa maoni hayo ya wafanyabiashara ilionekana wakati ule tujitoe. Lakini sasa hivi yako pia mawazo na maoni kwa kweli niseme kwamba Serikali sasa hivi inashauriwa kwamba tuangalie tena utaratibu wa kurudi *COMESA*.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Serikali ni kwamba Serikali hii ni sikivu, kama zipo hoja ambazo sasa ni tofauti na zilizokuwepo wakati ule Serikali itaziangalie hoja hizo itazipima kwa uzito wake na uamuzi muafaka utafikiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini ifahamike kwamba Serikali ilifanya hivyo wakati ule kwa kusikiliza kilio cha wafanyabiashara na sasa hivi itakuwa tayari kusikiliza na tutafuata utaratibu ili tena tuweze kurudi kwenye mamlaka husika kwa ajili ya kuona kwamba tufike kule au tusifike.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala pia la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Koani. Je, kuna utaratibu wowote kwa Balozi zetu kuwasaidia raia wa Tanzania wanapopata matatizo kwenye nchi zao za uwakillishi?

Mheshimiwa Spika, huo utaratibu upo na mara kwa mara Serikali ilikuwa ikitoa wito kwamba raia wetu wanaposafiri kwenda nchi za nje waweze kupiga ripoti kwenye kituo cha Ubalozi kama kipo. Lakini kama hakipo uko utaratibu wa nchi mbalimbali kuweza kutuwakilisha na mara nyingi nchi kama Uingereza hutumika kuweza kuangalia maslahi yetu kwa hiyo wale wanaojiandikisha inakuwa ni rahisi endapo kutapotokea shida yoyote kwa wao kuweza kusaidiwa. Kwa hiyo, hili huwa linatokea.

Mheshimiwa Spika, tumeulizwa vile vile na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, ametuuliza kuhusu suala la Kiswahili. Nashukuru kwamba leo hii suala pia liliulizwa hapa Bungeni na lilijibiwa vizuri. Labda niseme tu kwa upande wa Wizara yetu sisi tunaendelea kuwasiliana na Serikali ya Libya kupitia Ubalozi wao uliopo Dar es Salaam ili kubainisha utaratibu mzuri zaidi wa kuweza kuwatoa walimu hapa pale ambapo maandalizi yatakuwa yamekamilika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na jitihada hizi Wizara yangu pia itaendelea kama ilivyosemekana asubuhi tutaendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu, Habari na Michezo ili kuona tunakuwa na utaratibu gani wa kuandaa walimu hawa waweze kuchukua nafasi hizi ambazo zinahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini ni yeye ambaye jina lake lilikuwa limenitoka alikuwa ametuuliza msimamo wa Tanzania kuhusu mgogoro huu wa Mashariki ya Kati unavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, Israel kushambulia Lebanon na Mamlaka ya Palestina nadhani tumeeleza vizuri labda niseme tu kwa upande wa Palestina ni kwamba katika nchi ile hivi sasa chama kinachoongoza ni *Hamas* kilifanya uchaguzi wake vizuri, kilichaguliwa kihalali na Umoja wa Mataifa ulitambua uchaguzi ule kwamba ulikuwa huru wa haki na salama.

Kwa hiyo, kwa kweli kinachotokea hivi sasa kwa upande wa Palestina ni jambo la kushambuliwa kutokana na uamuzi wa wananchi wale pamoja na sababu nyingine kuichagua *Hamas.*

Mheshimiwa Spika, lakini sisi Tanzania kama nilivyosema tunakwenda sambamba na maamuzi ya Umoja wa Mataifa ambayo tunayaamini lakini pia kwa kuwa sisi ni Wajumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa tunaungana na Baraza hilo kusema kwamba tunatambua uchaguzi wa *Hamas* kwani ulifanywa na wananchi wenyewe na tayari umeshachukuliwa kwamba ni uchaguzi huru, haki na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati najibu hoja aliyozungumzia Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, nadhani kuna moja ambayo niliiruka na hili lilikuwa linahusu wananchi ambao wametueleza kwamba waliuawa kutokana na wakimbizi katika vijiji viwili vilivyoko jimboni kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana na naungana na Mheshimiwa Mbunge kuwapa pole wale ambao walikumbwa na tukio hili la kuhuzunisha. Labda nimwombe tu Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi kwamba atuletee taarifa kamili ili tuone kwamba kwa kutumia njia za kidiplomasia tunaweza kufanya nini ili haki iweze kutendeka.

Mheshimiwa Spika, tumeulizwa kuhusu ujenzi wa Chuo cha Diplomasia kinashiriki vipi katika kuandaa sera ya nje na kufanya utafiti. Nadhani hili linaweza kuwa limegusiwa lakini niseme kwamba kwa mwaka ujao wa fedha mambo ambayo tutayafanya kuhusiana na chuo hiki ni kukifanya kiwe chuo sio tu kitakachotoa taaluma bali kitakachoweza pia kutushauri kwa mambo ya kisera, kufanya utafiti na kufanya pia tathmini ya Balozi zetu kama ambavyo imeshauriwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala lililoulizwa hapa kwamba nchi zile ambazo ziliahidi, Mheshimiwa Mporogomyi aliuliza kwamba kumekuwa na ahadi zinazotolewa na nchi zilizoendelea kwa mfano kupitia Mkutano wa Gleneagles, kwamba waliahidi watatusaidia, sasa wanatusaidiaje? Kuna ahadi ambazo hazikutekelezwa. Niseme tu kwamba kwa kawaida tunasema ahadi ni deni. Lakini katika eneo hili la ahadi za wenzetu hawa, sisi ndani ya Wizara yetu tumekua tukiongea nao kupitia taratibu za kidiplomasia na pia tumekuwa tukijaribu kuainisha ile miradi ambayo inaingia katika programu zilizozungumziwa katika Mkutano ule Gleneagles.

Kwa mfano, nchi ya Uingereza imetoa kitabu ambacho kwa bahati mbaya hatuna hapa, lakini imetoa kitabu na nadhani tutajitahidi kukipata ili tuweze kuona taarifa zile zinawafikia vipi Waheshimiwa Wabunge au zinawafikia vipi sekta zinazohusika. Lakini nchi ya Uingereza kitabu kikionyesha kwamba katika kipindi fulani nchi hiyo itatimiza ahadi yake katika maeneo, kwa mfano katika maeneo ya afya imejielekeza vizuri kwamba kama tunazungumzia haja ya kufanya umaskini uwe historia tufanye nini katika afya. Mojawapo ni kuangalia magonjwa kama UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria na kadhalika. Lakini kwa mfano kwenye eneo la elimu wamejielekeza kulekule kwenye malengo ya milenia ambayo asubuhi kwenye hotuba yangu niliyazungumza. Kwa hiyo, kipo hicho kijitabu na tutajitahidi taarifa hizo kama ilivyo kawaida tulivyosema kwamba tutatoa taarifa za kuwezesha kuchukua fursa hizo za kimataifa tutakitafuta na tutaweka katika utaratibu.

Mheshimiwa Spika, lakini hivi karibuni kwa mwezi huu huu wa Julai kulikuwa na Mkutano wa nchi hizi zinazojiita *G8* na ambazo pia walipitia maeneo mbalimbali waliyoyatolea ahadi toka walipokutana kule *Gleneagles*. Sasa maeneo hayo yapo katika taarifa ambayo tunadhani na yenyewe tunaweza tukaipata, lakini Mkutano huo ulikwisha juzi tu tarehe 16 Julai, 2006. Sina shaka na matokeo ya Mkutano huo yatakuwa ni kujielekeza katika maeneo yale ambayo waliahidi. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya kazi na Balozi zilizoko hapa ili tuangalie nini tunaweza kushirkiana nao katika kuhakisha kwamba ahadi walizozitoa wanazitimiza na sisi tuna nufaika nazo.

Mheshimiwa Spika, kulitolewa hoja hapa na hii kweli niseme sio hoja, niseme tu ulikuwa ni ushauri na tunaupokea vizuri, huu ni ushauri ambao umetolewa na Mheshimiwa Membe, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Yeye ametushauri kwamba Chuo chetu kiweze sasa kuwa ni Kituo cha kushughulikia masuala ya migogoro na kuleta utengamano katika nchi za Maziwa Makuu. Nadhani huu ni ushauri mzuri sana kwa sababu unakwenda sambamba pia na jitihada za nchi yetu za kuleta amani katika aneo la Maziwa Makuu.

Tumepokea pia ushauri kutoka kwa Mheshimiwa Dr, Batilda Buriani, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Yeye anataka kuona ni hatua gani hasa zinachukuliwa na anapendekeza kwamba tuhakikishe kunakuwa na mipango maalum ya kushughulikia watoto ambao wameingizwa katika migogoro ya kivita na hasa katika eneo hili la Maziwa Makuu. Tunapokea pendekezo lake, tutaendelea kushirikiana naye na Wizara yake ili tuweze kuona kwamba katika ule mkataba wa amani tuliozungumza asubuhi na katika Itifaki za kutekeleza Azimio la Dar es Salaam masuala haya ya watoto yanapewa umuhimu unaostahili.

Tumepewa pia ushauri kwamba katika Chuo cha Diplomasia tuweze kuendeleza wanafunzi kwa ngazi ya Stashahada na Diploma. Mheshimiwa Kumchaya, alitupa ushauri huo, tunaupokea na tutauzingatia wakati tunapitia mitaala ya Chuo kile na programu nyinginezo.

Kuna suala pia limejitokeza kuhusu umiliki wa Chuo cha Diplomasia. Chuo hiki kinamilikiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Msumbiji na hii inatokana na Mkataba ambao tulitia sahihi mwaka wa 1978. Lakini hivi sasa mazingira yanaendelea yakibadilika, uendeshaji wa Chuo tumeutazama, upya. Kwa hiyo, nadhani katika mkutadha huo tutaendelea kutathimini Mkataba huo na tutaweza kushughulikia yale matatizo ambayo yamejitokeza.

Kulikuwa na hoja ya upatikanaji wa hati miliki za viwanja vya Chuo hiki, labda niseme kwamba tunazo hati, ninazo namba za hati hizi naweza kuzitoa baadaye. Labda niseme tu kwamba, tunahati ya kiwanja Na.3 na Na.8 na viwanja hivi tayari vina majengo na hati tulizonazo, tunahati Na. 186099/47, kiwanja Na.7 kina hati, hati yake ni 186099/42 na hii hati tumeipata. Hati ya kiwanja Na.6 ipo katika hatua ya mwisho ya kurekebishwa na tunatumaini kwamba tutapata hati hii katika muda sio mrefu.

Mheshimiwa Spika, tumepata ushauri kwamba tuchukue au tutafute eneo lingine kwa ajili ya upanuzi wa Chuo cha Diplomasia, nadhani huo ni ushauri ambao tutautazama kwa kuzingatia malengo tuliyonayo ya kukiimarisha Chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, katika hoja ambazo tumezipokea, ipo hoja moja ambayo nadhani sikuitizama wakati najibu mchango wa Mheshimiwa Nsanzugwanko na hoja hii ilihusu Kituo cha Kiswahili cha Addis Ababa kitaanza kujengwa lini? Kama ambavyo nimeshasema hapa, Kiswahili hivi sasa kinatumika katika Vikao hasa vya Wakuu wa Nchi katika Mikutano ya Umoja wa Afrika na Tanzania tumechukua jukumu hilo sisi la kukikuza na kukilea Kiswahili ili kiweze kutumika kimataifa.

Mpango huu wa kuanzisha Kituo cha Kiswahili Addis Ababa ni mpango wa Wizara yangu na tumeanza kwa kweli kujitayarisha kwa ajili ya kujenga Kituo hicho, hasa ikizingatiwa kwamba pale Addis Ababa ziko nchi nyingi ndiyo Makao Mkuu ya Umoja wa Afrik na nchi nyingi zimeonyesha hamu ya kutaka kujifunza Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, kKama vile ambavyo tunajitayarisha kuchukua nafasi zilizojitokeza huko Libya, Rwanda Burundi na *DRC* kwa ajili ya kufundisha Kiswahili, azma ya kuwa na Kituo kama hiki ni azma ambayo tungependa kuitekeleza hivi karibuni na kufuatana na upatikanaji wa nyenzo, nadhani tutakuwa tunaweza kuanza, tunamshukuru Mheshimiwa kwa hoja yake hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ambayo wenzangu wameyatoa hasa walipokuwa wakizingatia michago iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, kulikuwa na hoja nyingine hapa ambayo ni ya Mheshimiwa Mporogomyi na yenyewe ilikuwa inahusu haja ya kuboresha mazingira katika Balozi zetu kwa maana kwamba wapo Mabalozi, wapo wafanyakazi, lakini wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Katika kitatu chetu cha hotuba tumeeleza kwamba tunao mpango wa muda mrefu, eneo mojawapo la mazingira ya kazi ambalo tunaliboresha ni ujenzi au ununuzi wa majengo na kama tulivyosema, kazi hiyo tumeshaianza. Lakini tumeweka pia vitendea kazi, tumeweza kuangalia hata posho wanazozipata wafanyakazi wetu na tunaendelea na suala hilo. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mporogomyi kwamba

tutaendelea kuboresha mazingira ili wote tuweze kufanya kazi vizuri zaidi na kuweza kufanya kwa tija.

Kulikuwa na suala la uanachama wa nchi yetu katika mashirika mbalimbali. Hivi sasa nchi yetu ipo ndani ya *SADC*, lakini pia ipo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, nina imani hili pia litakuja kutolewa maelezo zaidi na watoa hoja wenzangu watakaokuja, Waheshimiwa Mawaziri. Lakini niseme suala hili kwa upande wa Tanzania sisi tunalitazama kwamba, uanachama wetu ndani ya Mashirika haya kama ni suala la maslahi ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tulipoingia *SADC* na kwa kweli *SADC* tunaweza kusema ni mtoto aliyezaliwa hapa Tanzania. Kulikuwa na hoja za Nchi za Mstari wa Mbele kwa wakati ule kuweza kuona tunafanya nini ili kuzisaidia nchi ambazo zinatuzunguka na kwa wakati ule nchi ambazo zilikuwa zimekabwa koo na Afrika ya Kusini na nchi ambazo zilikuwa zinaathiriwa na masuala ya ukoloni.

Kwa hiyo, sisi tulikuwa ni waanzilishi wamojawapo. Kwa hiyo, tumeendelea kuwepo, lakini baada ya kupatikana kwa uhuru katika nchi zile ambazo tulikuwa tunazipigania, ilionekana uhuru ule ni lazima uimarishwe na mikakati ya kiuchumi ndiyo maana Jumuiya hii ikageuka sasa nakujielekeza katika maeneo ya kiuchumi. Kwa hiyo, tutaendelea kuwepo kwa sababu tunaamini kwamba maslahi yetu kiuchumi yatatizamwa ndani ya *SADC*. Lakini pia iko Jumuiya Afrika Mashariki. Tumo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na penyewe maslahi yake tunayajua. Lakini ikumbukwe kwamba, kwa hatua zinazokwenda hivi sasa, tunategemea itakapofika mwaka 2013, tutakuwa tumepiga hatua kubwa ndani ya Jumuiya hii na huenda labda tukawa hata na nchi inayofahamika kama Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, labda inapofika wakati huo, tutaona kwamba tuchague tuwe wapi. Lakini suala hili la kuwa katika vikundi mbalimbali vya ushirikiano, ni suala ambalo kwa kweli lina misingi yake hasa kwenye maslahi ya kiuchumi. Itakumbukwa kwa mfano katika siku za nyuma kabisa katika miaka ya sitini, nchi kama Rhodesia au kama *Nyasaland* ni nchi ambazo zilikuwa zinachukuliwa kwamba ziko Afrika ya Kati. Lakini hivi sasa utaona mwingiliano wa kiuchumi upo sana katika eneo la Afrika ya Kusini na kwa upande kidogo wa kaskazini utatukuta sisi Tanzania.

Nchi kama Burundi na Rwanda sasa hivi zinafikiria kutaka kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lakini Burundi sio nchi ambayo unaweza ukasema iko Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tunachosema hapa ni kwamba Tanzania itaendelea kuimarisha mchango wake katika Jumuiya hii, itaendelea kufuatilia maslahi yake, lakini pia itazingatia azma zinazojitokeza ,kwa mfano ndani ya Umoja wa Afrika wa kutaka makundi haya yawe na tija zaidi.

Kwa hiyo, mimi nadhani hili suala lisitufunge na wala lisitufanye tukawa tunajibana sana kwamba tuwe *SADC* au tuwe Afrika Mashiriki. Kadri harakati za kuungana zinavyoendelea utakuta labda wala hakuna haja ya kujiuliza suala hilo.

Mheshimiwa Spika, nadhani nitakuwa nimejibu yote ambayo wenzangu hawakuyagusia na kama kuna lololeteljingine ambalo nimeliacha, nadhani litajitokeza, lakini kwa mujibu wa dondoo niliyokuwanayo, hapa nadhani nimegusa yale yote ambayo hawakuweza kuyagusia.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge, kama ulivyo utaratibu, hoja iliyo mbele yetu itaamuliwa baada ya kazi Kamati ya Matumizi na kwa hiyo, kwa hatua hii kabla hatujaingia hatua hiyo, sasa ningeomba kuwahoji.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 34 – WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA**

Kifungu cha 1001- *Administration and General* ... ... ... ... ... ... Sh. 4,318, 908,300/=

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nimshukuru Waziri na timu yake yote kwa yale waliyotueleza, lakini pamoja na hiyo, katika *Vote 34, programme 10, sub-vote 1001*, ningependa kupata maelezo zaidi kuhusu maeneo ambayo nilichangia asubuhi kwa maandishi na pia yamechangiwa kwa kirefu na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amegusia juu juu tu, kuhusu tatizo la udhibiti wa fedha za walipa kodi zinazokwenda kwenye Balozi zetu nje ya nchi. Tatizo hili najua kabisa kwamba halimhusu Waziri, Manaibu wake wala Katibu Mkuu, kwa sababu najua wote ni watu wapya lakini Serikali ni moja. Mambo haya tumeyazungumza siku nyingi, yanaendelea kuwepo na leo tumeyauliza, lakini hatupewi mkakati, ndiyo sababu napenda kuliulizia na kupata maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja tu na nimeleta taarifa nzima ya *Auditor* na nimefanya kazi ya kupekua taarifa za *audit* toka mwaka 2000 mpaka 2004, ndiyo taarifa za *Auditor General* ambazo zipo. Hali hii inatisha na hatuambiwi mkakati maalum, nilitegemea kwamba angalau tutajibiwa kwamba wana hatua hii wanachukua kwa sababu Serikali ni mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano rahisi tu ni katika Ubalozi wetu wa Lilongwe, lakini hali inafanana katika Balozi zote na nina *document* zote hapa. Katika mfano huu wa Lilongwe, mtu anapewa fedha *imprest* ya zaidi ya milioni 100 anakwenda kununua gari kwa *imprest*. Sijawahi kusikia popote duniani kwamba fedha zinatolewa *imprest* kwenda kununua *unit* ambayo inajulikana kwamba kuna taratibu ambazo zingeweza kutumika na gari lililonunuliwa isitoshe lina kilometa 867. Taarifa hii ni ya mwaka 2004 ndiyo taarifa ya *Auditor* iliyoko. Tungetegemea kwamba leo sasa kinafanyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa kaa kwanza. Labda kwa faida ya Kamati, umesema tu mtu, nani alitumwa sasa? Hata kama humtaji jina, hana hadhi? Kwa sababu hatuwezi kubainisha tatizo ni nini kwa sababu alitumwa kutoka Dar es Salaam au kutoka wapi?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Jina la mtu lipo, ni Afisa wetu anaitwa Mwanjabala, sina hakika na *title* yake kwa sababu kwenye ripoti haitajwi sana. Lakini haya yote yaliyohusika katika Ofisi ya Lilongwe karibu yote yanamhusu huyu mtu mmoja. Kuna *anomalies* nyingi ambazo zimetajwa na *Auditor General* na analalamika.

Kwa taarifa niliyonayo, mpaka hapa tulipo, vitu hivi vyote havijapatiwa ufumbuzi wala jibu. Sasa inatutisha na ndiyo sababu tunapoona na kuomba kitu gani kifanyike, sio tu kwa Ubalozi huu tunatumia mfano huu kwenda kote kwingine na mfano huu unaweza kuona katika Ubalozi wetu wa Milan, ambapo Ubalozi au *consulate* yetu ya Milan imekaa na fedha zaidi ya Shilingi milioni 200 kwa mwaka mzima, 2002 kwenda 2003. Lakini umekaa pia mwaka 2003 kwenda 2004 zaidi Shilingi milioni 200, mtu anakaa nazo tu. Ni kinyume na taratibu za Serikali.

Sasa tunapouliza haya, tunategemea kwamba tutaambiwa tumetumia utaratibu huu au sasa tume-*establish system* yetu ni hii na hii. Sasa bila kupata haya, mimi nadhani maswali yetu hayakujibiwa, Waziri hakusema kitu kwenye hotuba yake kuhusu namna ya udhibiti, lakini tuna taarifa za hivi na *Auditor General* anasema hawa watu wachukuliwe hatua, hatujii walichukuliwa hatua gani, hatuambiwi.

Mheshimiwa Spiia, Wizara hii sasa hivi inaomba zaidi ya Shilingi bilioni 52, haiwezekani Bunge hili tukaendelea kupitisha kila mwaka tunalalamika, *Auditor General* analalamika, lakini hatupewi taarifa sahihi hapa ndani. Tunapopitisha fedha za walipa kodi, ni vyema tukajua kabisa kwamba, taratibu zetu ni moja, mbili, tatu. Je, Wizara inatuambia nini kuhusu utaratibu huu?

Lakini ya pili, tumeweka sheria yetu, *Public Procurement Act* na tumeuliza katika hotuba yetu ya Upinzani, hakuna jibu linalotolewa. Je, hiyo *Act* inahusu na Balozi zetu au zinahusu tu ndani? Kama hazihusu huko nje, sasa hawa huko nje wanatumia utaratibu gani na tunadhibiti vipi hela hizi tunazozitoa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni *details* kama mtu anahitaji. Ukiniruhusu ninaweza nikasoma, lakini sitaki, muda wangu ni dakika tano siwezi kuingia kwa undani. Lakini *imprest* moja nyingine ambayo mtu huyu amepewa sijui ni mwanaume au mwanamke lakini anaitwa G. Mwanjabala, amepewa *USD* 194,600 amekwenda kununua *unit* mbili za gari na kompyuta, alitoka Malawi kwenda Dubai....*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa dakika tano zimekwisha sasa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mhesimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Ningependa nipate maelezo ya kina.

**MWENYEKITI:** Hoja zako ni za msingi na namwomba Mheshimiwa Waziri atupe faraja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa masuala ambayo Mheshimiwa Dr. Slaa ameyazungumzia. Kwanza, niseme kwamba Wizara yetu inazingatia taratibu za matumizi ya fedha ambazo zimewekwa na Serikali, Sheria aliyoizungumzia. *Public Procurement Act*, inahusu Serikali kwa ujumla, hapa ndani na pia kwa Balozi zetu nje ya nchi. Niseme pia kwamba, kuhusiana na hii Sheria, sisi tumefanya mafunzo ili wafanyakazi wa Balozi zetu ziweze kuelewa *Public Procurement Act* inahusu nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba, sheria hii ilipitishwa na Bunge hili, lakini hata hivyo ilichukua muda mrefu kuweza kutekelezeka na kulikuwa na vipengele mbalimbali ambavyo vilihitaji kuangaliwa upya. Hii ni kuonyesha kwamba ilikuwa ni Sheria mpya na ilituchukua muda kuweza kuitekeleza.

Lakini hii haimaanishi kwamba ilikuwa haitumiki katika Balozi zetu, imekuwa ikitumika na hoja anayoizungumzia Mheshimiwa Dr. Slaa ya Lilongwe hii ni hoja ambayo sisi wenyewe kama Wizara tuliikubali ndani ya Wizara na itakumbukwa kwamba tulikuja kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali na tulimwita huyu mhusika Ndugu George Mwanjabala, alikuja akajieleza na baada ya kujieleza, sasa tunasubiri taarifa ya Mdhibiti Mkuu ya kuweza kubaini ni makosa gani yalifanyika pale. Aina ya makosa ndiyo itakayoamua hatua gani sisi kama Wizara tutaichukua. Kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Dr. Slaa na Bunge lako Tukufu kwamba tunalifuatilia suala hilo kwa utaratibu kusubiri nini kitatokea. *(Makofi)*

Kuhusu, *Consulate* ya Milan, tumeeleza hapa tulipokuwa tukijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwamba hivi sasa tunapitia taratibu za uendeshaji wa *Consulate* hizi. *Consulate* ya Milan pamoja na nyingine kadhaa ni *Consulate* ambazo zimekuwa zikiendeshwa labda na mtu huyo huyo mmoja kwa muda mrefu. Kwa hiyo, sasa hivi tumeona kwamba tuweke utaratibu wa kuzifanyia tathimini, lakini pia kuweka vigezo vitavyotusaidia kuthibiti mapato yanayopatikana.

Lakini kwa upande wa Milan niseme kwamba, kama zilivyo kwa Balozi nyingine kwamba *Consulate* zetu tunazifuatilia tuna utaratibu maalum wa kuweza kupata kile

tunachostahili na kidogo kumwachia yule mwendeshaji. Lakini kwa kuwa kasoro hazikosekani, ndiyo sababu Wizara yangu imeamua kwa dhati sasa kuzipitia upya na kuweka taratibu husika ili tuweze kwenda sambamba na *Public Procurement Act*, lakini pia na usimamizi mzuri wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani hilo limejibiwa. Sheria ni *Public Procurement*, mhusika na Lilongwe yumo katika mchakato wa kuchukuliwa hatua na *Consulate* Milan pamoja na *Consulate* zote inafanyiwa utaratibu ili uweze kufuatwa. Bado Mheshimiwa Dr. Slaa?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru umeliweka kwa ufupi vizuri na mimi sina tatizo na Mheshimiwa Waziri kwa sababu ni wageni katika Wizara hii. Kwa hiyo, sina sababu ya kukataa hayo wanayosema. Lakini ningependa niondolewe wasiwasi kwamba haya aliyoyasema yanaweza kutupa matumaini tu tunapokuwa na uhakika na mpango walionao.

Kwa mfano, mambo mengi ya ununizi hata ya ujenzi na hapo nimesema kwamba hii hali ya matumizi mabaya inajitokeza kwenye maeneo mengi. Sasa kuna fedha zimejifutika hapa, lakini hatuna kitabu cha nne kwa mfano majengo mengi yanajengwa, lakini hatujui fedha hizo zilizotengwa kwa majengo ziko wapi. Sasa hii haitupi imani kwamba haya aliyosema Mheshimiwa Waziri waliyafanyia kazi wakayaona au labda atupe tu maelezo kwamba wana utaratibu gani? Huwezi kuwa na majengo mengi najua na mimi juzi nilikua India, nimeona jengo letu ni kubwa sana, lakini nikitafuta hapa silioni liko wapi na labda nitauliza baadaye hilo.

Lakini kuna majengo karibu kila mahali sasa ukiniambia *Procurement Act* mtaifuata wakati sioni kwenye Kitabu cha Nne kwamba kuna fedha zilizotengwa kwa kazi hizo, mimi nadhani ni utaratibu mzima. Labda Waziri anihakikishie kwa kunipa maelezo kwamba: Je, mfumo mzima wa jinsi tunavyopeleka fedha zetu na kazi zinazofanyika kwenye Balozi zetu kama zitaandaliwa upya na labda tutaletewa utaratibu huu tukauona na sisi nitaridhika vilevile.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile *Public Procurement Act* ipo, kwa yale maeneo ambayo tumekuwa tukiamua kujenga tumekuwa tukifuata *Public Procurement Act*, tutaendelea kufanya hivyo kama nilivyosema yapo maeneo ambayo inawezekana *Act* hii haikufahamika vizuri Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala lililoulizwa hapa kwamba nchi zile ambazo ziliahidi, Mheshimiwa Mporogomyi aliuliza kwamba kumekuwa na ahadi zinazotolewa na nchi zilizoendelea kwa mfano kupitia Mkutano wa Gleneagles, kwamba waliahidi watatusaidia, sasa wanatusaidiaje? Kuna ahadi ambazo hazikutekelezwa. Niseme tu kwamba kwa kawaida tunasema ahadi ni deni. Lakini katika eneo hili la ahadi za wenzetu hawa, sisi ndani ya Wizara yetu tumekua tukiongea nao kupitia taratibu za kidiplomasia na pia tumekuwa tukijaribu kuainisha ile miradi ambayo inaingia katika programu zilizozungumziwa katika Mkutano ule Gleneagles.

Kwa mfano, nchi ya Uingereza imetoa kitabu ambacho kwa bahati mbaya hatuna hapa, lakini imetoa kitabu na nadhani tutajitahidi kukipata ili tuweze kuona taarifa zile zinawafikia vipi Waheshimiwa Wabunge au zinawafikia vipi sekta zinazohusika. Lakini nchi ya Uingereza kitabu kikionyesha kwamba katika kipindi fulani nchi hiyo itatimiza ahadi yake katika maeneo, kwa mfano katika maeneo ya afya imejielekeza vizuri kwamba kama tunazungumzia haja ya kufanya umaskini uwe historia tufanye nini katika afya. Mojawapo ni kuangalia magonjwa kama UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria na kadhalika. Lakini kwa mfano kwenye eneo la elimu wamejielekeza kulekule kwenye malengo ya milenia ambayo asubuhi kwenye hotuba yangu niliyazungumza. Kwa hiyo, kipo hicho kijitabu na tutajitahidi taarifa hizo kama ilivyo kawaida tulivyosema kwamba tutatoa taarifa za kuwezesha kuchukua fursa hizo za kimataifa tutakitafuta na tutaweka katika utaratibu.

Mheshimiwa Spika, lakini hivi karibuni kwa mwezi huu huu wa Julai kulikuwa na Mkutano wa nchi hizi zinazojiita *G8* na ambazo pia walipitia maeneo mbalimbali waliyoyatolea ahadi toka walipokutana kule *Gleneagles*. Sasa maeneo hayo yapo katika taarifa ambayo tunadhani na yenyewe tunaweza tukaipata, lakini Mkutano huo ulikwisha juzi tu tarehe 16 Julai, 2006. Sina shaka na matokeo ya Mkutano huo yatakuwa ni kujielekeza katika maeneo yale ambayo waliahidi. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya kazi na Balozi zilizoko hapa ili tuangalie nini tunaweza kushirkiana nao katika kuhakisha kwamba ahadi walizozitoa wanazitimiza na sisi tuna nufaika nazo.

Mheshimiwa Spika, kulitolewa hoja hapa na hii kweli niseme sio hoja, niseme tu ulikuwa ni ushauri na tunaupokea vizuri, huu ni ushauri ambao umetolewa na Mheshimiwa Membe, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Yeye ametushauri kwamba Chuo chetu kiweze sasa kuwa ni Kituo cha kushughulikia masuala ya migogoro na kuleta utengamano katika nchi za Maziwa Makuu. Nadhani huu ni ushauri mzuri sana kwa sababu unakwenda sambamba pia na jitihada za nchi yetu za kuleta amani katika aneo la Maziwa Makuu.

Tumepokea pia ushauri kutoka kwa Mheshimiwa Dr, Batilda Buriani, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Yeye anataka kuona ni hatua gani hasa zinachukuliwa na anapendekeza kwamba tuhakikishe kunakuwa na mipango maalum ya kushughulikia watoto ambao wameingizwa katika migogoro ya kivita na hasa katika eneo hili la Maziwa Makuu. Tunapokea pendekezo lake, tutaendelea kushirikiana naye na Wizara yake ili tuweze kuona kwamba katika ule mkataba wa amani tuliozungumza asubuhi na katika Itifaki za kutekeleza Azimio la Dar es Salaam masuala haya ya watoto yanapewa umuhimu unaostahili.

Tumepewa pia ushauri kwamba katika Chuo cha Diplomasia tuweze kuendeleza wanafunzi kwa ngazi ya Stashahada na Diploma. Mheshimiwa Kumchaya, alitupa ushauri huo, tunaupokea na tutauzingatia wakati tunapitia mitaala ya Chuo kile na programu nyinginezo.

Kuna suala pia limejitokeza kuhusu umiliki wa Chuo cha Diplomasia. Chuo hiki kinamilikiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Msumbiji na hii inatokana na Mkataba ambao tulitia sahihi mwaka wa 1978. Lakini hivi sasa mazingira yanaendelea yakibadilika, uendeshaji wa Chuo tumeutazama, upya. Kwa hiyo, nadhani katika mkutadha huo tutaendelea kutathimini Mkataba huo na tutaweza kushughulikia yale matatizo ambayo yamejitokeza.

Kulikuwa na hoja ya upatikanaji wa hati miliki za viwanja vya Chuo hiki, labda niseme kwamba tunazo hati, ninazo namba za hati hizi naweza kuzitoa baadaye. Labda niseme tu kwamba, tunahati ya kiwanja Na.3 na Na.8 na viwanja hivi tayari vina majengo na hati tulizonazo, tunahati Na. 186099/47, kiwanja Na.7 kina hati, hati yake ni 186099/42 na hii hati tumeipata. Hati ya kiwanja Na.6 ipo katika hatua ya mwisho ya kurekebishwa na tunatumaini kwamba tutapata hati hii katika muda sio mrefu.

Mheshimiwa Spika, tumepata ushauri kwamba tuchukue au tutafute eneo lingine kwa ajili ya upanuzi wa Chuo cha Diplomasia, nadhani huo ni ushauri ambao tutautazama kwa kuzingatia malengo tuliyonayo ya kukiimarisha Chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, katika hoja ambazo tumezipokea, ipo hoja moja ambayo nadhani sikuitizama wakati najibu mchango wa Mheshimiwa Nsanzugwanko na hoja hii ilihusu Kituo cha Kiswahili cha Addis Ababa kitaanza kujengwa lini? Kama ambavyo nimeshasema hapa, Kiswahili hivi sasa kinatumika katika Vikao hasa vya Wakuu wa Nchi katika Mikutano ya Umoja wa Afrika na Tanzania tumechukua jukumu hilo sisi la kukikuza na kukilea Kiswahili ili kiweze kutumika kimataifa.

Mpango huu wa kuanzisha Kituo cha Kiswahili Addis Ababa ni mpango wa Wizara yangu na tumeanza kwa kweli kujitayarisha kwa ajili ya kujenga Kituo hicho, hasa ikizingatiwa kwamba pale Addis Ababa ziko nchi nyingi ndiyo Makao Mkuu ya Umoja wa Afrik na nchi nyingi zimeonyesha hamu ya kutaka kujifunza Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, kKama vile ambavyo tunajitayarisha kuchukua nafasi zilizojitokeza huko Libya, Rwanda Burundi na *DRC* kwa ajili ya kufundisha Kiswahili, azma ya kuwa na Kituo kama hiki ni azma ambayo tungependa kuitekeleza hivi karibuni na kufuatana na upatikanaji wa nyenzo, nadhani tutakuwa tunaweza kuanza, tunamshukuru Mheshimiwa kwa hoja yake hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ambayo wenzangu wameyatoa hasa walipokuwa wakizingatia michago iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, kulikuwa na hoja nyingine hapa ambayo ni ya Mheshimiwa Mporogomyi na yenyewe ilikuwa inahusu haja ya kuboresha mazingira katika Balozi zetu kwa maana kwamba wapo Mabalozi, wapo wafanyakazi, lakini wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Katika kitatu chetu cha hotuba tumeeleza kwamba tunao mpango wa muda mrefu, eneo mojawapo la mazingira ya kazi ambalo tunaliboresha ni ujenzi au ununuzi wa majengo na kama tulivyosema, kazi hiyo tumeshaianza. Lakini tumeweka pia vitendea kazi, tumeweza kuangalia hata posho wanazozipata wafanyakazi wetu na tunaendelea na suala hilo. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mporogomyi kwamba

tutaendelea kuboresha mazingira ili wote tuweze kufanya kazi vizuri zaidi na kuweza kufanya kwa tija.

Kulikuwa na suala la uanachama wa nchi yetu katika mashirika mbalimbali. Hivi sasa nchi yetu ipo ndani ya *SADC*, lakini pia ipo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, nina imani hili pia litakuja kutolewa maelezo zaidi na watoa hoja wenzangu watakaokuja, Waheshimiwa Mawaziri. Lakini niseme suala hili kwa upande wa Tanzania sisi tunalitazama kwamba, uanachama wetu ndani ya Mashirika haya kama ni suala la maslahi ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tulipoingia *SADC* na kwa kweli *SADC* tunaweza kusema ni mtoto aliyezaliwa hapa Tanzania. Kulikuwa na hoja za Nchi za Mstari wa Mbele kwa wakati ule kuweza kuona tunafanya nini ili kuzisaidia nchi ambazo zinatuzunguka na kwa wakati ule nchi ambazo zilikuwa zimekabwa koo na Afrika ya Kusini na nchi ambazo zilikuwa zinaathiriwa na masuala ya ukoloni.

Kwa hiyo, sisi tulikuwa ni waanzilishi wamojawapo. Kwa hiyo, tumeendelea kuwepo, lakini baada ya kupatikana kwa uhuru katika nchi zile ambazo tulikuwa tunazipigania, ilionekana uhuru ule ni lazima uimarishwe na mikakati ya kiuchumi ndiyo maana Jumuiya hii ikageuka sasa nakujielekeza katika maeneo ya kiuchumi. Kwa hiyo, tutaendelea kuwepo kwa sababu tunaamini kwamba maslahi yetu kiuchumi yatatizamwa ndani ya *SADC*. Lakini pia iko Jumuiya Afrika Mashariki. Tumo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na penyewe maslahi yake tunayajua. Lakini ikumbukwe kwamba, kwa hatua zinazokwenda hivi sasa, tunategemea itakapofika mwaka 2013, tutakuwa tumepiga hatua kubwa ndani ya Jumuiya hii na huenda labda tukawa hata na nchi inayofahamika kama Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, labda inapofika wakati huo, tutaona kwamba tuchague tuwe wapi. Lakini suala hili la kuwa katika vikundi mbalimbali vya ushirikiano, ni suala ambalo kwa kweli lina misingi yake hasa kwenye maslahi ya kiuchumi. Itakumbukwa kwa mfano katika siku za nyuma kabisa katika miaka ya sitini, nchi kama Rhodesia au kama *Nyasaland* ni nchi ambazo zilikuwa zinachukuliwa kwamba ziko Afrika ya Kati. Lakini hivi sasa utaona mwingiliano wa kiuchumi upo sana katika eneo la Afrika ya Kusini na kwa upande kidogo wa kaskazini utatukuta sisi Tanzania.

Nchi kama Burundi na Rwanda sasa hivi zinafikiria kutaka kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lakini Burundi sio nchi ambayo unaweza ukasema iko Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tunachosema hapa ni kwamba Tanzania itaendelea kuimarisha mchango wake katika Jumuiya hii, itaendelea kufuatilia maslahi yake, lakini pia itazingatia azma zinazojitokeza ,kwa mfano ndani ya Umoja wa Afrika wa kutaka makundi haya yawe na tija zaidi.

Kwa hiyo, mimi nadhani hili suala lisitufunge na wala lisitufanye tukawa tunajibana sana kwamba tuwe *SADC* au tuwe Afrika Mashiriki. Kadri harakati za kuungana zinavyoendelea utakuta labda wala hakuna haja ya kujiuliza suala hilo.

Mheshimiwa Spika, nadhani nitakuwa nimejibu yote ambayo wenzangu hawakuyagusia na kama kuna lololeteljingine ambalo nimeliacha, nadhani litajitokeza, lakini kwa mujibu wa dondoo niliyokuwanayo, hapa nadhani nimegusa yale yote ambayo hawakuweza kuyagusia.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge, kama ulivyo utaratibu, hoja iliyo mbele yetu itaamuliwa baada ya kazi Kamati ya Matumizi na kwa hiyo, kwa hatua hii kabla hatujaingia hatua hiyo, sasa ningeomba kuwahoji.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 34 – WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA**

Kifungu cha 1001- *Administration and General* ... ... ... ... ... ... Sh. 4,318, 908,300/=

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nimshukuru Waziri na timu yake yote kwa yale waliyotueleza, lakini pamoja na hiyo, katika *Vote 34, programme 10, sub-vote 1001*, ningependa kupata maelezo zaidi kuhusu maeneo ambayo nilichangia asubuhi kwa maandishi na pia yamechangiwa kwa kirefu na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amegusia juu juu tu, kuhusu tatizo la udhibiti wa fedha za walipa kodi zinazokwenda kwenye Balozi zetu nje ya nchi. Tatizo hili najua kabisa kwamba halimhusu Waziri, Manaibu wake wala Katibu Mkuu, kwa sababu najua wote ni watu wapya lakini Serikali ni moja. Mambo haya tumeyazungumza siku nyingi, yanaendelea kuwepo na leo tumeyauliza, lakini hatupewi mkakati, ndiyo sababu napenda kuliulizia na kupata maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja tu na nimeleta taarifa nzima ya *Auditor* na nimefanya kazi ya kupekua taarifa za *audit* toka mwaka 2000 mpaka 2004, ndiyo taarifa za *Auditor General* ambazo zipo. Hali hii inatisha na hatuambiwi mkakati maalum, nilitegemea kwamba angalau tutajibiwa kwamba wana hatua hii wanachukua kwa sababu Serikali ni mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano rahisi tu ni katika Ubalozi wetu wa Lilongwe, lakini hali inafanana katika Balozi zote na nina *document* zote hapa. Katika mfano huu wa Lilongwe, mtu anapewa fedha *imprest* ya zaidi ya milioni 100 anakwenda kununua gari kwa *imprest*. Sijawahi kusikia popote duniani kwamba fedha zinatolewa *imprest* kwenda kununua *unit* ambayo inajulikana kwamba kuna taratibu ambazo zingeweza kutumika na gari lililonunuliwa isitoshe lina kilometa 867. Taarifa hii ni ya mwaka 2004 ndiyo taarifa ya *Auditor* iliyoko. Tungetegemea kwamba leo sasa kinafanyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa kaa kwanza. Labda kwa faida ya Kamati, umesema tu mtu, nani alitumwa sasa? Hata kama humtaji jina, hana hadhi? Kwa sababu hatuwezi kubainisha tatizo ni nini kwa sababu alitumwa kutoka Dar es Salaam au kutoka wapi?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Jina la mtu lipo, ni Afisa wetu anaitwa Mwanjabala, sina hakika na *title* yake kwa sababu kwenye ripoti haitajwi sana. Lakini haya yote yaliyohusika katika Ofisi ya Lilongwe karibu yote yanamhusu huyu mtu mmoja. Kuna *anomalies* nyingi ambazo zimetajwa na *Auditor General* na analalamika.

Kwa taarifa niliyonayo, mpaka hapa tulipo, vitu hivi vyote havijapatiwa ufumbuzi wala jibu. Sasa inatutisha na ndiyo sababu tunapoona na kuomba kitu gani kifanyike, sio tu kwa Ubalozi huu tunatumia mfano huu kwenda kote kwingine na mfano huu unaweza kuona katika Ubalozi wetu wa Milan, ambapo Ubalozi au *consulate* yetu ya Milan imekaa na fedha zaidi ya Shilingi milioni 200 kwa mwaka mzima, 2002 kwenda 2003. Lakini umekaa pia mwaka 2003 kwenda 2004 zaidi Shilingi milioni 200, mtu anakaa nazo tu. Ni kinyume na taratibu za Serikali.

Sasa tunapouliza haya, tunategemea kwamba tutaambiwa tumetumia utaratibu huu au sasa tume-*establish system* yetu ni hii na hii. Sasa bila kupata haya, mimi nadhani maswali yetu hayakujibiwa, Waziri hakusema kitu kwenye hotuba yake kuhusu namna ya udhibiti, lakini tuna taarifa za hivi na *Auditor General* anasema hawa watu wachukuliwe hatua, hatujii walichukuliwa hatua gani, hatuambiwi.

Mheshimiwa Spiia, Wizara hii sasa hivi inaomba zaidi ya Shilingi bilioni 52, haiwezekani Bunge hili tukaendelea kupitisha kila mwaka tunalalamika, *Auditor General* analalamika, lakini hatupewi taarifa sahihi hapa ndani. Tunapopitisha fedha za walipa kodi, ni vyema tukajua kabisa kwamba, taratibu zetu ni moja, mbili, tatu. Je, Wizara inatuambia nini kuhusu utaratibu huu?

Lakini ya pili, tumeweka sheria yetu, *Public Procurement Act* na tumeuliza katika hotuba yetu ya Upinzani, hakuna jibu linalotolewa. Je, hiyo *Act* inahusu na Balozi zetu au zinahusu tu ndani? Kama hazihusu huko nje, sasa hawa huko nje wanatumia utaratibu gani na tunadhibiti vipi hela hizi tunazozitoa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni *details* kama mtu anahitaji. Ukiniruhusu ninaweza nikasoma, lakini sitaki, muda wangu ni dakika tano siwezi kuingia kwa undani. Lakini *imprest* moja nyingine ambayo mtu huyu amepewa sijui ni mwanaume au mwanamke lakini anaitwa G. Mwanjabala, amepewa *USD* 194,600 amekwenda kununua *unit* mbili za gari na kompyuta, alitoka Malawi kwenda Dubai....*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa dakika tano zimekwisha sasa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mhesimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Ningependa nipate maelezo ya kina.

**MWENYEKITI:** Hoja zako ni za msingi na namwomba Mheshimiwa Waziri atupe faraja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa masuala ambayo Mheshimiwa Dr. Slaa ameyazungumzia. Kwanza, niseme kwamba Wizara yetu inazingatia taratibu za matumizi ya fedha ambazo zimewekwa na Serikali, Sheria aliyoizungumzia. *Public Procurement Act*, inahusu Serikali kwa ujumla, hapa ndani na pia kwa Balozi zetu nje ya nchi. Niseme pia kwamba, kuhusiana na hii Sheria, sisi tumefanya mafunzo ili wafanyakazi wa Balozi zetu ziweze kuelewa *Public Procurement Act* inahusu nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba, sheria hii ilipitishwa na Bunge hili, lakini hata hivyo ilichukua muda mrefu kuweza kutekelezeka na kulikuwa na vipengele mbalimbali ambavyo vilihitaji kuangaliwa upya. Hii ni kuonyesha kwamba ilikuwa ni Sheria mpya na ilituchukua muda kuweza kuitekeleza.

Lakini hii haimaanishi kwamba ilikuwa haitumiki katika Balozi zetu, imekuwa ikitumika na hoja anayoizungumzia Mheshimiwa Dr. Slaa ya Lilongwe hii ni hoja ambayo sisi wenyewe kama Wizara tuliikubali ndani ya Wizara na itakumbukwa kwamba tulikuja kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali na tulimwita huyu mhusika Ndugu George Mwanjabala, alikuja akajieleza na baada ya kujieleza, sasa tunasubiri taarifa ya Mdhibiti Mkuu ya kuweza kubaini ni makosa gani yalifanyika pale. Aina ya makosa ndiyo itakayoamua hatua gani sisi kama Wizara tutaichukua. Kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Dr. Slaa na Bunge lako Tukufu kwamba tunalifuatilia suala hilo kwa utaratibu kusubiri nini kitatokea. *(Makofi)*

Kuhusu, *Consulate* ya Milan, tumeeleza hapa tulipokuwa tukijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwamba hivi sasa tunapitia taratibu za uendeshaji wa *Consulate* hizi. *Consulate* ya Milan pamoja na nyingine kadhaa ni *Consulate* ambazo zimekuwa zikiendeshwa labda na mtu huyo huyo mmoja kwa muda mrefu. Kwa hiyo, sasa hivi tumeona kwamba tuweke utaratibu wa kuzifanyia tathimini, lakini pia kuweka vigezo vitavyotusaidia kuthibiti mapato yanayopatikana.

Lakini kwa upande wa Milan niseme kwamba, kama zilivyo kwa Balozi nyingine kwamba *Consulate* zetu tunazifuatilia tuna utaratibu maalum wa kuweza kupata kile tunachostahili na kidogo kumwachia yule mwendeshaji. Lakini kwa kuwa kasoro hazikosekani, ndiyo sababu Wizara yangu imeamua kwa dhati sasa kuzipitia upya na kuweka taratibu husika ili tuweze kwenda sambamba na *Public Procurement Act,* lakini pia na usimamizi mzuri wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani hilo limejibiwa. Sheria ni *Public Procurement,* mhusika na Lilongwe yumo katika mchakato wa kuchukuliwa hatua na *Consulate* Milan pamoja na *Consulate* zote inafanyiwa utaratibu ili uweze kufuatwa. Bado Mheshimiwa Dr. Slaa?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru umeliweka kwa ufupi vizuri na mimi sina tatizo na Mheshimiwa Waziri kwa sababu ni wageni katika Wizara hii. Kwa hiyo, sina sababu ya kukataa hayo wanayosema. Lakini ningependa niondolewe wasiwasi kwamba haya aliyoyasema yanaweza kutupa matumaini tu tunapokuwa na uhakika na mpango walionao.

Kwa mfano, mambo mengi ya ununuzi hata ya ujenzi na hapo nimesema kwamba hii hali ya matumizi mabaya inajitokeza kwenye maeneo mengi. Sasa kuna fedha zimejifutika hapa, lakini hatuna kitabu cha nne kwa mfano majengo mengi yanajengwa, lakini hatujui fedha hizo zilizotengwa kwa majengo ziko wapi. Sasa hii haitupi imani kwamba haya aliyosema Mheshimiwa Waziri waliyafanyia kazi wakayaona au labda atupe tu maelezo kwamba wana utaratibu gani? Huwezi kuwa na majengo mengi najua na mimi juzi nilikua India, nimeona jengo letu ni kubwa sana, lakini nikitafuta hapa silioni liko wapi na labda nitauliza baadaye hilo.

Lakini kuna majengo karibu kila mahali sasa ukiniambia *Procurement Act* mtaifuata wakati sioni kwenye Kitabu cha Nne kwamba kuna fedha zilizotengwa kwa kazi hizo, mimi nadhani ni utaratibu mzima. Labda Waziri anihakikishie kwa kunipa maelezo kwamba: Je, mfumo mzima wa jinsi tunavyopeleka fedha zetu na kazi zinazofanyika kwenye Balozi zetu kama zitaandaliwa upya na labda tutaletewa utaratibu huu tukauona na sisi nitaridhika vilevile.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile *Public Procurement Act* ipo, kwa yale maeneo ambayo tumekuwa tukiamua kujenga tumekuwa tukifuata *Public Procurement Act,* tutaendelea kufanya hivyo kama nilivyosema yapo maeneo ambayo inawezekana *Act* hii haikufahamika vizuri na sio tu kwenye Balozi zetu, hata ndani. Tutaendelea kuimarisha na namhakikishia kwamba tutaifuata kwa sababu na sisi tuna maslahi makubwa sana kuhakikisha kwamba tunatumia vizuri fedha hizi ili tufikishe pia azma yetu ya kuzipatia Balozi zetu majengo na vitendea kazi vingine.

**MHE. BALOZI HAMIS S. KAGASHEKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru sana Waziri amejaribu kujibu hoja kama tulivyoziweka, lakini bado sijaridhika na ningependa nipate ufafanuzi. Kwa mfano, nimezungumza juu ya suala la wastaafu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kagasheki fungu.

**MHE. BALOZI HAMIS S. KAGASHEKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza juu ya *Vote* 34, *Programme* 10, *Sub-vote* 1001 na nazungumzia *Basic Salary and Pensionable Post* hapo, ambayo ni *Sub-vote* 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia leo asubuhi, nilisema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amewashukuru Mheshimiwa Mstaafu Rais Benjamin W. Mkapa, Mheshimiwa Dr. Salim Ahmed Salim na kadhalika kwa mchango ambao wameufanya nje ya Tanzania na hiyo ni sawa na ni vizuri kwamba tuwashukuru.

Lakini mimi nimesema kwamba walipakodi wa Tanzania wanatumia pesa nyingi kwa Viongozi hawa. Hawa ni viongozi ambao tumekuwa nao na Viongozi ambao nchi za nje zinajua mchango wao. Sasa nimeuliza, sisi Tanzania tunawatumia vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujibiwa nimeambiwa kwamba *Doha Round*, ime-*fail* na kwa hiyo tutatizama. Mimi sikuzungumzia *Doha Round* kwa viongozi hawa. Mimi nilichozungumzia, nimesema kwamba *Doha Round* na ninaelewa kwa sababu kwanza Tanzania haimo katika *Doha Round*. *Doha Round* iko *restricted* kwa nchi kama nane au tisa na Tanzania haimo mle.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilichozungumzia na ambacho naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba hawa viongozi ambao tunao wengi tu, wengi ni wastaafu, wengine wako ndani, wako hata akina Mzee Malecela hapa. Tunawatumia vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wana *experience*, wana uwezo tunapozungumzia juu ya *think tank*, tunapozungumzia juu ya mchango wao katika *input* ya *Policies* mbalimbali bila kujali siasa au nini, lakini, tunawatumia vipi kwa *benefit* yanchi? Hapo ndipo nilipokuwa nataka, Mheshimiwa Waziri kama angeweza kunisadia. Mimi sikuzungumzia *specifically* kuhusu *Doha Round*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia *generally* tunawatumia kwa namna gani kwa sababu hapa tunaona kwamba umewashukuru, lakini kwa kutumiwa na nchi za nje ama kutumiwa na Mashirika ya nje ama kutumiwa na *Organizations* za nje. Sasa mimi nasema sisi kama Watanzania kwa wastaafu hawa, tuna-*benefit* namna gani kutokana na *input* ambayo tunawawekea? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo pia nataka pia nipatiwe *clarification* ambayo sikuipata katika *sub-vote* hii, inahusu Ubalozi wa *Holand*. Ubalozi wa Holland mimi nilichosema, sina tatizo na Serikali kufungua Balozi popote wanapotaka kufungua,

wala si jukumu langu ni *Pre-logative* ya Serikali. Lakini, kitu nilichosema ni kwamba, wakati Ubalozi wa *Holland* unafungwa, ni wakati huo huo Ubalozi wa *Rome* ulifungwa na nafikiri kuna Ubalozi mwingine. Lakini *Rome* ilifunguliwa na nyingine zilifunguliwa, Holland mpaka leo haijafunguliwa na Holland pale tuna jengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, mimi nikasema kwamba, hawa watu wa Holland, sisi *Tanzania as a Country* ni *beneficially number one* kwa misaada ambayo tunapata kutoka *Holand*. Katika Afrika nzima, Tanzania ni ya kwanza na katika Ulimwengu mzima, Tanzania ni ya tatu. Sasa kwa nini tusiwe na mahusiano ya karibu na watu hawa? Sikupata jibu. Sasa sijui wao Waholanzi hawataki tukafanya hivyo! Sasa kama hatufanyi hivyo, bado tuna jengo kule limekaa tunaambiwa tunalipangisha. Sasa sijui kama tunaingia katika *Real Estate Business*, sijui!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu, linahusu Mwalimu Nyerere. Hili nitalipigia kelele. Nimezungumza nikasema kwamba *Foreign Policy* ya Tanzania, misingi yake, mahala ambapo ali-*exceed* zaidi ni ya Mwalimu Nyerere. Sasa nikasema hivi, kwa nini… *(hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda umekwisha. Ni dakika tano tu kwenye Kamati. Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Balozi Hamis Sued Kagasheki, amezungumzia hoja ya Viongozi wetu Wakuu wastaafu na wengine. Labda nianze tu kwa vile Mheshimiwa John S. Malecela, yuko hapa, nianze kusema tunamtumiaje.

Kwanza, tunamtumia kwa kuwa yupo ndani ya Bunge hili, nadhani anatusaidia sana. Lakini pia Mheshimiwa John S. Malecela amekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge hili kwa muda mrefu, tumeendelea kumtumia. Tunamtumia kama Kiongozi wa Chama. Lakini nina hakika pia kwa mmoja mmoja kati yetu tunakwenda kumtumia Mheshimiwa John S. Malecela. Amewahi kuwa mmojawapo wa Jopo la watu Mashuhuri na alifanya kazi nzuri wakati ule. Kwa hiyo, tunaendelea kumtumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, Mheshimiwa Benjemin W. Mkapa, Mheshimiwa Dr. Salim Ahmed Salim, Mheshimiwa Jaji Joseph S. Warioba, kwa kweli baada ya wao kuitumikia nchi yetu kwa muda mrefu sana na kwa uadilifu, wameonekana kuwa lulu. Sasa wanapochukuliwa kule nje, sisi hatuwezi kusema kwamba labda kule nje wasiende, watakwenda tutawaunga mkono. Lakini ninaamini yale wanayoyafanya kule yatatusaidia sisi pia. Kwa mfano, Mheshimiwa Benjamin W. Mkapa, yupo katika Jopo la Kuangalia ni namna gani Mapendekezo ya Tume ya Afrika yanaweza yakatusaida. Yupo katika Jopo la kuangalia ni njia gani zitumike hasa katika nchi zetu hizi zinazoendelea kusaidia kuvutia uwekezaji. Kwa hiyo, kwa namna hiyo pia na sisi tutanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatuishii hapo, mimi nachukua ushauri wa Mheshimiwa Balozi Hamis S. Kagasheki kwamba labda kila kinapotokea kile kitu

ambacho badala ya kuwayawaya nje, tunaweza mara moja tukawakimbilia wastaafu hawa wakatusaida. Ni ushauri mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ubalozi wa Uholanzi, sasa hata ndani ya Wizara tumefanya tathmini. Ni kweli Ubalozi wa Uholanzi ulifungwa pamoja na Ubalozi wa Roma. Ubalozi wa Roma ukafunguliwa tena. Lakini hiyo ilikuwa ni hatua na sasa hivi tumefikia hatua ya kuweza kuangalia upya kufungwa kwa Ubalozi wetu na ninamhakikishia kwamba, hili ni jambo sisi ndani ya Wizara tunalifanya na tutakapokuwa tumelikamilisha kwa sababu tunataka kujenga hoja za kiuchumi, nyingine ambazo yeye mwenyewe Mheshimiwa ametuambia kwamba tunapata misaada mikubwa, kuna watu wengi wanatoka Uholanzi kuja huku kwa ajili ya Visa, tayari tuna jengo moja la Ubalozi lililoko kule. Kwa hiyo mazingira ni mazuri na sisi tuko katika mchakato wa kujenga hoja hizo na kutoa ushauri kwa mamlaka husika ili tuweze sasa kuona jinsi ya kuufungua upya Ubalozi wa Uholanzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Mwali Nyerere alikuwa ametoa ushauri kwamba labda umefika wakati wa kuwa na mkakati wa pamoja wa kuuchangia mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waheshimiwa Wabunge watakavyokumbuka, Mfuko huu unachangiwa kwa sababu uko utaratibu. Mimi najua utaratibu wa kudumu unaoendelea ambao kwanza, mwananchi mmoja mmoja anauchangia, lakini kupitia Matawi ya Kamati zilizoko kwenye Wilaya mbali mbali. Mchango huo unaendelea na ninafahamu pia kwamba hata sisi mmoja mmoja kama Wabunge tumeweza kuchangia. Kwa hiyo, tutaendelea. Lakini mawazo ya Mheshimwa Balozi Hamis S. Kagasheki ni mawazo ambayo yanazungumzika kwamba tuweze kuangalia kwa ajili ya kumuenzi Mwana wa Tanzania huyu Mwalimu Neyerere, tunaweza tukapenda kutazama kwamba tufanye nini kwa ujamla wetu, huenda hata tukianzia kama sisi wenyewe Wabunge hapa tuakajiwekea utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kupitia Ofisi ya Spika, hilo pia linawezekana na sisi tutaliunga mkono.

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Balozi bado hajaridhika!

**MHE. BALOZI HAMIS S. KAGASHEKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Sio kwamba sijaridhika, isipokuwa nafikiri kuna *confusion* kidogo. Mimi sikuzungumzia juu ya Mfuko wa Mwalimu Nyerere, wamezungumzia wengine. Mimi nilichozungumzia, nimesema kwamba *Centre For Foreign Relations* katika ku-*develop Foreign Policy* ya Tanzania ingeweza ika-*institute* kitu kama *Annual Lecture on Julius Kambarage Nyerere* na nikasema *infact* pale asubuhi, kwamba, mimi Taasisi ya Mwalimu Nyerere nina *reservations* nayo. Hiyo nimesema na naisema sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu nilichozungumzia ni kwamba Wizara ya *Foreign Affairs* na katika eneo la *Foreign Affairs* ndipo Mwalimu Nyerere alipo-*excel than*

*anywhere else* na *contribution* yake ikawa kubwa na kuipa Tanzania *influence* kuliko hali ya uchumi iliyokuwanayo. Sasa nikasema kwamba, tunaweza tuka-*institute something* ambayo ingeweza ikatusaidia ikachangiwa na mataifa mbalimbali na *Academics* mbalimbali lakini pia hapo tukawa tumekwenda hatua ya mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijazungumzia juu ya Mfuko. Mfuko wamezungumzia watu wengine, lakini mimi nimezungumzia *Ministry of Foreign Affairs* kupitia katika *Centre for Foreign Relations*, hapo ndipo ningetaka nipate *clarifications*. *Centre for Foreign Relations* ina-*develop* vipi *Foreign Policy* ya Tanzania kwa kupitia Misingi ya Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba radhi kwamba nimechanganya hoja yake, lakini ilikuwepo hoja ya kuchangia Mfuko wa Mwalimu Nyerere.

Naomba radhi kwamba nimechanganya. Lakini wazo analolizungumza Mheshimiwa Balozi Hamis S. Kagasheki ni wazo zuri sana, tunalipokea na nadhani ndiyo itakuwa mojawapo ya njia zenye manufaa sana za kumkumbuka Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, tunalipokea. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote 34*, *Programme No.10*, *Sub-vote 1001*, Kifungu 250100 - Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kumhakikishia Mheshimiwa Waziri, sitaki kumpa taabu hata kidogo, lakini nataka ufafanizi wa Serikali. Wakati tunazungumzia suala la hoja ya Rome, Serikali imetoa kauli zifuatazo:- Mawaziri waliotutangulia katika hoja hii walisema kwamba uchunguzi unaendelea na asubuhi vile vile tuliambiwa uchunguzi unaendelea. Lakini, sasa hivi imekuja kauli nyingine kwamba kuna kesi Mahakamani. *Which is which?* Hilo moja nilitaka kujua kwamba Serikali ina kauli ipi hasa, uchunguzi unaendelea au suala liko Mahakamani?

Mhehimiwa Mwenyekiti, pili, kama suala liko Mahakamani, hili suala liloko Mahakamani halihusiani kabisa na *Financial Procedure* au *Finance Act* tunayoizungumzia hapa na *Procurement Act*. Ni utaratibu wa Kiserikali mbali na huu, ni utaratibu wa binafsi, yeye mwenyewe kashughulika na vyombo vyake huko hatuna habari naye, sisi tunazungumzia utaratibu wa Kiserikali wa *Procurement Act* na *Finance Act*.

Mhehimiwa Mwenyekiti, ukitizama kitabu hiki, utakuta Ubalozi wa *Rome* kwa Mfano, mwaka 2005 ulipewa Shilingi milioni 969, mwaka 2005/2006 Shilingi bilioni 1.1, mwaka huu wa 2006 Shilingi bilioni 1.3. Lakini pesa zilizotumika kununulia nyumba ni *three Million Dollars, although officially* ziliandikwa *1.5 million*. Sasa ukitizama Bajeti yenyewe ya miaka hiyo, hazipo pesa, lakini pesa zimepatikana kwenda kununulia nyumba. Sasa tunachouliza, ni kitu kingine tofauti na hicho kilichoko

Mahakamani, hicho cha Mahakamani ni mashitaka ya mtu mwenyewe kukashifiwa. Hatuzungumzi naye sisi. Mimi sina habari naye.

Mimi habari yangu ni utaratibu wa *Finance Act* na *Procurement Act* kwamba haukufuatwa sawasawa na ndio maana hizo pesa hazionekani katika vitabu hivi vya matumizi kwa sababu wao hawana *Development Budget*, wana *Recurrent Budget*. *Recurrent Budget* zote ukizichukua, ukazitizama, hakuna pesa ambazo zinafikia kiwango cha nyumba kilichononulia. Pesa zimetoka wapi? Ndio *Auditor* alilo-*query*. Utaratibu gani uliotumika? Sasa hayo ndiyo tulitaka maelezo sisi tuyapate ili wananchi waweze kuelewa. Sasa Serikali imesema inafanya uchunguzi, inafanya uchunguzi gani na taarifa ya *Auditor* iko tayari na ilikabidhiwa Vyombo vya Dola *immediately* kushughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri aliyotoa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu suala la matumizi ya fedha za ununuzi wa jengo la Ubalozi kule Roma, ni kweli kwamba uchunguzi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchunguzi wa awali ulifanywa na Taasisi yetu ya Kupambana na Rushwa, lakini tufahamu kwamba matukio haya yalitokea Italia na Taasisi yetu isingekuwa na uwezo wa kupata nyaraka mbali mbalizilizoko Italia, hasa zile zilizoko mikononi mwa mwenye nyumba. Mwenye uwezo wa kupata nyaraka hizi ni shirika ambalo linafanya upelelezi wa masuala ya rushwa kule Italia. Sasa kinachofanyika sasa hivi ni mashirikiano ya kidiplomasia kati ya Shirika letu la Kupambana na Rushwa na Shirika la Kupambana na Rushwa la Italia kwa kifupi *AACC* ili kwa upande wa nyaraka zilizoko kwa mwenye nyumba, Shirika la Italia lifanye uchunguzi na ukikamilika, likabidhi nyaraka hizo au matokeo ya uchunguzi huo kwa TAKURU. Kwa kifupi, hali hii ndiyo tuliyofikia kwa maana ya sehemu ya uchunguzi iliyobaki.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwamba sasa Serikali imekuja na kauli. Lakini tunaiomba sana Serikali isipoteze muda wakati taarifa wanazo. Wamekuja Mawaziri wametoa taarifa tofauti kila wakati, kumbe taarifa ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanataka kujua taarifa, sisi Wabunge tunataka kujua taarifa, wala hatuna ugomvi na Serikali, ni kufuata utaratibu. Tumemchelewesha Waziri kumbe taarifa ipo. Kwa hiyo, ningeomba Serikali iwe *consistent* katika kutoa taarifa ili wananchi wajue juu ya masuala ya matumizi yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, sidhani kama kuna maelezo ya ziada.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 1002 – *Finance and Accounts* ... Sh. 473,130,800/=
Kifungu cha 1003 – *Foreign Affairs Office Zanzibar*... ... ... ...Sh. 229,327,300/=
Kifungu cha 1004 – *Policy and Planning*... ... Sh. 479,924,600/=
Kifungu cha 1005 – *International Cooperation*... ... ... ... Sh. 1,194,629,200/=
Kifungu cha 1006 – *Europe and America* ... ...Sh. 335,183,800/=
Kifungu cha 1007 – *Asia and Australia* ... ... Sh. 331,062,800/=
Kifungu cha 1008 – *Africa and Middle East*... Sh. 2,169,794,600/=
Kifungu cha 1009 – *Regional Cooperation* ... Sh.2,207,440,200/=
Kifungu cha 1010 – *Protocol* ... ... ... ... ... Sh. 6,531,098,700/=
Kifungu cha 1011 – *Legal Services* ... ... ... Sh. 275,960,600/=
Kifungu cha 1012 – *Information, Education and Communication* ...195,411,900/=
Kifungu cha 2001 – *Embassy of Tanzania* – Addis Ababa... 897,911,700/=
Kifungu cha 2002 – *Embassy of Tanzania – Berlin*. ... ... ... Sh. 1,179,246,000/=
Kifungu cha 2003 – *Embassy of Tanzania – Cairo* ... ... ... Sh. 681,313,300/=
Kifungu cha 2004 – *Embassy of Tanzania – Kinshasa* ... ... ... ... 698,486,200/=
Kifungu cha 2005 – *Embassy of Tanzania – Abuja*... ... ... ... Sh.753,362,100/=
Kifungu cha 2006 – *High Commission of Tanzania – London*... 1,225,218,300/=
Kifungu cha 2007 – *High Commission of Tanzania – Lusaka*... 781,866,600/=
Kifungu cha 2008 – *Embassy of Tanzania – Maputo*... ... ... ... ...580,720,100/=
Kifungu cha 2009 – *Embassy of Tanzania – Moscow* … … … 1,062,260,900/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2010 – *High Commission of Tanzania – New Delhi*...1,802,862,700/=

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi. Naomba nitumie *vote* hiyo hiyo, *sub-vote* 2010, kifungu kidogo cha 280900 kwa pamoja na 310900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia yote mawili kwa sababu mafungu yalivyopangwa, kwa bahati mbaya hayaonekani ni kitu gani kinafanyika wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wa maandishi, nilikuwa nimemwomba Waziri anisaidie kuhusu ujenzi wa jengo letu la nyumba ya Balozi kule India.

Lakini kabla sijafikia hapo, naomba niwapongeze watu wa Wizara pamoja na Balozi wetu kwa Ofisi nzuri sana waliyotujengea pale *New Delhi - India*, jengo la ghorofa mbili ambalo liko kwenye hatua karibu ya mwisho na ni imani yangu kwamba litapelekewa hela ili iweze kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimesimama pia kwa sababu, wakati tunapata eneo kwa ajili ya hiyo Ofisi, tulikuwa tumepewa ardhi kubwa, lakini tukawa tumedanadana, tumechelewa na tukakosa lile eneo zuri. Sasa tumejenga katika eneo dogo. Wakati huu Ubalozi unatafuta eneo lingine kwa ajili ya Balozi.

Mhehimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naangalia kwenye mafungu, Waziri anisaidie, kwa ajili ya kumalizia jengo la Ubalozi pamoja na nyumba ya Balozi, ni fedha kiasi gani zimetengwa na ziko wapi, kwa sababu hawana kitabu cha nne, imenipa taabu sana kupitia kwenye mafungu haya kugundua hizi fedha zimewekwa wapi!

Sitegemei kwamba jengo lile la ghorofa mbili kwa hatua iliyofikia linaweza kujengwa kwa kifungu chochote kilichoko hapa. Kifungu cha juu ni Shilingi milioni 100.

Mhehimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua hizo hela ziko wapi? Ni kifungu kipi? Kama hazipo kwenye kitabu hiki, huwa zinatoka wapi hizo fedha zilizofanya hiyo kazi? Kama huwa zinatoka nje ya hapa, zinapitishwa na chombo gani? Maana Bunge hili ndilo linalopitisha mambo yote.

Sasa hizo nyingine ambazo haziko hapa, zitakapotolewa wakati mwingine, zinatolewa kwa idhini ya nani? Maana yake kwa taratibu za Fedha hata zingetolewa, basi wangerudi hapa Bungeni kuomba idhini ya fedha ambazo walitumia kama hela fedha zinazotumika zinatumikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nime-*check* kwa mwaka 2004/2005, sioni mahali popote ambapo wameweka fungu kubwa kwa ajili ya kujenga zile ghorofa mbili hatua zile zilizofikia. Nime-*check* pia 2005, sioni pia fungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nauliza, hizi hela zinapitaga wapi? Kama zinapitaga huko, ni kwa utaratibu upi na nani anaidhinisha? Je, utaratibu huu uliojificha, siyo sababu ya haya tuliyoyaona ya ubadhirifu na matumizi mabaya ambayo Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti analalamikia kila mwaka? Je, utaratibu huu utarekebishwa lini? Ninataka hayo maelezo ili niweze kuridhika katika hilo.

**MWENYEKITI:** Sawa, lakini tu nikusaidie Kiswahili, siyo zinapitaga! Ni kupitia wapi. Ndio swali lenyewe. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa suala la Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa. Kwanza, niseme kwamba jengo letu la Ubalozi la India limefikia hatua kubwa na kwamba nadhani katika kipindi kifupi litakuwa limekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la nyumba ya Balozi, hilo ni suala ambalo bado hatujaanza kulitekeleza. Tutakapokuwa tumeliweka katika ule utaratibu wetu wa miaka 15, litakuwa limeonekana katika mipango yetu pia ya kifedha. Kwa hiyo, nataka tu kumwambia Mheshimiwa kwamba kwa lile jengo lililoko litakamilika, hela tulizokuwa tumetenga zitatutosheleza kukamilisha. Lakini kwa ile nyumba ambayo tunakusudia hapo baadaye kujenga tutaweka katika utaratibu huu wa kuomba fedha kupitia Bunge lako tukufu.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kifungu cha 2011 – *Permanent Mission to the UN – New York* ... 3,529,682,200/=
Kifungu cha 2012 – *High Commission of Tanzania – Ottawa... 1,595,246,900/=*
Kifungu cha 2013 – *Embassy of Tanzania* –Paris ... ... ... ... ... 1,345,614,000/=
Kifungu cha 2014 – *Embassy of Tanzania –Beijing ... ... ... ...* 828,978,600/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kifungu cha 2015 – *Embassy of Tanzania – Rome* … … … … 1,398,741,100/=

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote* 2015, kifungu kidogo, 260500 - *Military Procurements, Supplies anda Services*. Tunafahamu kwenye Balozi zetu kuna Waambata wa Kijeshi na huwa ndio wana fungu lao mbali na matumizi. Hii *Procurement* ina husu nini hapa? Nataka ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Nakuomba urudie, haikusikika vizuri.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nasema kifungu 260500 - *Military Procurements*. Kwa kawaida wale Waambata wa Jeshi wana fungu lao mbali na halipitii Wizara hii hapa. Je, hizi fedha za hapa zinazoombwa ni za nini? Kwa nini mwaka 2005 na mwaka 2004 fedha za kifungu hiki hazikuombwa? Pesa kidogo tu, *62 thousand*. Lakini nataka kuona ule utaratibu tu, kama ninavyofahamu, Mwambata wa Kijeshi wana fungu lao mbali. Je, Hii *Military Procurement* inahusu nini hapa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kuhusu kifungu cha 260500 hiyo fedha kidogo sana, hizi Sh. 62,000/= siyo?

**WAZIRI WA MAMBO NJE NA USHIRIKIANO WA MATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kuhusu kifungu hiki anachokizungumzia - *Military Procurement, Supplies and Services*. Nakubaliana naye kwamba hawa wanakuwa na utaratibu wao tofauti. Hizi Sh. 62,600/= Naamini ni za vitu vidogo vidogo ambavyo vinahusiana na utekelezaji wa kazi za kawaida za kila siku. Lakini siyo kwamba ndiyo za kumleta na kumweka pale kama Mwambata wa Jeshi.

**MWENYEKLITI:** Nadhani hii ni kama chai, keki kwa ajili ya Mwambata wa Jeshi, au siyo! *(Kicheko)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kifungu cha 2016 – *Embassy of Tanzania – Stockholm* … … … 978,533,600/=

Kifungu cha 2017 – *Embassy of Tanzania – Tokyo* … … … … 1,521,990,800/=
Kifungu cha 2018 – *Embassy of Tanzania – Washington* … … 2,445,287,600/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kifungu cha 2019 – *Embassy of Tanzania – Brussels*… … … 1,242,499,300/=

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye *Sub-vote* 2019, kifungu kidogo zaidi cha 280900. Kwa sasa hivi, tunavyofahamu Ubalozi wetu ulioko *Brussels* ndio pia unalea Ubalozi wa heshima ulioko *Netherlands*, *The Hague*. Sasa Waziri hapa ametueleza kwamba wako katika hatua ya kufufua Ubalozi ule. Mimi nilitaka nihakikishiwe tu kwamba Je, fedha kama tutakwenda kwenye kufungua Ubalozi huu, wametengewa kifungu kipi? Kwa sababu hapa kuna Shilingi milioni 226 tu za *transfer*. Kwanza sijui kama ndizo hizo huwa zinapelekwa kule kwa sababu mafungu kama tulivyosema hayaonyeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina tatizo pia kwamba kule tuliko na huu Ubalozi wa Heshima, nadhani kuna tatizo pia la udhibiti. Sasa, Je, wakati tunaendelea kusubiri, ule Ubalozi uendelee hivyo? Kwa sababu tuna taarifa ambazo tunazo pia hapa kwamba hata utaratibu wa kawaida wa utendaji kazi wa ule Ubalozi unatia mashaka.

Kwanza, hatujui kama tuna *agreement* na yule Balozi wa Hisani, kwa ajili ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Kwa kuwa hilo linakuwa ni vigumu hata kuweza kusema kwamba tunampelekea fedha kwa utaratibu wa Kiserikali, bado ni *doughtful*, kwa sababu kama hatuna mkataba, sijui tunampelekea fedha kwa misingi ipi! Lakini zaidi ya pale, hata fedha zetu zimekaa kule, pia amekaa nazo na yeye pia. Kinyume cha *Secular* ya Serikali ya mwaka 2003 inayosema *retention* lazima zirudishwe hapa. Waziri amejibu hapa kwa urahisi kwamba tumepungukiwa na maduhuli kwa sababu maeneo mengine huwa fedha hazikusanywi. Huyu amekaa na zaidi ya milioni 200, maduhuli yangekuwaje mengi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajaribu kuyachokonoa haya ili tuwe na uhakika na tunaposema haya, tunataka majibu yasiwe rahisi rahisi. Tungependa tunapouliza, Serikali itupe majibu ya kina. Kwa kuwa tunafanyia utafiti, sisi tunapata taarifa sahihi na tunapenda taarifa sahihi kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa uhakika tu, hizi fedha za Ubalozi huu wa Hisani ziko wapi? Kama huyu ambaye tunaendelea naye utaratibu wake umekuwa *regularized* au vipi ili hela za Serikali ziweze kwenda kule na kama hakuwa *regularize*, hela hizi zinapelekwa kwa kifungu kipi na kwa mamlaka yapi?

**SPIKA:** Peter, huyu ni nani? Huyu ni Balozi Brussels?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ubalozi wetu wa Brussels kwa sasa ndiyo unaohudumia Netherlands kwa sababu kule nadhani kwa

utaratibu wa kawaida kwa kuwa ni Ubalozi wa Hisani, hauna *vote* na kwa hiyo, hauwezi kupelekewa hela.

Kwa hiyo, hapa hatuna *vote* yoyote kwa ajili ya Netherlands. Kwa hiyo, fedha zinapitia pale. Sasa bahati nzuri na mimi naifahamu hii *issue* kwa sababu nilikuwa mwakilishi kule *SADC*. Sasa kwa kuwa haipo, ndiyo ninaulizia kwamba sasa zinapita wapi?

**SPIKA:** Nimekuelewa, nimekuelewa. Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa hoja za Mheshimiwa Slaa kama ifuatavyo: Kwanza ameuliza, hizi fedha zitatosha kufungua Ubalozi wa Uholanzi? Kama nimempata vizuri, tulichokisema ni kwamba, tupo katika kujenga hoja za kuweza kuishauri mamlaka husika ikubali tufungue Ubalozi. Itakapokubali tufungue Ubalozi ndiyo tutaanza utaratibu wa kutengea fedha. Kwa hiyo, hela hizi siyo za ufunguzi wa Ubalozi wa Uholanzi.

Lakini pili, ameuliza Ubalozi wa Heshima, yaani *Honorary Consul* kule Uholanzi kama tunawapelekea pesa. Kwa kweli utaratibu wa *Honorary Consul* hatuwapelekei pesa, wanazokusanya wanaweka kidogo kwa ajili ya kugharamia shughuli zao kwa utaratibu ambao tumejiwekea kwa matumizi yao kwa sababu wanakuwa wanayatunza au wanayahifadhi maslahi yetu kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mheshimiwa Dr. Slaa anasema kwamba tumesema maduhuli yanapungua. Ningependa nisahihishe kwamba, kitu tulichojibu ni kuwa maduhuli hayako sawa kwa kila Balozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilitokana na hoja kwamba je, tunachukua hatua gani kwa wale Mabalozi ambao hawakusanyi maduhuli ya kutosha? Tukasema kwamba kigezo hicho hakipo kwa sababu kinategemea wingi wa watu wanaokwenda kuomba *visa*. Kwa hiyo, upungufu hautatokana na fedha ambayo huyu Balozi wetu wa Heshima amezishika. Lakini kama nilivyosema, tuna utaratibu wa kuweza kuzipata hizo fedha ukitoa zile ambazo anatumia kugharimia shughuli zake za kila siku.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2020 – *Permanent Mission to the UN – Geneva...* Sh.1,766,234,400/=
Kifungu cha 2021 – *Embassy of Tanzania –Kampala...* ... ... ... ... 666,036,100/=
Kifungu cha 2022 – *High Commission of Tanzania – Harare...* 589,289,500/=
Kifungu cha 2023 – *Embassy of Tanzania – Nairobi...* ... ... ... ... 1,187,134,600/=
Kifungu cha 2024 – *Embassy of Tanzania –Riyadh...* ... ... ... 991,366,700/=
Kifungu cha 2025 – *Embassy of Tanzania –Pretoria* ... ... ... ... 822,217,800/=
Kifungu cha 2026 – *Embassy of Tanzania – Kigali...* ... ... ... ... 557,027,400/=
Kifungu cha 2027 – *Embassy of Tanzania – Abu-Dhabi* ... ... ... ... 916,616,200/=

Kifungu cha 2028 – *Embassy of Tanzania – Bujumbura... ... ...* 662,025,700/=
Kifungu cha 2029 – *Embassy of Tanzania – Muscat... ... ... ...* 721,642,600/=
Kifungu cha 2030 – *Embassy of Tanzania – Lilongwe... ... ... ...* 565,112,200/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Hatimaye na kwa furaha, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje sasa aweze kutoa taarifa ya kazi za Kamati.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2006/2007 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe makisio ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA**: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninafurahi kutangaza kwamba Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2006/2007 sasa yamepitishwa rasmi na Bunge hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nakumbushia tu kuhusu Semina ya kesho saa 3.00 Asubuhi na ile ya kesho kutwa, Jumapili saa 5.00 Asubuhi. Ninawaombeni mhudhurie.

Kesho ni Wizara ya Kilimo na kesho kutwa ni kile kitabu *"The Promise"*. Semina hiyo inatolewa na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Zote ni muhimu. Ukiwa hapa Dodoma, utakuwa umejinyima fursa nzuri sana ya uelewa kwa masuala yote mawili.

Kwa kukumbusha tena, wiki ijayo tunaanza Jumatatu tarehe 31 Julai na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Jumanne tarehe 1 Agosti, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto halafu tunaendelea tarehe 2 Agosti, Jumatano Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Mkumbuke tu hivyo ili wale ambao mnataka kuchangia kwenye Wizara hizo mjipange.

Naomba nitoe taarifa kwamba, kesho asubuhi nalazimika kwenye Jimbo la Uchaguzi na nitakuwa huko hadi Jumatatu. Kwa bahati mbaya, mawasiliano ya ndege kutoka Tabora ni magumu sana kwa sababu huwezi kurudi Dodoma, unapelekwa Dar es Salaam tu na ili uende Dar es Salaam unapelekwa kwanza Kigoma. Kwa hiyo, ni safari ya siku nzima. Ndiyo hali halisi ya baadhi ya Mikoa yetu hii na hakuna barabara ya kufika huko ambayo inaaminika. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, siwezi kuwepo Bungeni hadi Jumanne jioni. Nimepanga utaratibu, siku ya Jumatatu tarehe 31 Julai, Mheshimiwa Job Ndugai atashika shughuli za kuendesha Bunge kwa siku nzima mpaka jioni.

Siku ya Jumanne, siku ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto nimeona ni vizuri sana Mheshimiwa Jenista Mhagama aendeshe shughuli za Bunge hadi jioni. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo, nawatakia *weekend* njema na sasa naahirisha Bunge hadi hapo Jumatatu tarehe 31 Julai, saa tatu Asubuhi.

*(Saa 01.09 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 31 Julai, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*